*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Hamsini na Tano – Tarehe 21 Juni, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mbunge wa Arusha Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Joseph Selasini.

Na. 465

**Umuhimu wa Serikali Kuzisimamia Taasisi Binafsi Kulipa Mishahara Stahili**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y MHE. GODBLESS J. LEMA)** aliuliza:-

Mishahara ya Taasisi za Umma hupangwa na Serikali. Utaratibu huo wa Serikali kupanga mishahara ya watumishi wake huathiri pia upangaji na ukadiriaji mishahara katika taasisi binafsi:-

Je, Serikali haioni haja ya kuboresha mishahara yake na kuzielekeza taasisi binafsi kulipa mishahara inayoendana na hali ya maisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri, Mheshimiwa Antony Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha mishahara yake na kuzielekeza taasisi binafsi kulipa mishahara inayoendana na hali ya maisha, Serikali imeunda Bodi ya Kima cha Chini cha Mshahara ambayo hufanya utafiti kwa kuzingatia hali halisi ya maisha na uwezo wa kibajeti wa Serikali na kuwashauri Mawaziri wenye dhamana na masuala ya utumishi wa umma na sekta binafsi katika kupanga kima cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya Mwaka 2004 kama ilivyorekebishwa mwaka 2015 imeanzisha Bodi ya Mishahara ya Sekta Binafsi ambayo ina jukumu la kufanya uchunguzi na kupendekeza kiwango cha kima cha chini cha mshahara na maslahi ya wafanyakazi kwa ujumla. Serikali itaendelea kuiwezesha Bodi ya Mishahara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi pamoja na kuhamasisha majadiliano baina ya waajiri na vyama vya wafanyakazi katika kuboresha maslahi na kukuza tija na uzalishaji sehemu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sekta binafsi, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya Mwaka 2004, imeweka utaratibu kwa waajiri na wafanyakazi kujadiliana na kufunga mikataba ya hali bora mahali pa kazi kwa lengo la kuboresha maslahi yao ikiwemo mshahara na stahiki nyingine. Kupitia utaratibu huu wa kisheria waajiri

katika sekta binafsi wanaruhusiwa kuwalipa viwango vya mishahara hata zaidi ya kiwango kinachowekwa kama kima cha chini cha mshahara pale ambapo wanaona kwa kufanya hivyo itaongeza motisha kwa wafanyakazi wao kufanya kazi kwa bidii na kujituma kwa lengo la kuongeza tija katika kuzalisha mali au kutoa huduma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Selasini, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kama sikosei taarifa ya mwisho ya Bodi hii ilitolewa katika kipindi cha pili cha Awamu ya Nne. Hii ni bajeti ya tatu tunaijadili katika Awamu ya Tano na tunasema katika awamu hii uchumi umekua. Naomba niiulize Serikali, ni lini Bodi hii itatoa ripoti yake ili kuwezesha kupandishwa mishahara ya wafanyakazi ambao hivi sasa hata morali yao inashuka kwa sababu ya hali ngumu ya maisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, pamoja na mishahara, *statutory increments* ambazo ziko kisheria nazo hazitolewi. Ni lini takwa hili la kisheria litatolewa ili Serikali isionekane kwamba inavunja sheria ambayo tumejiwekea wenyewe? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na swali lake la kwanza la lini ripoti ya Bodi ya Mishahara itatoka. Kwa mujibu

wa kifungu cha 35(1) cha Sheria Namba 7 ya Mwaka 2004, Sheria ya Taasisi za Kazi imeelezwa uundwa wa Bodi ya Mshahara ambapo watapewa *teams of reference* na Mheshimiwa Waziri na baadaye kuwasilisha kwa ajili ya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, navyozungumza hivi sasa kwa muda wa tangu mwaka 2015 Bodi hii imeshaundwa na taratibu ambazo zimewekwa ni kuhakikisha kwamba Bodi hii inapewa kwanza mafunzo na kwa mujibu wa sheria wanapewa nafasi ya kufanya kitu kinaitwa *investigation* kabla ya kwenda kumshauri Mheshimiwa Waziri. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, tumetenga fedha kwa ajili ya Bodi hii iweze kufanya kazi, kwa hiyo, naamini fedha hii ikitoka na wakimaliza kazi yao ripoti hii itawasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu *annual increment*, ni dhahiri kwamba na Mheshimiwa Mbunge anafahamu limekuwepo zoezi la uhakiki wa wafanyakazi ambalo kwa kiwango kikubwa sana lengo lake lilikuwa ni kujaribu kutengeneza mfumo mzuri wa utumishi wa umma na kujenga utaratibu mzuri wa Serikali katika kufanya mambo ambayo wamepangwa kwa ajili ya watumishi wa umma na mojawapo likiwa ni hilo la ongezeko la mshahara. Kwa hiyo, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu taratibu hizi zimeshafanyika na zinaendelea basi pale Serikali itakapokuwa tayari kwa maana kibajeti hilo takwa la kisheria litafanyika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ni vizuri Serikali kwa hili la mishahara na stahili za watumishi wakawa tu wakweli. Mfano zoezi la uhakiki limeathiri madaraja kutokupandishwa na watumishi wengine wakastaafu wakati Serikali inaendelea na uhakiki jambo ambalo limeathiri pensheni zao. Naomba nifahamu

Mheshimiwa Naibu Waziri, hawa walioathirika na zoezi hili wakastaafu na pensheni zao zimeathirika Serikali inawafikiriaje ili walipwe stahiki zao kwa sababu wao hawakupenda hilo zoezi lifanyike na wao wameathirika sasa? Naomba nifahamu Serikali inasema nini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zoezi kama hili ambalo lilifanyika mwisho wa siku lazima kutakuwepo changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza. Niseme tu, Serikali ambacho inaweza kukifanya ni ku-*deal* kwa *case by case*. Inapotokea mazingira kama hayo, Ofisi ya Utumishi iko wazi kwa ajili ya kujadiliana na kuona namna bora ya kuwasaidia watumishi hawa wameathirika na mpango wa Serikali wa uhakiki wa vyeti. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba bado nafasi ipo kwa wote ambao wamepitia katika mazingira hayo kufanya majadiliano na Serikali na kuona namna nzuri ya kuweza kurekebisha changamoto hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venance Mwamoto, swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nashukuru kwa kutupa matumaini kwamba kuna siku mshahara utapanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niulize swali dogo kwamba watakapokuwa wanapandisha mishahara, je, watakuwa tayari kuzingatia watu wenye ulemavu hasa wa macho ambao wenyewe huhitaji msaidizi? Wanapolipwa mshahara sawa na wengine wao wanakuwa wanapata mshahara kidogo kwa sababu hauwatoshi. Je, Serikali

itakuwa tayari kuwapa motisha au kuwapa kitu cha ziada ili iwasaidie? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu kwa swali hilo muhimu kutoka kwa Balozi wa wenye Ulemavu wa Uoni wa Macho.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa mtetezi na mpigania haki wa watu wenye ulemavu. Katika hili, kwa sababu mshahara na stahiki na haki za wafanyakazi zinaongozwa kwa mujibu wa sheria, niseme tu kwamba kwa hivi sasa sheria ambayo imewekwa ndiyo utaratibu wake utaendelea kufuatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama unavyofahamu pia kuna Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ambayo inalinda haki zao na kwa namna moja ama nyingine pia kumekuwepo na *incentives* mbalimbali za kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata haki kama watu wengine. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inajali watu wenye ulemavu lakini katika hili la mishahara kwa mujibu wa sheria; sheria yetu inatuongoza katika utaratibu ambao umewekwa hivi sasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka, swali la nyongeza.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana wengi sana pale Tunduma wamejiajiri kwa ajili ya kufanya *escort* ya magari yaliyobeba *copper* kutoka Congo na wamefanya kazi kwa

muda mrefu lakini mpaka sasa hivi hawajapata mikataba kutoka kwenye kampuni hizo. Serikali inasema nini kuhusiana na vijana hao kwa sababu imeonesha kwamba kampuni hizo zinavunja sheria; kwa sababu wamefanya miaka mitatu wengine mpaka miaka nne lakini mpaka leo hawana mikataba kabisa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Frank Mwakajoka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2004, kifungu cha 14 kimetoa sharti la kila mfanyakazi kupewa mkataba. Kama vijana hawa wanaofanya kazi Tunduma hawana mkataba maana yake waajiri wamevunja sheria. Natoa maelekezo kwa Afisa Kazi wa Mkoa wa Songwe kuhakikisha kwamba anakwenda kufanya ukaguzi katika eneo hilo na taarifa itakayotoka tutaifanyia kazi ili vijana hao waweze kupata mikataba ya ajira.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 466

**Madeni ya Wazabuni**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** aliuliza:-

Serikali imeanzisha utaratibu wa kutoa elimu bure na kuanza kutekeleza utaratibu huo kwa kupeleka fedha shuleni kidogo kidogo kulingana na idadi ya wanafunzi husika tangu Oktoba 25, 2015:-

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba shule nyingi za msingi na za sekondari nchini zikiwemo za Mtwara Mjini zilikuwa na madeni mengi ya wazabuni na steshenari?

(b) Je, Serikali inaweza kueleza kuwa madeni hayo yatalipwa kwa utaratibu upi ikiwa fedha zinazotolewa ni kidogo kwa uwiano wa mwezi kwa mwaka husika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa madeni katika shule za msingi na sekondari ambayo yanaanzia mwaka wa fedha 2008/2009 hadi 2016/2017, ikiwa ni madeni ya wazabuni kwa ajili ya chakula cha wanafunzi shuleni na shajara. Katika ya hayo, Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani inadaiwa shilingi milioni 92.4. Madeni hayo ni yale yalikuwepo kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa Mpango wa Elimu bila Malipo Desemba, 2015. Kwa sasa, Serikali imejizatiti kutozalisha madeni, ambapo fedha za chakula na mahitaji mengi zinapelekwa kwenye kila shule moja kwa moja kila mwezi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha Nachuma, swali la nyongeza.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa sababu Serikali imeweza kutambua angalau kwamba kuna shilingi milioni 92.4 ambazo Manispaa ya Mtwara Mikindani inadaiwa, kwa maana ya shule za

msingi na shule za sekondari. Naomba kuuliza maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Shule ya Sekondari Sabasaba, Raha Leo, Chikongola na Shule zote za Msingi za Manispaa ya Mtwara Mikindani zinadaiwa hizi *stationery* kabla Serikali haijaanza utaratibu wa kupeleka elimu bure. Siku za nyuma ilikuwa michango inakusanywa kupitia kwa wazazi *then* zinalipwa *stationery* hizi ambazo zinatumika katika shule za msingi na sekondari. Ni lini Serikali italeta hizi shilingi bilioni 92.4 kwa ajili ya kulipa kwenye hizi shule ambazo zinadaiwa pale Mtwara Mjini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mkuu wa Shule ya Sekondari na Mwalimu Mkuu wa Shule za Msingi ndiyo wanaobeba haya madeni kama yao, ni *declare* tu *interest* nilikuwa Mkuu wa Shule, nafahamu kila Mkuu wa Shule anavyotembea anadaiwa yeye. Je, Serikali inawasaidiaje hawa Wakuu wa Shule za Sekondari na Walimu wa Shule za Msingi ili haya madeni yasionekane kama ni ya kwao yawe ni madeni ya Serikali na Serikali iweze kulipa kwa wakati? Ahsante *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumekiri kwamba Serikali kweli inadaiwa madeni hayo lakini utaratibu wake bado una mchakato ambapo tunahitaji kuyaangalia kwa undani zaidi madeni hayo. Ndiyo maana tumesema kwanza kuanzia Mwalimu Mkuu ajiridhishe na hayo madeni aandike barua kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kwamba nimeridhika kwamba madeni haya ni halali. Mkurugenzi wa Halmashauri

alete tena kwetu tuyaangalie tena baadaye tutapeleka Wizara ya Fedha madeni ambayo tulishajiridhasha tena kwa mara nyingine sisi kwamba hayo ni halali halafu Serikali itaweka utaratibu wake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kwamba tunawasaidiaje Wakuu wa Shule, wao wenyewe hasa wale waliokuwepo na Mheshimiwa Nachuma ulikuwepo na wewe umezalisha kumbe hayo madeni. Sasa wewe utakuwa shahidi mzuri vilevile katika kutuhakikishia kwamba madeni hayo ni halali. Kweli kama waajiriwa wetu Walimu Wakuu tumewakabidhi dhamana kubwa kwanza hatutaki waendelee kuzalisha madeni mengine kwa sababu sasa hivi tunapeleka fedha. Atakayezalisha deni lolote kuanzia sasa hivi itakuwa ni wajibu wake kulilipa kwa sababu tunapeleka hela sasa hivi. Kwa hiyo, kwa yale ya zamani tunaandaa huo mchakato kama nilivyokueleza katika swali la kwanza ili kusudi tuweze kuwaondolea huo mzigo wa madai.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Serikali inatoa elimu ya bure kwa ngazi ya shule ya msingi na kwa kuwa wanafunzi walewale ambao wametoka shule ya msingi wanaenaenda sekondari kwa maana ya *Form I - Form IV* na wanafunzi haohao wanafaulu kwenda *high school.* Kwa sababu hao watoto walikuwa na mazoea ya kutokulipa ada, sasa wanahangaika mitaani kwa kukosa ada ya kwenda *Form V*. Je, nini kauli ya Serikali kuwasaidia watoto hawa ambao walipata msaada kutoka shule ya msingi wamefanikiwa kwenda sekondari na sasa wamefaulu kwenda *high school* na hawana uwezo wa kulipa ada? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, hili swali linaulizwa mara nyingi sana nadhani ulitolee ufafanuzi halafu watu wa Katibu hapa na wenyewe wa-*note*. Maana kila likitokea swali la elimu linaulizwa swali la *Form IV* na *VI*. Nadhani Waheshimiwa Wabunge wakati mwingine

wanakuwa hawajayapata yale majibu vizuri. Tafadhali waeleze Wabunge ili wasiendelee kuuliza hilo swali maana hii ni mara ya nne nalisikia likiulizwa hivyo hivyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwita Waitara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba maoni kama hayo tumekuwa tukiyapata Serikalini siyo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge peke yao bali hata kutoka kwa wananchi na *NGOs* mbalimbali. Hata hivyo niseme kwamba Ilani ya Uchaguzi ya CCM imeelekeza kwamba Serikali iandae utaratibu wa kutoa elimu msingi bila malipo ambayo ni kuanzia shule ya msingi mpaka *Form IV.* Kadri uwezo wa Serikali utakavyokuwa unavyoendelea kuwa mzuri zaidi inawezekana tukachukua ile *Form V* na *VI* na mambo yakiwa mazuri zaidi, Serikali ikavyojizatiti ikawa *stable* zaidi inawezekana tukatoa elimu bure mpaka chuo kikuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D.CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa siku za nyuma Serikali ilijenga Vituo vingi vya Walimu *(TRC)* na kwa kuwa sasa hivi havitumiki kwa kukosa fedha, je, Serikali ina mpango gani wa kutumia sehemu ya fedha za elimu bure kupeleka kwenye Vituo vya Walimu ili ziendeshe semina kwa walimu hao katika maeneo yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Abdallah Chikota kwa jinsi ambavyo

anasimamia maendeleo kwenye Jimbo lake la Nanyamba na Mkoa wa Mtwara kwa ujumla na hata kulisaidia Bunge zima na Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda nilichukue hili kama sehemu muhimu sana ya mchango wa mawazo mazuri na maoni Serikalini kwa ajili ya kulifanyia kazi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary Badwel, swali la nyongeza.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lengo la Serikali kutoa fedha hizi katika shule za msingi ni kusaidia uboreshaji wa elimu hiyo na sasa ni takribani zaidi ya miaka miwili fedha hizi zimekuwa zikienda katika shule zetu za msingi na sekondari. Je, sasa Serikali katika utekelezaji wa jukumu hili imepata changamoto gani za matumizi sahihi na kuondoa ubadhirifu katika fedha hizi? Kama zipo changamoto hizo wamechukua hatua gani kutatua na kupunguza changamoto hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omary Badwel, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba sasa hivi tuna uzoefu wa miaka miwili katika kugharamia elimu msingi bila malipo. Napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Waziri wangu na Serikali kuwasifu sana wasimamizi wote wa elimu kuanzia Maafisa Elimu katika ngazi ya mkoa, wilaya na halmashauri na Wakaguzi wa Ubora

na wasimamizi wa elimu katika ngazi ya kata, Maafisa Elimu wa Kata na Walimu Wakuu wa Shule za Msingi wamejitahidi sana kusimamia vizuri fedha hizi kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali. Maeneo machache sana ambayo yamekuwa na matatizo hatua zimechukuliwa na wengine wameshtakiwa kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu na wachache sana ambao wameweza kuchukuliwa hatua. Siwezi kuwataja hapa kwa sababu idadi kamili sina lakini ni wachache sana ambao wamechukuliwa hatua. Kwa ujumla kazi ambayo sasa hivi inaendelea nchi nzima ni nzuri sana na wasimamizi wote wa sekta ya elimu wanastahili pongezi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Chatanda, swali la nyongeza.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa elimu ya msingi ni kuanzia elimu ya awali kwa maana chekechea. Kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya kupeleka fedha kwa kila kichwa cha mtoto kwenye elimu ya msingi, je, haioni sasa ni wakati muafaka wa kutoa fedha hata kwenye hii elimu kwa hawa watoto wa shule za awali ili kusudi ziweze kusaidia katika uendeshaji wa madarasa haya ya awali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mary Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia kwamba elimu msingi bila malipo inaanzia madarasa ya awali ambayo ni sehemu ya shule za msingi na shule za sekondari hadi kidato cha nne. Tunapopeleka fedha kwenye kila shule mgawanyo wake umeainisha wanafunzi wote kuanzia madarasa ya awali mpaka la saba, kuanzia kidato

cha kwanza hadi kidato cha nne. Kwa hiyo, hakuna mtoto anayeachwa katika elimu msingi bila malipo kuanzia madarasa ya awali. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Chemba sasa aulize swali lake.

Na. 467

**Hitaji la Maji Shule za Sekondari za Farkwa na Msakwalo - Chemba**

**MHE. JUMA S. NKAMIA** aliuliza:-

Shule za Sekondari za Farkwa na Msakwalo zilizoko Wilayani Chemba zimepandishwa hadhi kuwa za *A – level* na idadi ya wanafunzi imeongezeka katika shule hizo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipatia maji ya uhakika shule hizo ili kuwaondolea wanafunzi adha ya kutafuta maji badala ya masomo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari Msakwalo ilikuwa ikitumia maji ya bomba kutoka katika kisima cha kijiji na Shule ya Sekondari Farkwa ilikuwa inatumia miundombinu ya kuvuna maji ya mvua na pia ilikuwa ikitumia maji ya bomba kutoka katika kisima cha kijiji. Visima hivi pamoja na uchakavu wa miundombinu havikuwa na uwezo

wa kuzalisha maji ya kutosha kwa matumizi ya vijiji pamoja na shule. Hivyo, shule hizo kushindwa kupata maji ya kutosheleza kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua tatizo la maji katika Shule za Sekondari Msalikwa na Farkwa, Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018, ilitoa jumla ya shilingi milioni 104 kwa Shule ya Sekondari Msalikwa na shilingi milioni 87 kwa Shule ya Sekondari Farkwa kwa ajili ya kuchimba visima na kufanya ukarabati wa miundombinu ya mfumo wa bomba kwenye shule hizo. Kazi ya uchimbaji wa visima na ukarabati wa miundombinu ya mabomba katika shule hizo imekamilika na wanafunzi kwa sasa wanapata maji ya kutosha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina swali moja tu la nyongeza. Kwanza nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Elimu, Profesa Ndalichako, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara kwa juhudi walizochukua za kuhakikisha kwamba shule hizi za Msakwalo na Farkwa zinapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni moja tu kwamba katika Shule za Sekondari za Mondo na Soya ambazo nazo ni shule za *A-Level* zilizopo katika Wilaya ya Chemba, wanafunzi wanatembea umbali mrefu kutafuta maji. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba wanafunzi na walimu wa shule hizi wanapata maji ya uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, kaka yangu Mheshimiwa Kakunda kwa majibu mazuri, lakini sisi Wizara

ya Maji tunatambua umuhimu wa elimu. Kupitia elimu mtoto wa mama ntilie anaweza kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi kama Wizara ya Maji katika bajeti hii tumewatengea Chemba Sh.1,468,000,000. Labda nimuagize Mhandisi wa Maji wa Chemba aone umuhimu sasa kwa shule ambazo ameziorodhesha Mheshimiwa Mbunge wa kuhakikisha wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swali la nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo Chemba inafanana vilevile na kule Mkinga. Tunaishukuru Serikali katika kipindi hiki imetuwezesha kuanzisha sekondari za kidato cha tano na sita kwa Shule ya Mkinga Leo na Maramba Sekondari. Shule hizi zinakabiliwa na tatizo kubwa sana la maji na kukamilika kwa vyumba vya madarasa na mabweni. Je, nini kauli ya Serikali kuwezesha kukamilika kwa nia njema hii ya kuwa na sekondari za *A-Level* ili ziweze kutoa elimu stahiki kama walivyokusudia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda sana nimpongeze Mheshimiwa Jumaa Aweso kwa majibu yake mazuri. Pengine hakumalizia tu kwamba Wizara ya Maji na Umwagiliaji inakamilisha mchakato wa mwisho kabisa wa kupata dola milioni 350 ambazo ndani yake kuna programu nzuri sana ya kupeleka huduma za maji katika shule za sekondari na za msingi zote nchini ambazo hazina huduma ya maji, pamoja na hizo alizotaja Mheshimiwa Kitandula, Shule za Maramba ambayo ni shule ya zamani sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie kwamba tumeshatoa agizo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri wote akiwemo Mkurugenzi wake, kuhakikisha kwamba shule ambazo wamezipangia kwamba zitaombewa kibali ziwe kidato cha tano na sita wanaweka kipaumbele cha haraka ili kusudi miundombinu yake iweze kukamilika, maombi yake yaweze kufikishwa Wizara ya Elimu ili zipate kibali ili angalau mwakani ziweze kuanza kuchukua vijana wa kidato cha tano na sita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa David Silinde, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Tatizo la maji katika shule za sekondari pamoja na shule za misingi lipo Tanzania nzima na nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri hapa wakati anajibu anasema tatizo hilo litatatuliwa katika shule zote za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nifahamu jambo hilo litatekelezwa lini kwa kuwa tumeshapitisha bajeti na hakuna fedha yoyote iliyopitishwa kwa ajili ya kupeleka maji katika shule za sekondari. Upi ni mpango ambao utasaidia kupeleka maji shule za sekondari na shule za msingi Tanzania nzima ikiwemo Momba? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa David Silinde, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kitandula, nimetoa ufafanuzi kwamba tunakamilisha mchakato wa mwisho wa kupata hizi fedha ambao ni mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia,

dola milioni 350 si hela ndogo, ni hela ndefu. Kwa hiyo, mchakato huu unaweza ukakamilika vizuri kabisa 2018/2019 na fedha hizo zikaanza kutumika 2019/2020 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba shule zetu zote zinaondolewa matatizo kabisa ya kukosa huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika bajeti ambayo tumeipitisha Bungeni hapa ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na fedha nyingine chache tulizipitisha katika kasma yetu ya TAMISEMI ambazo zote sasa tutazipeleka Wizara ya Maji ili ziweze kusimamiwa vizuri zaidi, zipo bajeti ambazo si kubwa sana kwa ajili ya kuhakikisha tumepeleka huduma za maji katika baadhi ya shule. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kuongezea kidogo majibu mazuri ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba kupitia Mradi wa *SWASH* kuna kiasi cha shilingi bilioni 16 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya maji shuleni. Kwa hiyo, mimi hiyo naona si hela kidogo, tayari Serikali imeonesha *commitment,* shilingi bilioni 16 zipo kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya maji shuleni kwa mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ramadhan Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Singida Mjini tumeanza programu ya kupandisha hadhi shule zetu za sekondari kuwa kidato cha tano na sita ikiwemo Shule ya Sekondari ya Mungumaji. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutusaidia kukamilisha programu hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea majibu yangu ya awali ambayo nimeyatoa, kwanza yeye kama mwalimu namsifu kwa juhudi zake za kuendeleza sekta ya elimu katika jimbo lake lakini vilevile kutoa mawazo mazuri kwa ajili ya nchi nzima. Napenda kusisitiza kwamba maagizo ambayo tumeyatoa kwa Wakurugenzi wa Halmashauri ambao wanasimamiwa na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ni kwamba kipaumbele lazima waendelee kukiweka katika shule zote ambazo wameziteua kwa ajili ya kuzipandisha hadhi kuwa za kidato cha tano na sita kwa maana hizo zitakuwa ni shule za nchi. Waweke kipaumbele kuhakikisha kwamba miundombinu inayohitajika yote kwa mujibu wa vigezo vilivyotolewa na Wizara ya Elimu inakamilika mapema iwezekanavyo ili kusudi shule hizo ziweze kutusaidia kupokea watoto wengi zaidi au vijana wengi zaidi wa kidato cha tano na sita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin Monko, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Katika Jimbo langu la Singida Kaskazini tunazo sekondari tatu ambazo zilipandishwa hadhi ikiwepo katika Tarafa ya Mgori Mwanamema, Ilongero pamoja na Mtinku. Shule hizi bado zina changamoto zikiwepo za vitanda, magodoro na kadhalika na zingine zimeshindwa hata kupangiwa wanafunzi katika mwaka huu kwa sababu hazijakidhi vigezo. Je, Serikali itatusaidiaje ili kukamilisha

vigezo hivyo na shule hizo zianze kutoa huduma kama ilivyokusudiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Justin Monko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, amezitaja shule tatu katika jimbo lake ambazo zimepandishwa hadhi, lakini kati ya shule tatu Shule ya Mwanamema Shein kama ilivyo jina lake ni shule ambayo imeboreshwa kwa kiasi kikubwa na sasa hivi wamepangwa vijana kupelekwa pale. Wengine walikuwa wanakuja ofisini kwangu kusema bwana hii Shule ya Mwanamema Shein sisi hatuitambui tunaomba tuhamishe watoto, nimewaambia hatuwezi kuhamisha watoto pale. Watoto waende wakasome pale Shule ya Mwanamema Shein na watapata elimu nzuri, tumepeleka walimu wazuri pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Monko pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba zile shule ambazo zina usajili wa Wizara ya Elimu lakini zinatakiwa kuongezewa miundombinu kidogo tu ili kusudi ziweze kuchukua vijana wengi zaidi kuliko *capacity* yao ya sasa hivi, wiki ijayo Wizara ya Fedha itapeleka fedha kwenye hizo shule, kama walikuwa wanakosa bwalo watajengewa bwalo, kama walikuwa wanakosa darasa moja watajengewa darasa moja ili kusudi mpaka mwezi wa nane vijana wa *second selection* waweze kuripoti shuleni.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 468

**Uharibifu wa Mazingira Nchini**

**MHE. HAWA A. GHASIA** aliuliza:-

Je, Serikali inaweza kutuambia ni nini hasa kinachosababisha uharibifu wa mazingira kwa kiwango kikubwa kati ya sheria na usimamizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 Kifungu cha 11(1), 13(1), 14, 16(1) na 30 imeainisha mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa mazingira nchini. Ofisi ya Makamu wa Rais ina jukumu la kuratibu na kuna wasimamizi mbalimbali wa utekelezaji katika ngazi tofauti. Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* linasimamia utekelezaji na uzingatiaji wa sheria kwa ujumla. Aidha, Wizara za Kisekta na Serikali za Mitaa zina jukumu la kusimamia hifadhi ya mazingira kulingana na wajibu na maeneo wanayosimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo sheria za kutosha zinazohusu usimamizi wa mazingira. Pamoja na Sheria Mama ya Mazingira Na.20 ya mwaka 2004, pia tunazo sheria zifuatazo ambazo ni muhimu katika hifadhi ya mazingira. Sheria ya Madini (2010); Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (2009); Sheria ya Afya ya Jamii (2009); Sheria ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi (2003); Sheria ya Viwanda vya Kemikali na Wanunuzi wa Kemikali (2003); Sheria ya Uvuvi

(2003); Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi (2003); Sheria ya Misitu (2002); Sheria za Ardhi Na.4 na Na.5 (1999); Sheria ya Ulinzi wa Mimea (1997); na Sheria ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu (1994). Hivyo, tunahimiza usimamizi wa sheria hizi ili kulinda mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu wa mazingira kwa kiwango kikubwa unasababishwa na kukosekana kwa usimamizi thabiti wa shughuli za hifadhi ya mazingira katika ngazi za halmashauri unaochangiwa na kutokuwa na *GFS Code* kwa ajili ya kutenga fedha za hifadhi ya mazingira katika bajeti za Serikali za Mitaa. Aidha, uelewa wa wananchi kujua wajibu wao wa kuhifadhi mazingira bado ni tatizo. Pia uharibifu wa mazingira huchangiwa na ongezeko la idadi ya watu linalopelekea kuongezekana kwa mahitaji ya rasilimali kama vile matumizi ya ardhi katika vyanzo vya maji, ukataji wa misitu na pia uelewa mdogo wa jamii kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Hifadhi ya Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kuwaagiza watendaji wa ngazi zote kuchukua hatua kadri itakavyowezekana kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa sheria hizi ili kudhibiti uharibifu wa mazingira kwa ujumla.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa nini Serikali kama inaona umuhimu wa mazingira inashindwa kutenga fedha kwa ajili ya kutengeneza *GFS Code?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Wizara inao mkakati wa kusimamia hizi sheria kwa sababu sheria ni nyingi na zinajitosheleza lakini kinachoonekana hapa ni udhaifu

katika usimamizi wa sheria. Je, mkakati upo wa kuzisimamia hizo sheria? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hawa Abdullahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na kule kwao Naumbu karibu na Mkunguni wanamuita mama ambaye hakubali kushindwa, mama ambaye tunaamini kwa namna anavyowawakilisha Mtwara huyu mama mpaka mwenyewe atakaposema kwamba sasa basi nipumzike lakini anawawakilisha vizuri wananchi wa Mtwara Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana wakati mwingine yeye kama mchezaji huwa ana-*overlap* anasaidia mpaka Jimbo la Mtwara Mjini. Juzi juzi ameuliza maswali ambayo yalikuwa yanahusu mifereji pale Mtwara Mjini, anamsaidia rafiki yetu ndugu Mheshimiwa Nachuma. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kulikuwa na tatizo la kupanga bajeti au kuanzisha *code* maalum (kasma) kwenye Halmashauri zote katika nchi yetu lakini Mheshimiwa Waziri amekwishatoa mwongozo na kuomba Halmashauri hizi waweze kuanzisha hiyo kasma na kutenga fedha. Hii ni sambamba na Wizara zote za kisekta kuanzisha kitengo maalum ambacho pia kinatakiwa kwa mujibu wa sheria kusimamia mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, kwamba tuna mikakati na pengine anadhani ni udhaifu wa usimamizi wa sheria. Nimhakikishie Mheshimiwa Hawa Ghasia, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 27 imetoa wajibu kwa kila Mtanzania kulinda na kuhifadhi rasilimali za

nchi yetu. Pia tuna Sera hii ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 1997 na yenyewe ni sera ambayo inahakikisha kwamba mazingira yetu yanalindwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ghasia tuna sheria hii hapa Sheria Mama Na.20 ya 2004 ambapo Kifungu cha 6 kimewapa wajibu wananchi waweze kulinda na kuhifadhi mazingira. Tuna Ilani ya CCM hapa Ibara ya 152 ambapo tunakwenda kupambana na uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Ndiyo maana sasa kutokana na yote haya hata juzi hapa nilielezea tulivyo na mikakati ya 2007 ya kitaifa ya kuhimili katika masuala ambayo ni ya uharibifu wa mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge ni mashahidi hapa, suala ni *mindset* ya wananchi, tuna sheria nzuri na mikakati lakini *mindset* ya wananchi ndiyo tatizo. Mungu amemuumba mwanadamu kwa mfano wake lakini bado wanadamu hawahawa wanamuangusha pamoja na kwamba Mungu alimweka kuanzisha mazingira kwenye bustani ya Eden. Kwa hiyo, nitoe wote kwa wananchi wote na Wabunge, sisi wenyewe tuhakikishe kwamba tunalinda na kuhifadhi mazingira, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye majibu ya msingi Naibu Waziri amesema kwamba tatizo ni pia uelewa mdogo wa wananchi kuhusu kutunza mazingira. Kwa kuwa sasa Mlima Kilimanjaro ile theluji inaendelea kuyeyuka na mazingira yamekuwa kame muda wote lakini wanawake na vijana wa Kilimanjaro wapo tayari kuungana na Wizara hiyo katika kuboresha mazingira hayo. Ni lini sasa hii Wizara ya Mazingira itawezesha wanawake na vijana wale kiuchumi

ili wapate miche waweze kuotesha miti kwenye mashamba yao kuzunguka mipaka na pia kwenye barabara inayoelekea Mlima Kilimanjaro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la shemeji yangu Mheshimiwa Shally Raymond, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba katika Mlima Kilimanjaro kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambapo maeneo mengi yameathirika ni pamoja na theluji ambayo imekuwa ikipamba ule mlima kule juu unakuwa ni kivutio katika masuala ya utalii. Pia tumeendelea kusisitiza kupitia Halmashauri za Hai, Rombo, Moshi Vijijini pamoja na Moshi Mjini kuhakikisha kwamba wanapanda na kuhifadhi miti. Hawa akina mama ambao amesema mimi nipo tayari kabisa kuja kwa hao akina mama japo hakuwasema ni wengi kiasi gani ili na mimi pengine niambatane na akina baba wengi kidogo kuja kuonana na hao akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Shally, baada ya Bunge hili, naye ni shahidi nilipokuwa Kilimanjaro nilimpa taarifa na kukupigia simu kwamba aje tushughulike na mazingira. Aliweza kuja na akanipa msaada ambao kwa kweli mpaka leo bado naukumbuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonesha kwamba ukataji wa miti kwa ajili ya nishati ya mkaa umekuwa ni chanzo pia kikubwa sana cha kusababisha uharibifu wa mazingira. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inaondoa *VAT* katika nishati ya gesi ili wananchi waweze kununua gesi hiyo kwa matumizi ya nyumbani kwa bei ndogo ili kuondokana na adha ya uharibifu wa mazingira inayosababishwa na ukataji wa miti ambalo ni tatizo kubwa katika nchi yetu? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa katika Ilani ya CCM, ukurasa wa 212 - 213, sehemu ndogo ya (e) tumeelekezwa na chama sisi kama Serikali kwamba lazima tuhakikishe kwamba tunaongeza kiwango cha watumiaji wa nishati mbadala kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 50 katika kipindi cha miaka mitano. Ndiyo maana katika Wiki ya Mazingira Duniani ambapo tulikuwa na siku tano pale Dar es Salaam tuliweza kuwaalika wadau mbalimbali ambao sasa wanakuja na teknolojia ya nishati mbadala. Wananchi waliweza kwenda pale wakashuhudia namna ambavyo hizi taka ngumu zikiwemo randa za mbao pamoja na vinyesi vya mifugo, wameweza kuja na teknolojia na kubana na kutengeneza mkaa. Kwa hiyo, tunaamini kwamba tutapunguza ukataji wa miti kwa sababu ya teknolojia mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye upande wa gesi kulikuwa na *ORYX* wanaonyesha kutumia gesi tutatumia fedha kidogo sana ambapo huwezi kulinganisha na mkaa. Ndiyo maana Mheshimiwa Waziri wa Nishati tayari wameshahakikisha kwamba usambazaji wa gesi katika Jiji la Dar es Salaam kwa kupitia mabomba sasa umeanza. Ni

lengo la Serikali kwamba tutaenda na miji mingine na miji ndiyo inayotumia mkaa zaidi kuliko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Msongozi, naamini wewe kama mdau wa mazingira jambo hili ambalo lipo kwenye ilani tutakwenda kufanya mageuzi makubwa ya kuhakikisha kwamba tunatumia nishati mbadala badala ya kuendelea kukata miti. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf, swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nimuulize mtani wangu kama anavyotaka. Mwishoni mwa miaka ya 80 kulikuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira ambao ulipelekea mmomonyoko mkubwa wa ardhi katika Mikoa ya Dodoma na Shinyanga na kukawa na miradi ya uhifadhi wa mazingira ambayo ilikuwa inaitwa *HADO* kwa Dodoma na *HASHI* kwa Shinyanga. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kufufua miradi ile ambayo ilipelekea Mikoa husika kuwa na hali nzuri kama ilivyo Dodoma sasa? Serikali ina mpango gani wa kuhuisha miradi kama ile katika mikoa mingine ambayo imeathirika zaidi kwa uharibifu wa mazingira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la mtani wangu wa kisiasa Mheshimiwa Yussuf, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 19 wakati tunajibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji tulieleza mikakati mbalimbali ambayo tunayo katika kuhakikisha kwamba tunapambana na uharibifu wa mazingira katika masuala ya vyanzo vya maji lakini pia kwenye ardhi kama ambavyo Mheshimiwa Yussuf amezungumzia. Tulisema mkakati ule tumehusisha wasomi na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na utakuwa tayari hivi karibuni, unaonesha namna gani

ambavyo katika nchi yetu maeneo yalivyoathirika, si tu kwa Dodoma huku ambako tunasema kuna ukame lakini pia maeneo yale ya wafugaji ambapo ardhi imeharibika kwa kiasi kikubwa. Mkakati ule tunauita ni Mpango Maalum Endelevu wa Matumizi Bora ya Ardhi pale ndipo ambapo tutakwenda kutekeleza mambo hayo kwa sababu mikoa yote ambayo ina shida kubwa zaidi ya mmomonyoko wa udongo imeanza kubainishwa katika mkakati ule. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kuna tangazo muhimu hapa.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika anatarajiwa kuzindua zoezi la kupima virusi vya UKIMWI kwa hiari hapa Bungeni kwa Waheshimiwa Wabunge lakini pia na wafanyakazi wa Bunge. Atazindua zoezi hilo saa nne kamili leo hii kwenye viwanja vilivyopo nyuma ya Ukumbi wa Mheshimiwa Pius Msekwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hasa wale wa Kamati ya UKIMWI mnaombwa kuhudhuria zoezi hilo la uzinduzi halafu Waheshimiwa Wabunge wale ambao hawajapima wanaombwa kuanzia saa saba waende huko kupima kwa hiari ili Waheshimiwa Wabunge wote tuwe tunafahamu afya zetu vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea, Mheshimiwa Ignas Malocha, swali la nyongeza.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Rukwa linatoa ajira kwa wananchi wengi kutoka katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Vilevile ni ziwa ambalo imegundulika gesi aina helium lakini ziwa hilo hilo linatabiriwa kukauka kwa miaka ijayo. Nini mkakati wa Serikali katika kunusuru ziwa hilo lisikauke? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Malocha, Mbunge wa Kwela, shemeji huyu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi sana, tayari Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Waziri wa Nchi (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa January Makamba alishatoa maelekezo kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba wanawasilisha ofisini kwetu vyanzo vyote vya maji pamoja na changamoto zake. Ziwa Rukwa ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vya maji ambavyo hata bila kutuletea jina hilo tayari kitaifa tunafahamu kwamba Ziwa Rukwa ni chanzo cha maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Malocha na Mheshimiwa Mulugo, baada ya mkutano huu mimi pamoja na wataalam tutakuja kwenye Ziwa Rukwa ili kujionea sisi wenyewe namna gani mazingira yalivyoharibiwa ili tuweze kuchukua hatua stahiki na za haraka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Malocha pale kwa shemeji yangu Movu pale wapelekee salamu waanze kufanya maandalizi ili wanipokee twende nao Ziwa Rukwa tuweze kufanya kazi hii ya Serikali. ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutamalizia swali la mwisho, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba Mbunge wa Busanda sasa aulize swali lake.

Na. 469

**Ujenzi wa Barabara ya Geita – Bukoli – Kahama**

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Geita – Bukoli – Kahama kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Geita – Bukoli – Kahama yenye urefu wa kilometa 120 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS).* Mpango wa kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami umeanza ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika tangu mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia *TANROADS* imepanga kutekeleza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza *(Lot.1)* ni Geita – Nyarugusu – Bulyanhulu *Junction* (km 58.3) na sehemu ya pili *(Lot.2)* ni Bulyanhulu Junction – Kahama (Km 61.7). Utekelezaji wa ujenzi utaanza mara fedha zitakapopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha, *TANROADS* itaendelea kuimarisha barabara hii kwa kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, swali la nyongeza.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu, japokuwa niseme tu kwamba barabara hii imekuwa kwenye mpango kwa muda mrefu sana. Kulingana na majibu yake ni kwamba upembuzi

yakinifu umekamilika tangu 2014/2015, ni muda mrefu sasa inakaribia miaka minne. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Geita na Mkoa wa Shinyanga na ni muhimu kiuchumi. Mimi na wananchi tungependa kujua ni lini fedha itapatikana ili utekelezaji uanze mara moja? Hilo ni swali langu la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015, Mheshimiwa Rais akiwa pale Katoro aliweza kuahidi kilomita 10 za lami; kilometa 5 Katoro na kilometa 5 Buseresere lakini mpaka sasa hakuna chochote kinachoendelea. Je, ni lini sasa utekelekezaji huu utaweza kuanza? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba uniruhusu nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Lolesia Bukwimba kwa sababu amekuwa akifuatilia sana juu ya maendeleo katika Jimbo lake. Niseme tu kwamba barabara hii tumezungumza naye sana nje ya Bunge lakini naona pia anavyoshirikiana na pia na Wabunge wengine kwa sababu barabara hii inagusa maeneo mengi na kama alivyosema inaunganisha Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa kuitengeneza barabara hii na niseme kweli imekuwa ni muda mrefu tangu usanifu ukamilike na kwa kuwa Serikali inaendelea kutafuta fedha, nimjulishe tu Mheshimiwa Lolesia Bukwimba juhudi zake zimesababisha angalau kwa kuanza katika mwaka wa fedha 2018/2019, Bunge lako limetenga shilingi bilioni 13 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii. Wakati tunatafuta fedha za kutosha lakini juhudi zimeshaanza

kwa kuweza kupata hizi fedha ambazo Bunge limepitisha ili kuanza kuitengeneza hii barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Lolesia Bukwimba pamoja na wananchi wa Jimbo la Kahama Mjini, Jimbo la jirani yangu pale Mheshimiwa Maige kule Msalala pamoja na Jimbo lake la Busanda pamoja na Geita na wananchi wote wa Nyarugusu, Bukoli, Bulyankulu, Itobo, Busoka na Kahama Mjini kwamba ujenzi sasa unaanza na tunaendelea kusukuma ili tuweze kupata fedha za kutosha kujenga barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Rais katika Mji wa Katoro na Buseresere, Serikali inatambua kilometa kumi ziko kwenye ahadi, kilomita 5 ziko Katoro na kilomita nyingine 5 ziko Buseresere. Niseme tu kwamba tumefanya uratibu ili kuweza kuzitambua barabara zote ambazo zimeahidiwa na Mheshimiwa Rais nchi nzima. Tumeendelea kuzipanga zile zinashughulikiwa na *TARURA* na *TANROADS* na tunaendelea kuhakikisha kwamba kwenye ule mpango mkakati wa Wizara basi barabara zote ambazo Waheshimiwa viongozi wametoa ahadi zinatekelezwa. Kwa hiyo, nimtoe hofu, tunazisimamia kwa nguvu kuhakikisha kwamba ahadi hizi za Mheshimiwa Rais na zilizopita katika awamu nyingine tunaendelea kuzishughulikia ili tuweze kutengeneza barabara hizi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hebu angalia Wabunge waliosimama maana si wote watapata nafasi ya kuuliza maswali. Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kabla ya kuuliza swali, naomba kuipongeza Wizara ya Kilimo, Bodi ya Wakurugenzi wa Pamba kwa kuwapa nafuu wakulima wa pamba kwa kuwapa utaratibu mzuri wa ununuzi wa pamba na kuwaondolea kero ambayo ilikuwa inawapa usumbufu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, barabara ya Mgeta – Mihingo – Nikomalile na Sirolisimba imekuwa na ahadi ya muda mrefu na imeharibika sana na ina umuhimu mkubwa wa kuleta wateja katika Mnada mkubwa wa Mgeta ambao unafanyika mara mbili. Je, ni lini barabara hii itakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi, umeulizwa ni lini.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Getere kwa sababu mimi kila nikikutana naye namuita mzee wa Silolisimba kwa sababu yah ii barabara ya Mgeta – Silolisimba, anaifuatilia kweli. Kwa kweli kama nilivyokuwa nimemuahidi ilikuwa ni kuhakikisha kwamba barabara hii tunaipa kipaumbele kwa sababu ina matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Bunda kwa ujumla kwamba baada ya mvua kuwa zimepungua mkandarasi yuko *site* na nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge mazungumzo ambayo tumeyafanya na kuhakikisha kwamba barabara inatengenezwa majibu yake yanapatikana kwa sababu fedha za kupeleka kwa ajili ya barabara hii zimeshapatikana, kati ya wiki hii na wiki ijayo fedha zitakwenda. Nimuombe na kumuagiza tu mkandarasi aliyeko *site* afanye kazi kwa nguvu na mimi baada ya Bunge hili ntafika kuona kwamba kazi inaendelea ili kuweza kuondoa hii shida ambayo ipo katika eneo hilo. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Getere, tuendelee kushirikiana na kubadilishana mawazo lakini nia yetu ni moja ni kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu hii ya barabara. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Mheshimiwa Naibu Waziri pia atueleze, kwa sababu wakati alipokuja Mtwara alipita pia kukagua barabara ya Umoja, hii inayoanzia Mtwara – Newala mpaka Masasi lakini pia inayokwenda mpaka Nachingwea. Wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba barabara ile itajengwa kwa mara moja na wataweka pale wakandarasi wanne ili kuweza kufanya barabara hiyo ijengwe kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kufahamu, ni lini hasa barabara inayotokea Masasi - Nachingwea - Lukuledi - Chikunja - Ndomoni - Nachingwea, itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kama ambavyo iliahidiwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nimetembelea Mtwara na Lindi na nimeona harakati za ujenzi. Kwanza kwa ufupi tu ni kwamba maeneo yote yaliyokuwa na shida kubwa ujenzi unaendelea. Ukiangalia kwenye bajeti hii pia tuliyopitisha tumeweka fedha za kutosha kukamilisha daraja katika Mto Lukuledi kwa sababu eneo hili lilikuwa ni hatari, wananchi walikuwa wanapita kwenye maji na walikuwa na hatari ya kuliwa na mamba. Kwa hiyo, tumeweka fedha za ujenzi pale na tunaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kifupi kwa barabara hii ambayo ameitaja ili kuwa na *Lot* 4 kama alivyosema kuharakisha ujenzi ule, utaratibu unaendelea vizuri kwa sababu tunatafuta fedha. Wakati tunafanya juhudi za kupata fedha za kutosha ziko fedha ambazo zimetengwa wakati wowote tutaweza kutangaza ili kuweza kuanza ujenzi huu. Kwa hiyo, nimpongeze sana, tuendelee kuwasiliana, nami nitapita pia wakati mwingine nione harakati hizi zikiendelea. Nimeona barabara hii ni muhimu sana inawaacha watu wengi walioko kule Liwale kwani tukikamilisha eneo hili tunaweza kwenda tena kilometa 129 kutoka Nachingwea kwenda Liwale ambayo sasa tumeiweka kwenye hatua ya usanifu ili wananchi wa maeneo yale waweze kunufaika na barabara hii itakapokuwa imejengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kama lilivyo swali la msingi, barabara inayotoka Mgakorongo – Kigalama – Bugomola - Mlongo ni barabara muhimu na inaunganisha nchi jirani pamoja na Wilaya jirani ya Karagwe. Barabara hii ni ahadi ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne, lakini na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi itajengwa kwa kiwango cha lami. Ni lini barabara hii itajengwa na wananchi wakalipwa fidia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Innocent Bilakwate, maarufu kama Mchungaji, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya Mgakorongo – Kigalama – Mlongo ni barabara ambayo inaunganisha nchi yetu na Uganda na inahudumiwa na

Wakala wetu wa Barabara *TANROADS.* Katika sera ni kati ya barabara ambazo zina kipaumbele katika kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo tumeongelea hizi barabara, sijafika Kagera kwa ziara lakini nazitambua kwa sababu tumekuwa tukibadilishana mawazo. Niwapongeze sana wananchi wa Kyerwa kwa kweli hawakukosea kumchagua Mheshimiwa Bilakwate kwa sababu kazi nzuri anaifanya. Jukumu ambalo wamempa analifanya kisawasawa na sisi kama Serikali tunaendelea kushirikiana naye kuhakikisha kwamba hatuwaangushi wananchi wa Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu barabara hii urefu wake ni takribani kilometa 79 hivi, ambapo itakwenda kuungana na barabara kubwa ambayo inakwenda kuunganisha nchi yetu pia na upande ule wa Mtukula. Kwa hiyo, tunatambua umuhimu wa barabara hii, inapita maeneo yenye uzalishaji mkubwa na itakuwa na mchango mkubwa sana kwenye uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ipo kwenye mpango kwa kweli, labda Mheshimiwa Bilakwate baada ya hapa tukae tuzungumze ili tuangalie kwa upana kwenye *strategic plan* tumepanga namna gani hatua kwa hatua kuikamilisha barabara hii. Pia tumetenga fedha kuhakikisha kwamba barabara hii inaimarishwa ili dhana nzima ya kuhakikisha tunatekeleza sera yetu ya kuunganisha mikoa yetu na nchi za jirani inakamilika na wananchi wanapata huduma na kwa kweli inachangia pia katika uchumi wa nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, swali la nyongeza.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anafahamu barabara ya Muheza – Amani, kilometa 36 ambayo aliipita, imepangiwa fedha mwaka uliopita shilingi bilioni 3 kujengwa kwa kiwango cha lami na bajeti hii pia imepangiwa shilingi bilioni 5 ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ni lini barabara hii itaanza kutengenezwa kwa sababu inazidi kuharibika? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nilitembelea Muheza na nilipita barabara hii Mheshimiwa Mbunge anayoizungumzia na nilizungumza na wananchi kule Amani, hata kiu ya wananchi wa maeneo yale kuunganishwa na majirani zao wa Maramba na Korogwe ni kubwa. Kuna kitu ambacho kinaendelea kuhakikisha kwamba fedha hizi sasa zinakwenda ili barabara itengenezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli maeneo haya ni hatari kwa sababu hata barabara zake tutengeneza kwa kutumia zege la saruji kwa sababu ina miteremko mikali sana. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Balozi Adadi, kama tulivyokubaliana nitaendelea kuhakikisha wakati wowote fedha hizi zitolewe hii barabara itengenezwe kwa wakati kwa sababu sehemu ambazo zina maporomoko makubwa ni hatari sana na wakati mwingine inakuwa kikwazo wananchi kupita kabisa katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali inatambua hivyo, sisi kama Wizara tutahakikisha kwamba fedha ambazo zilikuwa zimetengwa mwaka wa fedha unaoisha na mwaka unaokuja zinakwenda kutibu na kuhakikisha barabara hii inatengenezwa. Kwa hiyo, nitampa

mrejesho kuona hatua gani kama Wizara tunachukua kwa kadiri tunavyopata fedha kutoka Hazina tuweze kuipelekea barabara hii ili iweze kutengenezwa na ipitike kwa urahisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Mtolea, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la barabara ya Bukoli – Kahama linafanana kabisa na barabara ya Davis Corner – Jeti Lumo ambayo ipo kwenye ule mpango wa barabara pete za Dar es Salaam kwa ajili ya kupunguza foleni. Mkandarasi *Nyanza Construction* alipewa pesa ya kujenga kipande kidogo tu cha kutoka Tandika - Yombo Dovya – Makangarawe – Buza - Mwisho wa Lami, kipande kilichobaki cha kutoka Mwisho wa Lami - Jeti Lumo bado hakijafanyiwa kazi na kina mashimo makubwa. Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha ili mkandarasi amalize kujenga barabara hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna mradi huu wa *Davis Corner* - Jeti Lumo na natambua pia kuna kiasi ambacho kimeshatengenezwa. Matumaini yangu baada ya kukamilisha kipande hiki sasa ile safari ndefu ya kuitengeneza barabara hii imeshaanza. Tulikuwa na shida kidogo ya kuendelea kulipa wakandarasi lakini mpaka hivi navyozungumza karibu wakandarasi wote nchi nzima wamelipwa. Kwa hiyo, kwetu sisi ni fursa ya kuendelea kufanya

matengenezo ya barabara. kwa hiyo, nafikiri hata baada ya kikao tuzungumze ili tuone kwamba hiki kipande kinachobakia tuweze kuona kwamba kinaweza kukamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba hizi barabara za Dar es Salaam na mzunguko wake zinaweza kutengenezwa. Pia kuna fedha ambazo zimeendelea kutolewa ili kuhakikisha kwamba kazi hazisimami na hasa baada ya mvua hizi kupungua tunarejeshea maeneo ambayo yalikuwa yameharibika ili waanchi wasipate adha. Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi wa Dar es Salaam na maeneo yote kwamba tumejipanga vizuri kuhakikisha shughuli za ujenzi zinaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda, mnanipa wakati mgumu sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Margaret Sita, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa sana ya kutujengea barabara ya kutoka Ndono - Urambo na sasa hivi inaendelea kutoka Urambo - Kaliua. Je, Serikali haioni kwamba kazi nzuri inaharibiwa na kipande ambacho mpaka sasa hivi hakijajengwa kutoka Posta - *Seed Farm?*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu pili, je, Serikali...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa mama Sitta, unauliza swali moja tu la nyongeza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza

la mama yangu, Mheshimiwa Margaret Sitta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Mheshimiwa Mbunge anatambua kwamba hii barabara kutoka Urambo - Kaliua kipande kilichobakia kilometa 48 mkandarasi yuko *site.* Tutakuwa tumefanikiwa kuunganisha sasa kutoka Tabora Mjini mpaka Urambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua pia kiu ya Mheshimiwa mama hapa hiki kipande cha barabara kutoka Posta – *Seed Farm* kiunganishwe lakini kwetu tuliona kwamba muunganiko wa barabara kubwa ulikuwa na kipaumbele lakini baada ya hapo tutaendelea mama yangu kukiangalia hiki kipande. Najua pia ana kiu ya kupata *round about* ambayo tutaiita *Mama Round About.* Kwa hiyo, tunaendelea kuiangalia uwezekano wa kupata *round about* ili tuweze kuunganisha vizuri na kuhakikisha kwamba ajali katika makutano ya hii barabara tunaziondoa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Nagu amesimama sana, simuoni tena sehemu yake sijui yuko sehemu gani. Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, swali la nyongeza.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote kwanza napenda sana nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ynanaleta matumaini kwetu na kwa wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka 2015 kulitolewa ahadi na Mheshimiwa Makamu wa Rais ya kujenga barabara inayoanzia Wilaya ya Namtumbo - Lusewa – Mchoteka - Nalasi kwa kiwango cha lami. Ni nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha tunatekeleza ahadi hii kabla ya mwaka 2020 wakati wa uchaguzi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitembelea maeneo haya nikitokea Nakapanya kuja Tunduru. Natambua pia ile kiu ya wananchi wa Tunduru ili kuweza kupita kwenye barabara hii kutoka Namtumbo - Lusewa - Nalasi lakini nia yao twende kuunganisha na wananchi wa Msumbiji. Najua katika Mto Ruvuma maeneo haya ya kutoka Nalasi tunahitaji kuwe na kivuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie tu kwa ujumla wake kwamba barabara hii iko kwenye mpango na hata kwenye bajeti kuna kiasi cha fedha kimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii. Vilevile nimhakikishie pia tutakapokamilisha Daraja la Ruhuhu kile kivuko ambacho muda mwingi tumezungumza tutakipeleka eneo hili ili wananchi wa Nalasi na majirani zao waweze kuvuka kwenda Msumbiji. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona, nilikuwa nimetoka kidogo nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara kule Manyara inafanana na barabara iliyoulizwa na muuliza swali la msingi, inaitwa Mogitu – Basotu - Hyadom na Hyadom ni hospitali kubwa ya rufaa kule ambayo inahudumia watu wengi wa Mkoa wa Manyara. Barabara hiyo ni ahadi ya Rais akiomba kura; je, *process* au mchakato wa kujenga barabara hiyo utaanza lini ili watu wanufaike na ile Hospitali ya Hyadom ambayo kwa kweli imekuwepo kwa miaka mingi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la shemeji yangu, Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ambayo anaizungumzia Mheshimiwa Mbunge ni barabara ambayo kwa kweli imekuwa ikisemewa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Mbulu wana ushirikiano mkubwa maana wanaizungumzia sana barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba wakati wowote wadau wote ikiwemo Waheshimiwa Wabunge tutakuwa na kikao cha kuzungumzia barabara hii ambapo sasa itakuwa inatoka Mbulu Mjini - Katesh - Hyadom - Sibiti tunaungana pia na mikoa ile ya upande wa Kanda ya Ziwa. Barabara hii usanifu wake na michoro imeshakamilika, hatua iliyopo sasa ni kuzungumza na wadau ili tuendelee na hatua nyingine kwa sababu zipo *indication* za kupata fedha kutoka Serikali ya Ujerumani kama sikosei kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Kwa hiyo, natambua umuhimu wa muunganiko wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Bunge linaendelea kama wiki mbili zilizopita nimetembelea kipande ambacho kinakwenda kuunganisha barabara hii kikitokea Singida. Kutokana na umuhimu wa eneo hili la Hyadom kwa sababu ile hospitali ni kubwa na huduma nyingi sana kwa wananchi wengi kutakuwa na kipande cha kilometa 93 kutoka Singida kwenda Hyadom. Wakati naikagua ile barabara kwa sababu ilikuwa haipitiki, nimeenda mpaka Hyadom lakini nimeona pia *logistics* za barabara hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge anaizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na wananchi wote wa maeneo yake kwamba hii barabara sasa ujenzi wake uko karibu. Imechukua muda mrefu lakini wasiwe na wasiwasi, upo mpango mzuri wa kujenga barabara hii inayounganisha Mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Simiyu, Shinyanga pamoja na Mwanza. Hii ni barabara muhimu sana kwa sababu eneo hilo linazalisha sana mazao mengi na huduma ya afya kama nilivyosema ni muhimu sana kwa wananchi wa maeneo haya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana nami Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu maswali mengi sana hapa na hatujamwekea maji ya kunywa hapo pembeni. Tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, nitaleta kwenu matangazo, halafu tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Tangazo la kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Spika, ambao wako Jukwaa la Spika ambao ni Ndugu Isumaili A. Suleimani ambaye ni Katibu Mkuu wa Baraza la Taifa la *NGOs* yaani NAKONKO; Ndugu pia Daun Well ambaye ni *Country Director of* VSO; na Ndugu Inocent Augustino ambaye ni *Deputy Country Director*. Karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kundi la kwanza ni wageni 15 wa Mheshimiwa Injinia Atashasta Nditiye ambaye ni Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha St. John, wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na mwanafunzi mmoja kutoka Chuo cha Mipango. *(Makofi)*

Wageni 66 wa Mheshimiwa Antony Mavunde ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira ambao ni wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari ya Maria De Mathias iliyopo Jijini Dodoma wakiongozwa na walimu wao. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Doto Biteko ambaye ni Naibu Waziri wa Madini ambao ni rafiki zake kutoka kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab ambao wapiga kura wake kutoka Wilaya ya Muheza Mkoani Tanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 24 wa Mheshimiwa Dustan Kitandula ambao ni wananfunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Wilaya ya Mkinga, Mkoani Tanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunay pia mgeni wa Mheshimiwa Willy Qambalo ambaye ni mpiga kura wake kutoka Wilaya ya Karatu, Mkoani Arusha. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambao ni ndugu zake, rafiki zake na wana CCM kutoka Mkoani Mwanza. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 38 wa Mheshimiwa Innocent Bilakwate ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya Kyerwa na Makatibu Kata wa CCM na marafiki zake. Karibuni sana viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Kyerwa. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Shally Raymond ambao ni mama yake Dkt. Edi Wilson na mtoto wake **Jelly** kutoka Mkoani Morogoro. Karibu sana mama na mtoto. *(Makofi)*

Tunao pia wageni kumi wa Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ambao ni Madiwani na viongozi wa CCM kutoka Wilaya ya Namtumbo Mkoani Ruvuma. Karibuni sana viongozi wetu kutoka Namtumbo, naamini tulionana wakati wa kuchangisha fedha za hospitali, karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa James Ole Millya ambao ni marafiki zake kutoka nchini Marekani. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa James Ole Millya. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaye ni Mwandishi wa Habari kutoka Radio Furaha Mkoani Iringa Ndugu Lauson Mgani. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni nane wa Mheshimiwa Elias John Kwandikwa ambao ni wahitimu wa kidato cha sita mwaka 2018 wa Shule ya Sekondari Dakama iliyopo Ushetu, Mkoani Shinyanga, karibuni sana. Mheshimiwa Kwandikwa naamini hawa wahitimu ndiyo waliofaulu zaidi uko kwenye Jimbo lako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni la kuwakumbusha nilishalitangaza hapa kuhusu upimaji wa hiari wa virusi vya UKIMWI kwa Wabunge na watumishi wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge mnakumbushwa huduma hii itaendelea kutolewa nyuma ya Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mjitokeze kwenda kupima kwa sababu viongozi wengine humu ndani wameshapima wakiongozwa na Mheshimiwa Keissy na majibu yake pia ameshachukua Mheshimiwa Keissy. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mkipima afya pia mchukue majibu yenu.

**MBUNGE FULANI:** Wewe je?

**NAIBU SPIKA:** Nami pia nimeshapima, maana kuna mtu ananiuliza na nilipelekwa na Mheshimiwa Dkt. Suleiman, kwa hiyo, nilipelekwa na Daktari jamani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU-KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Na**

**Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa majina hapa kama ulivyo utaratibu wetu na vyama vyote. Tutaanza na Mheshimiwa Cosato Chumi atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah na Mheshimiwa Ali Salim Khamis ajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Naomba moja kwa moja nianze kwanza kwa kushukuru Mamlaka ya *TRA* hususani Kamishna Mkuu na Kamishna wa Kodi za Ndani, lakini pia na Waziri kwa sababu wakati fulani niliwasilisha kwao malalamiko, licha ya kuwa niliwasilisha kwa meseji juu ya wananchi wangu wanaofanya biashara ya mbao na matatizo wanayokutana nayo. Kwa kweli hatua zilichukuliwa, Kamishana wa Kodi za Ndani akaja Mafinga akafanya mkutano karibu saa sita kuwasikiliza wale wadau. Kwa sababu ilifika wakati ilikuwa kama vile kufanya biashara ya mbao ni laana. Ukipakia mzigo mtu mwenye lori anaulizwa mashine ya *EFD* aliyokulipa mwenye mzigo ya *transport* iko wapi, hana, faini milioni nne. Kwa hiyo, tulikuwa tuna *paralyse* sekta ya mazao ya misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa hili napenda kupongeza lakini pia napenda kushauri. Kumekuwa na malalamiko sana ya wafanyabiashara hususani

wafanyabiashara wadogo wa Mji wa Mafinga. Ushauri wangu kwa Serikali na kwa *TRA*, naomba kupitia Idara ya Elimu kwa Mlipa Kodi kwa mwaka walau mara mbili iwe inatoa elimu lakini pia ikutane na wafanyabiashara na kujua ni changamoto gani wanakutana nazo ili kwa pamoja waweze kuwa *on the same boat.* Kwa sababu tunachotaka watu walipe kodi *sustainably* siyo mwaka huu mtu alipe kodi Sh.1,000,000, mwaka unaofuatia Sh.800,000, mwaka unaofuata Sh.500,000, mwaka unaofuatia ame-*collapse.* Lazima tuwekeane mazingira Serikali ipate chake lakini pia na wafanyabiashara wa-*survive progressively*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, mimi nilishika shilingi hapa wakati wa bajeti ya Wizara kuhusiana na fedha za miradi viporo. Mheshimiwa Jitu jana amezungumza, kwamba fedha hizi Serikali imekubali itatoa kwa awamu nne, itaanza na shilingi bilioni 32 kwa 29 kwa miradi ya elimu na afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mimi kwa Serikali fedha hizi Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana zikawa ni *reflected* kwenye hiki kitabu cha matumizi. Naiamini Serikali yangu lakini wasiwasi wangu Waheshimiwa kama tutapewa hizi fedha awamu hii ya mwezi wa sita na ambazo Mheshimiwa Waziri nikuombe, tumebakisha siku tisa kumaliza mwaka wa fedha, ni matarajio yangu kwamba ya kufanya majumuisho fedha hizi zitakuwa zimeshaenda kwenye halmashauri ili michakato ya manunuzi kupitia *force account* iweze kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema zile *reflected* humu Waheshimiwa Wabunge, tukianza mwaka 2018/2019 kama hazipo humu, pamoja na kuwa naiamini Serikali yangu tunaweza tukapigwa changa la macho. Kwa sababu baadaye tutaambiwa haipo katika vitabu. Nawaomba sana muangalie suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, Serikali hapa imesema kuhusu asilimia kumi ya wanawake na vijana na kwa mujibu wa Kamati imependekeza kuwa iwe 4, 4, 2 kwa

maana wanawake, vijana na walemavu. Hata hivyo, lazima tukubaliane, halmashauri hazifafani uwezo. Mimi napendekeza hii asilimia kumi ilenge maeneo ambayo ni majiji au manispaa. Kuna halmashauri baada ya Serikali ku-*centralize* vyanzo vingi hii *ten per cent* inakuwa kama maigizo *unless otherwise* tunafanya *politics.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tuko *serious* kabisa tumehamasisha wananchi wajiunge katika vikundi Serikali itusaidie katika baadhi ya maeneo ambako vyanzo viko chini iweze kupeleka asilimia kumi ya vikundi kama ruzuku. *Otherwise* kama halmashauri kwa vyanzo vya ndani inakusanya shilingi milioni 500 asilimia kumi unazungumzia shilingi milioni 50, hivi ukiwapa vikundi Sh.100,000 na vikundi viko vingi tumewasaidia au tumefanya *politics?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, usahuri mimi kwa Serikali kwenye *ten percent* hii katika baadhi ya maeneo tusifanye *unform.* Majiji kama Arusha, Dar es Salam, Mwanza na Manispaa unaweza ukasema waende kwa utaratibu huo, lakini kuna maeneo kwa kweli vyanzo ni dhoofu. Kwa hiyo, Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka ruzuku ili hamasa tuliyowapa wananchi kwamba wajiunge katika vikundi iwe ni kweli kwa vitendo isiwe tu katika makaratasi *ten percent. Ten percent* yenyewe imekuwa ngumu kwa sababu hata *OC* haiendi ipasavyo; halmashauri zinajikuta kwamba zinachukua fedha matokeo yake inakua *ten percent* katika makaratasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia *challenge* mbalimbali ambazo Serikali imesema inakabiliana nazo katika masuala ya kuongeza makusanyo. Mheshimiwa Waziri tuna fedha tunapoteza kwenye suala la *fuel levy* kwa sababu hatujui mpaka leo mafuta kiasi gani yanaingia katika Taifa hili. Ameenda Mheshimiwa Rais pale bandarini, ameenda Waziri Mkuu tena Waziri Mkuu nadhani ameenda hata tatu kuhusiana na suala la *flow meter* lakini mpaka leo hatufahamu suala la *flow meter* limefikia wapi. *Flow meter* yenyewe iliyopo watu wana *tamper* nayo wakati mwingine

wanacheza nayo isipige alamu lakini hata ule mchakato wa kupata *flow meter* nyingine hatujui umeishia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama Waziri anataka pesa, kuna pesa zingine ziko nje nje lakini tutaweza kuzipata kama tutadhibiti baadhi ya mianya moja wapo likiwa ni suala zima la kudhibiti tuweze kujua idadi ya mafuta yanayoingia katika taifa letu. *Otherwise* tutawakamua Wamachinga, tutawapa sijui hiyo *TIN* namba *that's is very peanut*, kuna pesa mamilioni kwa mabilioni katika suala zima la mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la *ETS*, yaani *I am very layman* linapokuja suala la mambo ya uchumi lakini na u-*layman* wangu nashindwa kuelewa hivi sisi kweli Mheshimiwa Mpango katika zama hizi za *digital* tunashindwa kuwa na *control mechanism* ya sisi kama sisi ili kuokoa yale mabilioni badala ya kwenda kwenye kampuni tu bora kampuni yakabaki hapa yakatusaidia na tumesomesha vijana. Nadhani Mheshimiwa Waziri hili jambo kama Serikali mnatakiwa mlitafakari mara mbili. Hatuwezi tukawa tunahangaika kwamba hatuna vyanzo lakini kuna pesa tunazipoteza tu. Naamini katika mifumo ya kisasa Serikali ina uwezo kabisa wa kujua na ku-*cotrol* uzalishaji uwe wa maji, soda au wa vinywaji vyovyote hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la Mheshimiwa Waziri kurejeshewa mamlaka ya kusamehe, kuna watu wengine hapa tunapata miradi ambayo ni misaada kutoka kwa wafadhili marafiki, kutoka kwa *NGO's* na Balozi mbalimbali, niombe sehemu ile ya msamaha Mheshimiwa Waziri hebu iwe *extended* iende mpaka kwenye miradi ya namna hii ambayo tunaipata katika kuangaika kwa ajili ya wananchi wetu. Mimi nina mradi pale Ubalozi wa Japan unatujengea *theater* ya kisasa, Halmashauri imelazimika kulipa zaidi ya shilingi milioni 30 kama sehemu ya *VAT*. Niombe pamoja na mipango hii ambayo umeileta hebu huo msamaha tukupe nguvu uweze kusamehe hata misamaha ambayo sisi tumehangaika kwa marafiki zetu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ukurasa 59 wa hotuba na Waheshimiwa Wabunge naomba mnisikilize sana, amekuja hapa na hizi *HS Codes* kwa ajili ya makaratasi ya kuzalishia madaftari na vitabu. Mheshimiwa Waziri hizi *HS Codes, unless* ama mmejua au hamjajua, Waheshimiwa Wabunge niwafahamishe kilichosamehewa kwenye daftari kwa mujibu wa hizi *HS Codes* ni *cover,* hili hapa, kama ni kitabu ni *cover.* Hizi *HS Codes* Mheshimiwa Waziri ni za makaratasi magumu. Kama kweli tunataka tusamehe kwa ajili ya uzalishaji wa madaftari, muende mkazi-*review* hizi *HS Codes.* Niwaombe Waheshimiwa Wabunge tujitahidi kujifahamisha na kuhabarishana. Kwa sababu ukienda tu ukiona hizi *HS Codes* hapa tumepiga makofi; lakini sisi kama Wabunge wa Bunge Tukufu tupigie makofi hii *cover?* Katika daftari *cover* na hiki cha ndani kipi kingi? Kina Mwalimu Mulugo wanajua mambo ya madaftari. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri muende mka-*review* kitu hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za *LGDG,* mimi naendelea kuomba mmesema kuna miradi mikakati; siyo kila halmashauri inaweza kuwa na mradi mkakati, hapa ndiyo sisi pakutokea kama Wabunge na kama halmashauri. Kwa hiyo, mimi naomba tusijifiche kwenye kichaka cha miradi mikakati, fedha hizi zinazokwenda kwenye maendeleo na ku-*stimulate* wananchi kuchangia na kuhamasisha na kufyatua matofali kwa kutumia nguvu zao Serikali iendelee kuzitenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, *sports betting,* hatuwezi kukwepa duniani sasa hivi hicho ni chanzo kikubwa sana cha mapato. Sheria imetoka asilimia 6 mpaka 10 ya mauzo ghafi, napendekeza na kushauri ili kuleta *fairness* kwa mchezaji na mchezeshaji na ili kuvutia wachezaji wengi wasikwepe waendee kwenye *online sports betting*, Serikali iweze kuangalia kusudi tupanue wigo wa mapato. Kwa sababu ukiweka mazingira ambayo yanavutia kwa mchezaji na mchezeshaji maana yake tutapata fedha nyingi lakini sehemu ya fedha tutenge iende kwenye michezo. Kama ni kugharamia timu ya taifa, timu za riadha , kuboresha viwanja kwa sababu michezo nayo ni sehemu ya kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Salim Khamis na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula ajiandae.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiisikiliza kwa makini taarifa ya Kamati ya Bajeti na ukawasikiliza kwa makini wachangiaji mbalimbali utaona kwamba wanatilia mashaka bajeti yetu hii. Mimi nasema kwamba nina mashaka makubwa sana kuhusiana na bajeti yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia bajeti hii vipaumbele vyake havitoshelezi. Nasema hivi kwa sababu Mheshimiwa Waziri wakati akiwasilisha hotuba yake alisema uchumi umepanda kwa asilimia 7, jambo ambalo ni mashaka makubwa sana. Kama uchumi umepanda, tukija kwenye kilimo, kilimo kimekua kwa asilimia 3.7, ambapo ili uweze kupunguza umaskini kwa wakulima ni lazima kilimo kipande angalau kwa asilimia 8 hadi asilimia 10. Sasa tuna asilimia 3.7 kwa miaka kumi, Mheshimiwa Waziri anasema uchumi umepanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara kilometa 86,472 lakini barabara za lami ni asilimia 9.7 tu, lakini tunaambiwa bado uchumi wetu umepanda. Tunahitaji megawati 3,000 lakini tangu nchi hii ipate uhuru tuna megawati 1,424.6, bado tunahitaji megawati 1,575.4 ili tufikie mahitaji yetu. Sijui ni miaka mingapi tunahitaji ili tufikie lengo hili kwa sababu hizi megawati 1,400 tumechukua miaka 57, sasa megawati 1,500 tutachukua miaka mingapi? Sidhani kwamba katika Bunge hili tutakuwepo na sidhani kwamba CCM itakuwepo katika madaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali Kuu ilitakiwa ikusanye shilingi trilioni 19 lakini imekusanya shilingi trilioni 14, huu uchumi umepanda vipi? Halmashauri zetu zinatakiwa zikusanye Sh.687,304,000,000, zimekusanya Sh.437,607,000,000 ambapo tofauti ni shilingi bilioni 249.699, ni nusu yake. Sidhani hawa wataalam ambao wanafanya tathmini za makusanyo wako sawasawa na wanazijua halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu chochote kinaathiriwa na idadi ya watu. Kila mwaka idadi ya watu inaongezeka asilimia 3.1, katika miaka mitano kuna watu milioni 7.6 kwa hivyo kwa muda wa miaka 10 tutakusanya watu milioni 15.2. Hawa watu wanataka matibabu, madawa, shule na wana mahitaji mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nakieleza, kila mwaka deni linapanda, kwa hiyo, kwa mwaka huu deni limepanda mara mbili ya mwaka uliopita. Kila mwaka wahitimu wetu wanaomaliza shule ni 800,000 lakini Serikali ina uwezo wa kuajiri 40,000, kwa hivyo, kuna watu 760,000 kwa kila mwaka wanakosa ajira. Kwa hivyo, tukifanya miaka mitano tuna watu milioni 3,800,000 wako *bench* wanasubiri ajira, leo tunaambiwa uchumi umepanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ukurasa wa 79 wa kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Mpango katika hitimisho lake anasema:-

*"Naomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla tuunganishe nguvu zetu, vipaji vya wananchi wetu na biashara zetu ili kufikia malengo tunayoyakusudia. Hivyo, tunahitaji uzalendo na nidhamu ya kazi ya hali ya juu tukikusudia kuondoa umasikini".*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri hapa amesema Wabunge na wananchi wote kwa jumla, hii ni kusema kwamba uchumi wa Taifa unategemea wananchi wote. Hata hivyo kwa sasa wapinzani katika Taifa hili wanaonekana ni maadui wakubwa na nusu ya wananchi ni

wapinzani na uchumi unahitaji mshikamano wa umoja katika Taifa kwa mwendo huo uchumi huu utakua kwa kaisi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima kuwe na uhusiano wa kimataifa kwani umeporomoka, haupo. Ni lazima tuwe na demokrasia, demokrasia haipo. Ni lazima tuwe na utawala wa sheria, utawala wa sheria haupo. Ni lazima tuwe na utawala bora, utawala bora unanuka kabisa katika nchi hii. Katika hali hii, vipi tutaweza kujenga uchumi wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nitoe ushauri kwamba turejee nyuma tuweze kuimarisha kilimo. Sijaona msukumo wa Serikali katika kilimo.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid, kuna taarifa. Mheshimiwa Mkuchika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, msemaji aliyekuwa anaongea sasa amesema kwamba utawala bora unanuka katika nchi hii. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa kwamba katika nchi za Afrika Mashariki, Tanzania ni ya pili kwa utawala bora baada ya Rwanda. Wako watu waliobobea katika masuala ya utawala bora likiwemo na Shirika linaitwa *Transparency International.*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, sihitaji kubishana na watu ambao wanaongea bila ruhusa yako, ndivyo walivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkuchika, hawa Waheshimiwa Wabunge huo Uheshimiwa yaani wanawatia mashaka wale watu waliowaleta humu ndani. Mnaitwa Waheshimiwa kwa sababu mna heshima sasa msiwaaibishe watu wenu kwa sababu inaonekana wametuma sampuli za huko, tafadhali. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa kwamba *Transparency International* katika ripoti yao ya mwisho wamesema katika nchi zilizofanya vizuri katika utawala bora ni pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukirudi hapa nyumbani, *REPOA* pamoja na TWAWEZA wamefanya *research* wametoa taarifa kwamba Serikali ya Awamu ya Tano tangu imeingia madarakani utawala bora unakwenda vizuri. *(Makofi)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnazijua Kanuni unampa nani taarifa? Mheshimiwa Khatib kaa chini. Huwezi kumpa taarifa anayetoa taarifa na nyie ni Wabunge wazoefu mnazijua Kanuni zilivyo.

Mheshimiwa Rashid unapokea taarifa ya Mheshimiwa Mkuchika?

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa naibu Spika, taarifa hiyo siipokei, tuna ushahidi wa kutosha, mauaji yanayotokea katika nchi hii, watu wanafungwa hovyo katika nchi hii, maonevu yanayotokea katika nchi hii na ushahidi

upo. Hawezi Mheshimiwa Waziri akafananisha Tanzania na nchi ile ya Rwanda na Burundi, zile ni nchi ndogo sana *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema malengo makuu katika Taifa hili ni lazima tuwekeze kwenye kilimo. Adui mkubwa wa nchi hii ni yule ambaye anashindwa kuwekeza katika kilimo, anashindwa kutoa misaada katika kilimo kwa sababu asilimia kubwa ya wananchi wake wako kwenye kilimo. Serikali bado haijaamua kuwekeza kwenye kilimo. Nchi moja ya Rwanda imewekeza kwenye kilimo takribani shilingi trilioni 7 lakini leo Tanzania wametoa pesa za maendeleo asilimia 11.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, *CUF* mnachangia dakika nane nane kwa sababu mmeleta majina matano badala ya majina manne.

Tunaendelea na Mheshimiwa Ali Salim Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Neema Mgaya ajiandae.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia leo hii kusimama hapa kwa ajili ya kuchangia bajeti hii. Leo mimi nitakuwa zaidi na maswali na nina mambo matatu tu ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimuulize Waziri wa Fedha, makusanyo yote ambayo yamekusanywa ndani ya nchi ni shilingi trilioni 21, matumizi yake ni shilingi trilioni 21, wapi imewahi kutokea makusanyo yaliyokusanywa na matumizi yakaenda sawasawa? Yaani hata shilingi haibaki, *21 trillion* mmekusanya, *21 trillion* mmetumia. Hebu mtuambie ninyi wachumi na watu wa bajeti hii imekaaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ni kwamba ukiacha hayo hizi shilingi trilioni 21 zimekwenda kwenye matumizi ya kawaida tu, deni, mishahara, hizi fedha za maendeleo hapa ziko wapi?

**T A A R I F A**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salim, kuna taarifa.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilindie muda wangu tafadhali.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kumtaarifu Mheshimiwa anayechangia rafiki yangu sana kwamba unaiona kwamba iliyokusanywa ndiyo iliyotumika kwa sababu mfumo wa nchi yetu ni wa *cash budget,* tunakusanya, tunatumia. Kwa hiyo, lazima uone haionekani iliyobakia kwa sababu *cash budget. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salim, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niendelee kwa sababu jana yeye mwenyewe alikiri kwamba siyo mchumi, wapo wachumi hapa watasema kwamba unapokusanya unatumia 100% hakuna hata senti ambayo inabakia unatumia kama ilivyo, watatuambia hapa wachumi wapo, tuna madaktari wawili hapa watatueleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuonyesha kwamba hizi taarifa ni za kutengeneza tuje katika pato la Taifa. Pato la Taifa Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema kwenye kitabu chake kwamba ni shilingi trilioni 50. Sasa hivi Tanzania *current*

*population* ni watu milioni 59, sasa milioni 59 ukigawa kwa shilingi trilioni 50 unapataje 2,275,000 kuwa pato la mtu wa kawaida kwa kila Mtanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wakija hapa watusaidie hizi hesabu zimekaaje kwa sababu ukifanya hesabu hapa, kama ukifanya kwa hiyo milioni 50 maana yake pato la kila Mtanzania ni wastani wa 1,063,000. Sasa hapa Waziri wa Fedha anatuambia kwamba pato la Mtanzania limeongezeka na ni 2,275,000 kwa mwaka wakati yeye mwenyewe amekiri hapa pato la Taifa ni shilingi trilioni 50. Kawaida katika kujua pato la mwananchi unagawa pato la Taifa kwa idadi ya watu ambao unao. Sasa Mheshimiwa Waziri akija hapa atuambie hii hesabu imekaaje. Nasema haya kuonyesha kwamba haya ni mambo ya kutengeneza. Sasa tukisema hii ni bajeti hewa tunakosea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo tuje kwenye masuala ya uwekezaji. Serikali ya Awamu ya Tano ilisema kwamba inafufua Shirika la Ndege kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi hii. Ukichukua taarifa hii ya *CAG* anasema wazi kwamba taratibu za manunuzi ya umma hazikufanyika na Serikali imekiuka Kanuni ya 10(4), Kanuni ya Manunuzi ya Umma katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyopitishwa mwaka 2013. Sasa ikiwa leo utaratibu tu tunaukosea, tunakwendaje kuwekeza na mradi huu uweze kuwa na tija kwa wananchi wa Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zinakinzana, ukiangalia kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Mpango anasema kwamba mwanzo waliomba shilingi bilioni 500 kununua ndege na mwaka 2017/2018 wakaomba tena shilingi bilioni 500 kumalizia kulipia ndege na sasa wameshaomba tena pesa nyingine kwa ajili ya kukamilisha malipo kwa baadhi ya ndege na utaratibu wa kufanya operesheni lakini inatofautiana na kitabu cha Waziri wa Uchukuzi. Waziri wa Uchukuzi anasema mwaka jana wameomba kwenda kukamilisha malipo ya ndege sita lakini leo humu Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango kwenye kitabu chake anasema wametenga shilingi bilioni 495.6 na kuwa wamekamilisha

malipo ya asilimia 30 ya ndege mbili za *CS*3100 wakati huku walisema wanakamilisha malipo, sasa hii biashara mnaifanyaje?

Mheshimia Naibu Spika, nimuombe Waziri akija hapa atupe sera ya ufufuaji wa hili Shirika la Ndege, atuambie hapa sera ni hii kwa sababu ikiwa sera ya shirika imekosekana unatengenezaje *business plan?* Unalifanyaje Shirika lijiendeshe kwa faida? Ukiangalia kuna mashirika kadhaa ambayo yana hali mbaya kwa sababu hapa tatizo siyo kununua ndege, tatizo ni utaratibu wa kuendesha shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Shirika la Alitalia, wanazo ndege lakini sasa hivi linatafutiwa wabia ili waweze kuliendesha shirika. Kuna Shirika la *British Airways* sasa hivi *Qatar* ndiyo wanakwenda kulihuisha lina-*suffer.* Kuna Shirika la *Air* Rwanda limeshafilisika tayari. Kuna Shirika la South Africa sasa hivi linaomba watu wakalisaidie ili lifufuke. Sasa sisi tukisema hapa hatusemi kwa sababu tunaichukia Serikali, tunataka hili shirika liendeshwe kwa faida. Kama tunaendesha shirika kwa kupitia safari zetu za ndani basi tungeanzia hapa halafu baadaye tukaenda sehemu nyingine lakini huku tunakoelekea na ndege ambazo mmenunua inaonekana wazi ndege hizi mnakwenda kuzikodisha kwa mashirika mengine kwa sababu mtakuwa hamuwezi kuzihudumia na wala hamtaweza kufanya ushindani wa kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoyasema haya tunayasema kwa sababu nchi hii ni yetu sote. Ikiwa hamtaki ushauri huu ambao tunawapa matokeo yake mtakuja kuona. Kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tano mnakataa kujibu maswali ya Serikali ya Awamu ya Nne, mnasema Serikali ya Awamu ya Tano imejipambanua, imeamua, inafanya, sasa hii yenu nyie mkimaliza anakuja kujibu nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimalizie kwa kusema kwamba tatizo kubwa linaloonekana ni kwamba Rais amewaamini watu wake lakini wanapomrejeshea taarifa hawamrejeshei taarifa sahihi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

Tunaendelea na Mheshimiwa Dunstan Kitandula atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Andrew Chenge ajiandae.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye hoja zilizoko mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye kwa rehema zake ametuwezesha tumeendelea kuwa wazima na kuwa na afya njema ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia kwenye eneo moja ambalo nisipolichangia nitakuwa sijajitendea haki. Hali yetu ya lishe nchini siyo nzuri. Katika bajeti ya mwaka jana, kwenye fedha tulizotenga ziende kwenye halmashauri zetu ilikuwa ni shilingi bilioni 11 lakini tulipeleka asilimia 8 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa sababu nataka kama Taifa tulione jambo hili ni tatizo. Takwimu zinatuambia nini juu ya hali yetu? Takwimu zinatuambia kwamba asilimia 34 ya watoto wetu walioko chini ya miaka mitano wamedumaa. Takwimu zinatuambia asilimia 58 ya akina mama waliko kwenye kipindi cha kuweza kuzaa wana upungufu mkubwa wa damu. Hii ndiyo hali ya Taifa letu kwamba tuna changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine wakati tuna lishe duni lakini tuna tatizo lingine la lishe iliyopitiliza, viriba tumbo. Ttizo hili linatuletea sasa magonjwa yasiyoambukiza mfano *BP,* kisukari na kadhalika. Kwa hiyo, tuna matatizo ya aina mbili kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Rais wa Benki ya Afrika anatuambiaje? Anasema *stunted children today means stunted economy tomorrow*. Tukiwa na watoto ambao hali yao ni mbaya leo basi tusitegemee kuwa na uchumi mzuri siku zijazo. Ukiangalia hali ya uchumi takwimu zile zinaonyesha kwamba uchumi wetu unakua lakini kwa taarifa hizi maana yake tunakoelekea ni kubaya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mpango mwaka huu hakikisha fedha hizi tulizotenga kwa ajili ya kupambana na tatizo la utapiamlo tunazipeleka zikafanye kazi. Maana wataalam wa *economics* wanatuambia *stunted children today means stunted economy tomorrow. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye eneo lingine, naipongeza Serikali nimeanza kuona jitihada za kuzigeuza halmashauri zetu kuwa ni *center* za *investment,* ni jambo nzuri. Nasema ni jambo nzuri kwa sababu tumeanza kuona *trend* ya kuzinyang'anya vyanzo vyake vya mapato lakini sasa tunapoziwezesha kuwa na vyanzo vingine mbadala vya kupata mapato hili ni jambo nzuri. Maana tumeanza kushuhudia kupitia TAMISEMI tunashawishi halmashauri zianzishe miradi, vituo vya maegesho, standi za magari na mabasi, masoko na kadhalika. Yawezekana ni jambo nzuri lakini uwekezaji huu usipogusa maisha ya mtu wa chini, mtu wa kawaida yatakuwa hayana faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndipo napokuja kwenye lile jambo mahsusi la sisi watu wa Pwani. Tafiti zinaonyesha kwamba *we have unattempted potential* kwenye bahari na maziwa yetu. Mheshimiwa Dkt. Mpango Tanzania tuna Ukanda wa Pwani kilometa 1,424, tuna *EEZ* kilomita 220,000 lakini kwenye eneo la maziwa na mito tuna takribani kilomita 64,500 lakini tunatumiaje rasilimali hii. Uzalishaji wetu wa samaki ukoje? Takwimu zinaonyesha kwenye mpango kwamba kwa takribani miaka mingapi hii, tumekuwa tukivua kati ya tani 325,000 na 380,000. Katika hizo, asilimia 85 uvuvi huu umefanyika kwenye maziwa, asilimia 14 tu ndiyo umefanyika kwenye eneo la bahari. Mbaya zaidi, ufugaji wa samaki kwenye nchi hii, katika hizo tani 380,000 *its only one percent,* hii haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ambayo ina *potential* kubwa namna hii, inachangia ajira asilimia 0.7, haikubaliki. Ukisikiliza taarifa ya Kamati wanasema kwamba tuna tatizo kwenye ajira, tuna tatizo kwenye kuagiza zaidi bidhaa kutoka nje kuliko tunavyoweza kuuza nje, lazima tuwekeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaige wenzetu South Africa, wao kwenye kutatua jambo hili la ufugaji wa samaki, walichofanya wameanzisha *Aquaculture Investment Zone*. Wanachofanya wanaenda kuanzisha *zone* maalum kwenye maeneo fulani fulani, kule *Eastern Cape*, wanazo hizi karibu saba na maeneo haya yameweza kuzalisha ajira karibu 150,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji kwenye eneo hili leo hii wanazungumzia mapato yanayotokana na sekta ya ufugaji wa samaki ya shilingi bilioni 115, sisi hatuzitaki hizi? Wenyewe wamejipanga ndani ya miaka miwili ijayo waweze kufikia mapato yanayotokana na ufugaji wa samaki yanayofikia shilingi bilioni mita tano, sisi hatuzitaki hizi? Mheshimiwa Dkt. Mpango tusaidieni watu wa Ukanda wa Pwani, hizi jitihada mnazotuambia tuanzishe standi za mabasi, masoko, tuwezesheni sisi kwenye ufugaji wa samaki kuanzisha *Aquaculture Special Economic Zone*, tuweze kupiga bao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine, Bunge hili liliridhia tuingie kwenye matumizi ya sarafu moja kwa Ukanda wote huu wa Afrika Masharika. Sijaona kwenye bajeti hii tumeelezwa vipi. Nafikiri ni vizuri kila tunavyokwenda tuwe tunapeana taarifa kwamba maandalizi ya kuelekea huko tumefikia wapi tukijipima na wenzetu. Vilevile tuelezane vihatarishi tunavyoviona, maana taarifa zilizopo wenzetu Kenya wameshafikia ukomo wa kukopa nje. Kila wanavyokopa wamekuwa wakiambiana kwamba deni linahimilika, hii iwe changamoto kwetu kwamba tukope vizuri tusifike huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye eneo la umeme.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA**: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, sasa tutamsikia Mheshimiwa Neema Mgaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Andrew Chenge na Mheshimiwa Hassan Elias Masala ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Dkt. Ashantu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwa kusema bajeti hii ni nzuri kwa sababu imejikita katika kuhakikisha kwamba inalinda viwanda vyetu vya ndani lakini vilevile imeweka urahisi wa kuanzisha viwanda vipya. Kwa mfano, tuna *zero rate* katika viwanda vinavyozalisha mafuta ya kula na mafuta haya ya kula yanatumia malighafi ambayo tunalima ndani ya nchi yetu ikiwemo michikichi, alizeti na parachichi kule Mikoa ya Njombe na Iringa. Naishauri Serikali iangalie upya Sera ya Viwanda na Uwekezaji ili tuweze kuwa na viwanda vidogo, viwanda vya katina viwanda vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naiomba Serikali iweke mkazo katika kuhakikisha kwamba tunajitosheleza kwa kuwekeza kwenye viwanda ambavyo vinazalisha malighafi ili iweze kutumika katika viwanda vikubwa. Kwa vile viwanda ambavyo vinazalisha malighafi vitumie malighafi ambayo zinatokana na mazao yetu humu nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Tunaweza tukatoa mfano tukawa na viwanda vinavyochambua mbegu na pamba, kiwanda hicho kinachochambua mbegu kinaenda kutumika kama malighafi kwenye kiwanda ambacho kinatengeneza mafuta. Hali kadhalika ile pamba inaenda kutumika kama malighafi kwenye viwanda ambavyo vinatengeneza majora ya nguo na majora ya nguo yanaenda kutumika kama malighafi kwenye viwanda ambavyo vinatengeneza suruali, sketi, mashati na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mifumo ya upatikanaji wa mapato kwa kutumia teknolojia ya *IT*. Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake cha bajeti amesema kwamba tutaendelea kuendeleza mifumo ya upatikanaji wa mapato kwa kutumia teknolojia ya *IT*. Ni jambo jema lakini nilitaka kumwambia Mheshimiwa Waziri ili kuendana na mifumo hiyo katika suala zima la ukaguzi ni vyema Serikali ikaweka mkazo kuhakikisha wakaguzi wetu wa ndani na wa nje wanaenda sambamba na teknolojia hiyo ili kuweza kuwasaidia kipindi cha ukaguzi. Kwa sababu kama ukaguzi hautaendana na mifumo hiyo, utatokea udanganyifu mkubwa kipindi cha ukaguzi. Hivyo basi, Serikali ione umuhimu kwa *Internal* na *External Auditors* wetu waweze kupata elimu hii ya teknolojia mpya katika mifumo ya ukusanyaji wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Nimepitia taarifa ya ukaguzi ambayo ilifanywa na Mkaguzi wa Nje, Eng. Maganga Machi, 2018, katika Halmashauri ya Misungwi. Katika mambo ambayo amegundua Mkaguzi huyu kulikuwa na baadhi ya mashine za kukusanyia ushuru ambazo hazikuunganishwa kwenye mfumo zaidi ya miaka miwili. Kutokana na kutokuunganishwa huko kwa mashine hizo za kukusanyia ushuru kwenye mifumo kumesababisha kupotea kwa pesa nyingi ndani ya halmashauri hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tujiulize, wale Wakaguzi wa Ndani wanafanya ukaguzi katika halmashauri kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka *(quarterly)* na muda

wa miaka miwili mashine hizo za *POS* hazikuunganishwa na mfumo na wao wamekuwa wakikagua ndani ya miaka miwili ina maana wamekagua zaidi ya mara nane ndani ya miaka miwili bila kugundua kwamba kuna pesa zinaibiwa mpaka alipokuja *External Auditor* kutoka Mwanza na kugundua kwamba kuna tatizo hilo na kuna pesa ambazo zimeibiwa kwa sababu tu ya hizo *Point of Sale Machine* hazijaunganishwa na mfumo ili kuweza kusaidia ukaguzi wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la gawio la asilimia 5 kwenye halmashauri zetu. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuondoa riba katika gawio la asilimia tano kwa wanawake na vijana kwenye halmashauri zetu. Naiomba Serikali pesa hizo zitoke kwa wakati ili ziweze kwenda kuwasaidia wanawake pamoja na vijana kwenda kufanya maendeleo na vilevile kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye *sanitary pads*, niwapongeze kwa kuondoa kodi katika suala zima la uingizwaji wa *sanitary pads*. Hata hivyo, nilitaka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri tuna viwanda vya ndani ambavyo vinatengeneza *sanitary pad* na lengo letu ni kuvikuza viwanda vyetu vya ndani viweze kufanya kazi vizuri lakini ukiangalia hii kodi iliyoondolewa kwenye hizi *sanitary pads* imewa-*favor* wale watu wanao-*import* hizo *sanitary pads*. Hivyo basi, naishauri Serikali iangalie ni jinsi gani inaweza ikapunguza kodi kwenye malighafi ambayo inatumika kutengeneza *sanitary pads* ndani ya nchi yetu ili hivi viwanda vya ndani viweze ku-*compete* na zile *sanitary pads* zitakazokuwa zinaingia ndani ya nchi yetu, ziweze kushindana vizuri kwenye soko nao waweze kuuza kwa bei ya chini ili ile azma yetu ya kuwasaidia watoto wetu wa kike katika suala zima la kupata *sanitary pads* kwa bei nafuu tuweze kulifikia. *(Makofi)*

Mheshimia Naibu Spika, mwisho kabisa nipongeze kwa msamaha wa *penalty* na *interest* ambayo mmetoa kwa muda wa miezi sita. Mimi nashauri muongeze muda iwe

mwaka mmoja ili kuweza kuwa-*motivate* wafanyabiashara wetu waweze kufanya biashara vizuri na kwa kujiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Andrew Chenge atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Elias Masala na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Nianze kwa kusema naunga mkono hoja zote mbili. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya. Tunaelewa changamoto mlizonazo na kwa hali yetu hii tunaelewa lakini nasema hongereni sana kwa haya ambayo mnayafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia huko tulikotoka miaka 20 iliyopita maboresho ambayo yamefanywa *consistently* na Serikali hasa kuanzia Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne na yanayoendelea sasa ndiyo yamewezesha kuona mafanikio tunayoyaona sasa hivi. Jitihada za Serikali za kuhakikisha kwamba tunakuwa na uchumi wa jumla ulio tulivu, tunajenga mazingira mazuri ya uwekezaji na kufanya biashara, tunaendelea kuwekeza kwenye miundombinu ya barabara, umeme, maji, yote haya ndiyo yanawezesha mafanikio haya tunayoyaona. Mheshimiwa Waziri na timu yenu naendelea kuwapongeza sana pamoja na changamoto za rasilimali fedha ambazo tunazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii mikubwa ambayo Mheshimiwa Rais wetu ameanza kuitekeleza, pamoja na maneno mengi, hii ndiyo itakayochochea zaidi maendeleo yetu. Ujenzi wa reli ya kati kwa *standard gauge* na matawi yake muhimu, maboresho yanayoendelea sasa hivi katika bandari ya Dar es Salaam, niongeze hapo, siyo maboresho tu na upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam lakini napenda

tuanze ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo kwa sababu tunafahamu Bandari ya Dar es Salaam tayari imekuwa *chocked*. Tujenge bandari mpya ya Bagamoyo ambayo itakuwa ni kwa faida kubwa ya Taifa hili kwa miaka 100 inayokuja ili tuweze kushindana na tujenge mazingira ambayo yatatuwezesha kutumia nafasi yetu ya kijiografia kama vizuri kama nchi, tunaweza, tunaweza. Ndiyo maana Mwalimu alikuwa anatukumbusha wakati wenzetu wanatembea sisi tukimbie. Ndiyo maana ya kufanya uwekezaji mkubwa kama huu, ndio una gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia, ni vema tukachukua uamuzi haraka, tukapata *a financing instrument* itakayotuwezesha ku-*fund* reli ya kati na matawi yake tumalize mapema kuliko hii ya kwenda vipande vipande na tutaona jinsi uchumi utakavyokua kwa haraka. Hili linawezekana, ni ombi langu sana kwa Serikali, twende haraka na baadaye mtaona faida kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha tulilisema miaka minne iliyopita mamlaka ya nchi haiwezi ikajiondolea *sovereignty* yake. Nashukuru mmerejesha mamlaka ya Waziri wa Fedha ya kuweza kusamehe pale inapobidi miradi mikubwa kwa faida ya maendelao yetu, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, kwa miradi ambayo tayari iko kwenye *pipeline* maamuzi yafanyike haraka, twende mbele. Baada ya Bunge kama litakubali marekebisho haya tufanye maamuzi ya haraka. Matamanio yangu ni kuona Mradi wa Liganga na Mchuchuma unaanza kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha na ndiyo tutaona faida. Tukianza utekelezaji wa Mradi huo wa Liganga na Mchuchuma mtaona wawekezaji kwa upande wa *PPP* kwa eneo hilo maana mzigo upo. Ndiyo rai yangu kwa Serikali twende haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la *Electronic Tax Stamp*. Ripoti ya Kamati ya Bajeti ni nzuri sana mapendekezo yako wazi. Sasa hivi tunatumia *stamp* za kodi

za karatasi na wanalipia nadhani kama dola moja. Kinachogomba hapa nilivyowasikia Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wamechangia kwenye eneo hili wanasema malipo ambayo atachukua mwekezaji hayawiani vizuri na kiwango cha uwekezaji wake na lingine ni ule muda wa miaka mitano. Bidhaa ambazo tulianza nazo na *stamp* hizi za kodi za karatasi, tunajua ni pombe kali, mvinyo, filamu za wasanii wetu hawa, pamoja na sigara. Pamoja na maeneo ambayo wameanza kutumia mfumo huu ambao una tija sana hawajabeba bidhaa zote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tuanze na bidhaa chache na hasa hizi ambazo tayari zilikuwa zinatumia mfumo huu. Pendekezo langu la pili ni kwamba viwango vya sasa vinavyotumika vya dola moja kwa *stamp* ya karatasi ndiyo viendelee kutumika katika mfumo huu. Tunaweza kuongeza hata bia lakini tusiingize bidhaa zingine kama maji, soda na *juice,* hapana, tusifike huko kwa sasa kwa maoni yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tukienda hivyo tutakuwa tumeliweka vizuri suala hili. Tunataka tujiridhishe na uzalishaji wa ndani wa viwanda hivi na baada ya pale tutaona, Serikali itakuja Bungeni itaonesha, pale ambapo mapato yatakuwa yameongezeka tutakuwa na hoja ya msingi ya kusema sasa twende mbele kwenye bidhaa nyingine, tukienda hivyo tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda mfumo huu mpya tufanikiwe kwa sababu haiwezekani leo Tanzania makusanyo yetu ya ndani yawe *around* 15 au 14.5 chini ya viwango tunavyovifahamu katika *region* hii vya kati ya 17 na wengine wameenda mpaka 20. Naomba sana tuunge mkono jitihada hizi za Serikali lakini tuanze na bidhaa chache ambazo tutazisimamia lakini pia viwango vinavyotozwa sasa ndivyo vitumike, tusiongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutoongeza Ushuru wa Bidhaa na hili tumekuwa tukilisema

na baada ya mwaka mmoja tutaona *numbers.* Napenda eneo hili Waheshimiwa Wabunge Serikali ituelewe, tusiwe tunaenda mbele halafu tunarudi, tuwe *very consistent* tulee *manufacturing industry* ya Tanzania bado *contribution* yake kwenye pato la Taifa ni ndogo sana ya asilimia 5 tunapenda ipande kwa haraka kwa asilimia 10 mpaka 15 na mtaona faida ya uchangiaji wake katika uchumi. Tukienda na hatua hizi za kwenda mbele na kurudi hatutaona tutakuwa tunarudi pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho naomba tuwekeze katika sekta ya kilimo kwa upana wake. *Land bank* ambayo tumeizungumzia kupitia *TIC* tufike mwisho, maeneo hayo yapatikane na tukaribishe wawekezaji wakubwa. Wawekezaji wadogo hawa wakulima wetu wametusaidia mpaka sasa lakini ili kwenda kwa kasi kubwa kwenye kilimo lazima tukaribishe wawekezaji wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ubarikiwe sana kwa kunipatia nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chenge. Nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Hassan Elias Masala, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae.

Kabla hajaanza kuchangia Mheshimiwa Masala nimeletewa ujumbe hapa kwamba kuna Wabunge wanasema mashine ya kupima virusi vya UKIMWI ni mbovu. Waheshimiwa mashine ni nzima, twende tu tukapime. Nimeambiwa kuna Wabunge wanapimwa halafu wanaanza kusema hii mashine ni mbovu. Mashine zile kila moja inatumika, kwa hiyo, hamna mashine mbovu, twendeni tukapime. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Elias Masala.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya bajeti. Nami niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake kwa kutuletea yale mambo ambayo tunafikiri yana manufaa makubwa kwa wananchi wetu lakini kwa Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba nijielekeze kwenye eneo moja linalohusu kilimo. Kabla sijazungumza lolote, naomba nijaribu kumpitisha kidogo Mheshimiwa Waziri na timu yake ili waweze kujua wapi tumetoka. Toka mwaka 2015 wakati tunaingia hapa kwa mara ya kwanza tulitoa mapendekezo kadhaa kwa ajili ya kuboresha mazao yetu makubwa ambayo yamekuwa yanaliingizia Taifa letu kipato. Katika mazao haya lipo zao kubwa la korosho ambalo limekuwa linalimwa kwenye baadhi ya maeneo au kwenye baadhi ya mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada ambazo zimefanywa na Wizara ya Fedha kwa kutondoa tozo tano ambazo zilikuwa kikwazo zimepelekea kuongeza tija lakini pia kiasi kikubwa cha fedha katika mzunguko mzima, kwanza kwa wakulima wetu lakini pia kwa Taifa zima. Kama mwakilishi wa wananchi, nitakuwa mtovu wa fadhila kama sitatoa shukurani kwa sababu ni Mheshimiwa Mpango ndiye aliyefanya kazi ya kuondoa zile tozo za usafiri, unyaufu, kulipa wale viongozi wa vyama vikuu na maeneo yale yote ambayo nafikiri yalipelekea kwa mara ya kwanza kuanza kuuza korosho kwa bei kubwa na wananchi wameweza kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kumpa pongezi hizi kidogo nimepata mashaka kupitia pendekezo la bajeti ambayo iko mbele yetu. Nilikuwa nasoma katika ukurasa wa 69 juu ya azma ya kuleta mabadiliko kwa ajili ya kuhakikisha fedha zinazotokana na mazao ambayo yako chini ya Bodi za Mazao kufikiria kuziingiza katika Mfuko Mkuu. Jambo hili Mheshimiwa Dkt. Mpango na Serikali yangu naomba niseme kwetu sisi kama wakulima hamtakuwa mmetusaidia kwa namna ambavyo mmefikiria. Nimwombe

Mheshimiwa Dkt. Mpango wazo hili ambalo analileta hebu afikirie kuliondoa kwa sababu atakwenda kutugombanisha na wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja kwa nini nasema hivi lakini yako mapendekezo ambayo napenda kwa umakini ayachukue na akayafanyie kazi. Asipofanya hivyo, nafikiri jana amemsikia Mbunge mwenzetu mmoja alikuwa anazungumza kwa utani lakini alichokuwa anakizungumza ndicho kitu ambacho kipo kwa wakulima ambao wametutuma kuwepo hapa ndani. Sisi Wabunge ambao ni wenye Serikali hii tusingependa kuona jitihada kubwa zilizofanywa na Serikali zinaenda kuharibika kwa ajili ya kufanya yale ambayo tunaona hayatatusaidia na wala hayatawasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yale mapendekezo ambayo nataka kuyasema, Mheshimiwa Mbunge mwenzetu wa Mtama wiki mbili zilizopita alikuja hapa na hoja ambayo kimsingi iko *pending* mpaka leo na ilikuwa *pending* kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Mpango wakati tunamuita kwenye kikao cha bajeti aje atuambie liko wapi rejesho la fedha za wakulima ambazo zinafika takribani bilioni 81 bahati mbaya sana hakutokea kwenye vile vikao. Sasa leo anapokuja na mapendekezo ya kutaka kuchukua asilimia 100 ya fedha yote ambayo kimsingi ukisoma hiyo *Finance Act* ya mwaka 2010 inaeleza asilimia 35 itaingia Hazina, asilimia 64 itarudi kwa ajili ya kuboresha zao hili la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la korosho linaboreshwa kwa kununua mbegu, mbegu hizi zinapandwa kwa maana ya miche, wako watu mpaka leo tunazungumza hawajalipwa fedha zao za kazi ambayo wamefanya ya ku-*supply* miche. Pia tunatakiwa tujenge maghala mpaka sasa hivi hatujajenga kwa sababu fedha haijarudi. Mbaya zaidi napozungumza leo wananchi wanagawana mifuko ya *sulphur* kitu ambacho siyo cha kawaida na kitakwenda kuondoa kabisa uzalishaji mkubwa ambao tumeufanya kwa miaka hii mitatu kutokana na mabadaliko tuliyoyafanya. Sasa ukifikiria kuchukua asilimia 100 ya fedha hii kutoka kwenye

sheria hii ambayo nimeitaja, Mheshimiwa Dkt. Mpango anakwenda moja kwa moja kudidimiza na kuua zao la korosho. Pia nimhakikishie kwamba anaenda kuwagombanisha wananchi wa mikoa inayolima korosho pamoja na Chama chao cha Mapinduzi kitu ambacho tusingependa kitokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunampenda sana Rais wetu na tunaamini Rais wetu anatupenda sana sisi wananchi na ndiyo maana alisikiliza kilio chetu, naomba Waziri asirudishe nyuma jitihada za Mheshimiwa Rais katika hili. Waziri akifanya hivi, hata mimi Mbunge wa CCM nakwenda kuungana na wananchi wangu kupinga hicho ambacho anakwenda kukifikiria kukifanya lakini tunakwenda kusimama na wakulima wetu moja kwa moja kuhakikisha maazimio haya ya kwenda kuchukua asilimia 100 ya fedha hii hayawezi kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nafikiri ni vizuri nikashauri na nimwombe Mheshimiwa Waziri kama nilivyomuomba kwanza aende kwenye takwimu. Bajeti tuliyomaliza au tunayomaliza 2016/2017 kwenye bajeti ya kilimo zaidi ya asilimia 10 tu ya fedha ambayo imeidhinishwa ilikwenda. Leo anaposema anaenda kuchukua asilimia 100 ya makusanyo ya korosho au ya mazao yote yaliyoko kwenye bodi na wakati asilimia 90 ya bajeti nzima haijaitekelezwa, ndiyo kusema kwamba hata hizi asilimia ambazo wanataka kuzichukua na kwamba zao hili litagharamiwa na Serikali Kuu tunaenda kufeli. Kwa sababu bajeti ya jumla peke yake tayari tumesha-*prove failure,* tumeshindwa kutoa fedha na hivyo leo kilimo tunachozungumza ambacho ndiyo uti wa mgongo wakulima wetu hawajaweza kunufaika nacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Waziri kwamba zoezi la kwenda kuichukua hii fedha halitakuwa na tija kwa sababu hata hiyo bajeti kuu ya Wizara nzima tumeshindwa hata kufikia asilimia 50 ya utekelezaji wake. Tukichukua hii maana yake unaenda kuondoa moja kwa moja uzalishaji na unaenda kutudidimiza moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nilitaka pia nijaribu kumpitisha Mheshimiwa Waziri ni namna gani ambavyo ataenda kutueleza na ataenda kuwaeleza wakulima. Kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2005/2006, 2006/2007, 2007/2008 tuna zaidi ya shilingi bilioni 201 imekwama katika Wizara yake. Hela hii haijarudishwa na mpaka sasa hivi tunavyozungumza shilingi bilioni 10 tu pekee yake ndiyo imetolewa, tena yenyewe imetolewa kama mkopo kutoka NMB, kama ni mkopo maana yake ni nini? Wananchi wetu wanapaswa kulipia riba ya mkopo huu wakati fedha yetu ya ruzuku ambayo yeye ameshaichukua hajaturudishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo anapoenda kuleta mabadiliko ya sheria na kutaka tubadilishe ili fedha iende Mfuko Mkuu atueleze fedha yetu ya miaka mitatu iko wapi na inaenda kufanya nini? Inafutwa au ndiyo sisi wakulima tayari tumeshadhulumiwa? Kitu ambacho kwa kweli narudia kusema, tena nasema nikiwa na utulivu wa hali ya juu Mheshimiwa Dkt. Mpango asitulazimishe, asitake kututia majaribuni kati ya sisi na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuendelee kuwa watiifu kwa Taifa letu na kwa Rais wetu kwa sababu tunampenda na tunataka awatumikie wananchi. Katika hili Mheshimiwa Dkt. Mpango tunaomba sitisha mara moja zoezi la kwenda kuchukua fedha ya wakulima ambayo nyingine mpaka leo hujairudisha na majibu hujatoa leo unakuja na mapendekezo mengine ambayo kwetu sisi hayana tija na hayatatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la lingine ambalo nataka nilizungumzie ni kuona namna gani ambavyo mapungufu ambayo wao wameyaona kama Wizara juu ya hoja walizozitoa wakati wanajibu kwamba kuna matumizi mabaya kwenye Mfuko wa Uendelezaji wa Zao la Korosho lakini *solution* haiwezi kuwa kwenda kuufuta ule. Nafikiri *solution* ilikuwa ni kufanya maboresho. Fedha ambazo wamezizuia maelezo yanayotolewa ni kwamba kuna matumizi mabaya ya *honorarium* na matumizi mengine, sisi

hatuna tatizo katika hilo na tutaendelea kuunga mkono jitihada za Serikali kupinga matumizi mabaya yasiyokuwa na tija lakini hatuwezi kuzuia na kuua zao zima kwa ajili tu ya eneo moja ambalo tungeweza kulibana kwa maana ya kuwabana watu wa Bodi ya Korosho na wale watumishi ambao wanatumia fedha hii. Yale yanayohusu kununua miche, kufanya utafiti, leo Chuo cha Naliendele hakifanyi kazi yoyote, magonjwa yameanza kuvamia zao la korosho watu hawana fedha za kulipia kwa sababu fedha yote imeingia kwenye Mfuko Mkuu na hairudishwi. Sheria ambayo imetungwa ni ambayo sisi kama Wabunge tunapaswa kuisimamia na tunapaswa pia kuiheshimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri Mpango hebu hapa tunapokwenda kuhitimisha zoezi hili binafsi sitamuunga mkono na naenda kupinga moja kwa moja wazo hili kwa niaba ya wananchi wangu ili tuhakikishe haki na hatima ya zao la korosho inaenda kuimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho atuambie, najua mapendekezo aliyoyatoa siyo kwa zao la korosho peke yake yako mazao mengine kama pamba, kahawa na mazao mengine. Hebu atoe takwimu ndani ya miaka mitatu kila zao ambalo amefikiria na lina bodi ni kwa kiasi gani mazao hayo yameingiza fedha katika Taifa letu? Kwenye kitabu chake kinaeleza pamba tumepata hasara, hapa anachoelekea kukifanya ni kwenda kuua pia zao la korosho ambalo linafanya vizuri kwa kisingizio cha kutaka kuchukua mazao ya Bodi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme siungi mkono hoja mpaka pale jambo hili litakapokwenda kukamilika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga Bananga atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii. Kwanza kabisa napenda kumwomba Waziri wa Fedha na Naibu Waziri wa Fedha watupe taarifa sahihi, nzuri na itakayoturidhisha ambayo tutaweza kwenda kuwaambia wananchi wetu kuhusiana na suala zima la shilingi trilioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili mtaliona kama dogo mkiwa mmekaa kwenye viti vyenu lakini mkienda kule kwa wale ambao mnadhani hawajui masuala ya uchumi ni zito na ni kubwa na wanahitaji majibu ya kuridhisha. Mheshimiwa Naibu Waziri alitujibu hapa hata sisi Wabunge wengine ambao hatujui masuala ya kiuchumi tunajiita mabushi uchumi hatukumuelewa alichotuambia. Watakapokuja kumalizia tunaomba watuambie na watupe kauli ya Serikali wapi iko shilingi trilioni 1.5? Ili na mimi nikitoka hapa nikienda kumwambia mwananchi wangu wa Itonjanda kule Tabora aelewe hii shilingi trilioni 1.5 imetumika vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye bajeti. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hatua yake ya kuamua kwenda kwenye Kiwanda cha Urafiki. Sisi kama wajumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira tulikwenda pale na yale aliyokutana nayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ni masuala ambayo na sisi kama wana Kamati tulishauri na tuliiomba Serikali iende pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kile Serikali ya Tanzania inakimiliki kwa asilimia 49 na China inamiliki kwa asilimia 51. Kwa yanayoendelea pale, tungeiomba sana Serikali na kwa sababu na Waziri Mkuu amekwenda ni afadhali tukamiliki sisi wenyewe ili tuweze kupata faida inayotokana uzalishaji ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *demand* ya nguo za Kiwanda cha Urafiki ni kubwa sana nchi kwetu kuliko hata ambavyo watu wanafikiria. Siku tulipokwenda pale tulikuta

msururu wa magari umepaki pale unasubiri mzigo utoke kiwandani ili waweze kusafirisha. Cha ajabu mzigo hakuna kwa siku wanatengeza khanga chache na nafikiri ndani ya miezi sita ama saba iliyopita walishafunga kabisa hata huo uzalishaji. Hayo ambayo Waziri Mkuu alitaka kuyajua hata sisi Kamati tuliuliza mashine zetu mmepeleka wapi? Hizi mlizoleta mbona hamjazifunga mnasema ni mbovu, leteni zile za kwetu kwanza halafu na hizi mlizonunua ambazo ni mbovu zirudisheni mtuletee nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wizi wa hali ya juu katika nchi hii. Wakati Waziri wa Viwanda akisisitiza viwanda aanze na Kiwanda cha Urafiki ambacho tunamiliki asilimia kubwa sana, asilimia 49 siyo mchezo, hiyo asilimia moja kuichukua ni rahisi sana tukisema jamani sasa ninyi basi mmeshindwa kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna viwanda vya khanga Morogoro vya Textile, viwanda vya khanga vya Nida, vinafanya kazi vizuri sana na ukienda sokoni khanga za Nida na Morogoro ni nyingi ziko wapi khanga za Kiwanda cha Urafiki? Kwa nini Nida na Morogoro wanaweza Urafiki wanashindwa? Lipo tatizo na tatizo hili tunaomba liangaliwe. Tunamshukuru Waziri Mkuu ameingilia kati tunaamini kabisa sasa hivi Urafiki itaanza kufanya kazi kwa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe. Hili neno la Liganga na Mchuchuma nimekuwa nikilisikia toka nikiwa binti mdogo sana. Kwanza nilikuwa naona kama ni kitu fulani cha kuchekesha, nilikuwa sielewi lakini nimeelewa hii Liganga na Mchuchuma ni kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la makaa haya ya mawe linakadiriwa kuwa na zaidi ya tani milioni 428 na wanasema tunaweza kutumia kwa takribani miaka 500 kwa mujibu wa NDC. Chuma kiko zaidi ya tani milioni 126. Hivi ndugu zangu utajiri huu wote tulionao toka tumeanza kusikia Liganga na Mchuchuma, hatujawahi kusikia tumepata mafanikio gani kwenye hili. Hivi hizi pesa ambazo tunazitoa

kutakwenda kununua Bombardier, kujenga viwanja vya ndege, kujenga kuta Mererani kwa nini tusiwekeze kwenye mradi huu ambapo tutapata faida kubwa na ya haraka kabisa. Ndugu zangu tutakapochimba wenyewe chuma chetu tutapata faida kubwa kwelikweli katika hii nchi ya Tanzania ya viwanda ambayo tunaizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kauli mbiu ya Tanzania ya Viwanda na imekuwa ikizungumzwa sana. Mpaka tunakwenda kumaliza bajeti hii, Wizara hii imepata asilimia 9 peke yake ya fedha za maendeleo. Halafu tunasema hii ni Tanzania ya Viwanda, ndugu zangu Tanzania ya Viwanda ipi? Asilimia 9 peke yake kwenye fedha za maendeleo halafu tunajinasibu kwamba Tanzania ya Viwanda, kwenye viwanda vipi? Watendaji wa Wizara ukiangalia maelezo yao na taarifa zao wana mikakati mizuri kwelikweli ya kuijenga Tanzania ya Viwanda lakini hawana pesa. Kwa nini tusiwasaidie ili waweze kutimiza azma ya Mheshimiwa Rais ya Serikali ya Viwanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kumekuwa na fungua fungua ya viwanda vingi sana, tunaambiwa tuna viwanda 3,306, mimi sijawahi kuviona na Mheshimiwa Mwijage anajua hatujawahi kuviona lakini takwimu ndiyo zinavyosema na zinavyoonyesha. Viwanda hivi pamoja na kufunguliwa lakini vipo vingine ambavyo vinafungwa kutokana na ukiritimba wa mambo mengi ikiwepo mambo ya kodi za hovyo hovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa kwenye Kamati lilikuja suala la sukari ya viwandani. Naomba hili niwaambie Wizara ya Fedha, mambo haya mnayafanya mwisho wa siku ng'anya linakuja kuwashukia Wizara ya Viwanda. Ninyi ndiyo mnatakiwa mtoe vibali na msababishe sukari ile iweze kutolewa mwisho wa siku hamtoi na kusababisha viwanda kufungwa. Kiwanda cha Sayona kilifungwa kwa sababu kilikosa sukari. Matokeo yake unaambiwa Wizara ya Viwanda haifanyi kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulileteWa *list* ya viwanda 10 ambavyo walisema tayari vimeshapata vibali vya kutolewa sukari, lakini mpaka tunamaliza kikao cha Kamati walikuwa hawajapata. Nami naendelea kushauri Serikali, kama hawa wafanya biashara wanashindwa kulipia kodi za pale bandarini tengenezeni *bonded warehouse* muweke hizo sukari ili hawa wafanyabiashara wakishakuwa tayari waweze kuchukua mzigo wao wafanye biashara. Leo mmezuia, mnawadai madeni makubwa ambayo na wao wanashindwa kufanya uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine kuna sababu gani ya sukari hii isitozwe kodi ili kupunguza huu urasimu ambao mnausema, mnauona, mnaudai na mnaujua. Kwa nini msitoze kodi? Kwa nini msifanye kama sukari ya kawaida inayoingia ili mfanyabiashara ajue nikiagiza sukari ya kiwandani nitalipa kodi kuliko ilivyo hivi sasa hawalipi kodi lakini mwisho wa siku kumekuwa na urasimu wa hali ya juu. Hali ni mbaya, baadhi ya wafanyabiashara ambao wanaotengeneza bidhaa zinazotumia sukari wanahangaika, wanateseka kupata hiyo sukari waambieni kama kuna kodi waweze kulipa ili maisha yao yaweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu suala la biashara. Watu wanafunga biashara kwa sababu kuna mambo yanayowakera. Mimi kama mfanyabiashara niambieni natakiwa kulipa kodi kwa mwaka kiasi gani nilipe, nikishamaliza hapo niacheni nifanye biashara yangu. Leo kumekuwa kuna ufuatwaji wa wafanyabiashara mpaka inaleta kero. Kuna baadhi ya wafanyakazi wa *TRA* wasiokuwa waaminifu, mmewatengenezea mazingira ya rushwa ya ajabu, Mheshimiwa Dkt. Mpango nilimwamba hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wafanyabiashara na wafanyakazi wa *TRA* wamekuwa wanachukua watu wanakwenda kwenye maduka, ananunua kitu cha Sh.20,000 au Sh.50,000, nimeshuhudia mwenyewe kwa jicho langu, anaambiwa subiri risiti anasema nina haraka. Dakika tano nyingi anarudi na watu wa *TRA* wanakwenda kumdai mtu

Sh.3,000,000 kwamba hujatoa risiti, nimelishuhudia mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapoomba hizo Sh.3,000,000 wakiona mfanyabiashara hataweza kulipa hela hiyo wanaomba rushwa. Kauli wanazotumia wanasema utatoa mita, ukiambiwa kutoa mita ni Sh.1,000,000, ukiambiwa kutoa nusu mita ni Sh.500,000. Mimi ni mwakilishi wa wananchi niliuliza hilo suala na Mheshimiwa Dkt. Mpango *TRA* wapo wengi, hawa vijana mnaowatuma kwenda kufanya hiyo shughuli huko wanakera sana wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sehemu iliyokuwa na tatizo la kupata mlango wa biashara kama Kariakoo. Leo milango Kariakoo inatangazwa. Ukifika unaambiwa mlango huu unakodishwa watu wamefunga biashara zao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bananga. Umeshaongezewa na za ziada hapo ili umalizie hoja yako Mheshimiwa Dkt. Mpango ili aipate vizuri na naamini ameipata vizuri. Pia Mheshimiwa Waziri wa Viwanda ameipata hiyo ya Urafiki nadhani ataanza na Kiwanda cha Urafiki. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pia kuwa mmoja wa wachangiaji wa bajeti hii. Binafsi naunga mkono bajeti ya Kambi Rasmi ya Upinzani iliyozuiliwa kusomwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na ndugu yangu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ukishasema hivyo maana yake umeunga mkono bajeti ya Mheshimiwa Waziri huku kwa sababu bajeti huwa ni moja tu. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba usiniwekee maneno, naunga mkono Kambi Rasmi ya Upinzani.

**NAIBU SPIKA:** Haipo hapa mezani, kwa hiyo, kimsingi umeunga mkono bajeti ya Serikali, ndiyo unachosema hapa. Sasa mimi nakurekebisha ili uweke vizuri maneno yako unasisitiza, umeshaunga mkono bajeti hii na kwa kuwa maneno hujafuta ndiyo utaratibu ulivyo, hamna bajeti ya upinzani hapa ndani, haipo.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ulinde muda wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wake kama tulivyosema bajeti hii ni ya kufikirika na sidhani kama itatekelezeka. Kwanza kabisa Deni la Taifa. Wizara hii ndiyo msimamizi mkuu wa Deni la Taifa na mali za nchi. Toka awamu hii imeingia madarakani Deni la Taifa limeongezeka kwa kasi kubwa sana na yeye kama kiongozi anayehusika haoni kama analiletea Taifa hili changamoto inayotusubiri hapo mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwezi ameji-*commit* na Wizara yake kulipa Deni la Taifa shilingi bilioni 883. Ameji-*commit* na ana wajibu wa kulipa mishahara ya watumishi karibu shilingi bilioni 617 na kuendelea. Wakati huohuo kuna OC shilingi bilioni 254. Mapato, tukiachia mnavyo-*forge* maana mmeeleza mapato ni mengi wakati uhalisia si kweli. Matumizi ni 1.7 lakini mapato ni 1.2, hizi nyingine anapata wapi? Kwa hiyo, namsisitiza kwa faida ya Watanzania na hasa wanawake ninaowawakilisha namwomba awe *realistic,* asiweke *figure* za kufurahisha viongozi au baraza lake, ahakikishe anaweka *figure* ambazo zitawasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, naona niache habari ya Deni la Taifa kwa sababu ni *cancer* ya Taifa. Nataka niingie kwenye habari ya kilimo. Toka tunapata uhuru tulikuwa tunasema kilimo ni uti wa mgongo na kilimo kinachukua zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania, bajeti ya 2016/2017

**TAARIFA**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Tulitenga shilingi bilioni 101 lakini…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kuna taarifa, Mheshimiwa Goodluck.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka nimuweke sawa mama yangu Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kuwa trilioni 1.3 ni mapato yanayotokana na kodi, kuna mapato mengine ambayo yanatokana na wahisani (*development partners).*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mama ni yake wa kambo, kwa hiyo, naelewa anachofanya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachotaka kusema ni kwamba 2016/2017 tuliweka bajeti ya shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya bajeti ya kilimo lakini ni shilingi bilioni 3 tu ndiyo zilitoka. Kama unazungumzia kilimo ni uti wa mgongo na sisi kama Bunge tulipitisha hizo pesa tukijua hata kama hazitoshi zinaweza zikasaidia lakini ikatoka shilingi bilioni 3 peke yake. Mwaka huu tunaoumaliza sasa tulitenga shilingi bilioni 150 lakini mpaka leo zimetoka shilingi bilioni 27 peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ndiyo kila kitu na wewe mwenyewe umetoka kwa wakulima unafahamu, kama pesa haijatoka na sisi Bunge tumepitisha, sioni umuhimu wa kuwepo mahali hapa *unless* tunafanya siasa. Bunge kama chombo muhimu kimesema pesa kadhaa itoke Wizara haijatoa na wanajinasibu wanakusanya pesa nyingi, sielewi wanasimamia mpango gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutoa pesa ndogo kwenye kilimo bado kilimo kinaingiza kwenye pato la Taifa takribani asilimia 30 ya pato la Taifa. Kwa nini kama Watanzania tusione umuhimu wa kuwekeza zaidi kwenye kilimo pamoja na viwanda tunavyovizungumzia tukaweza kupata pesa nyingi isiyokuwa na matatizo. Leo hii tuna Vyuo vya Kilimo, kwa mfano, SUA na Uyole huu ni mwaka wa tatu hawajapata pesa za utafiti. Unawezaje kuwa na kilimo safi hufanyi utafiti?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza kilimo, tunazungumzia mbegu bora, jana kuna mmoja ametoka kuuliza swali juu ya mbegu za alizeti, mkulima kwa gharama yake anapanda mbegu lakini mbegu haioti. Watafiti hawawezi kusema lolote kwa sababu hawajapewa pesa kwa ajili ya utafiti. Leo hii kuna mbegu za mahindi zinapandwa, hakuna chochote kinafanyika kwa sababu hizo mbegu si mbegu bora lakini hatuwezi kuwalaumu watafiti wetu kwa sababu hawana fedha ya utafiti. Tukienda kwenye mambo hayo hayo ya kilimo, katikati ya kilimo kuna mitamba ile inayotakiwa kufanyiwa utafiti hawajapata pesa. Pale SUA Arusha hawajapata pesa kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia habari ya kilimo ambacho kimebeba idadi kubwa sana ya Watanzania na mimi ninayewakilisha Mkoa wa Mbeya asilimia kubwa wewe ni shahidi, wanawake ndiyo wanaoingia kwenye kilimo. Kwa gharama zao wenyewe wanaamua kulima, hawana Maafisa Ugani, wako wachache, hawana maelekezo yoyote mwisho wa siku wameshalima lakini masoko pia hamna. Tumeingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki wenzetu

wamejipanga kwa nini na sisi tusiige, kwa kweli masoko ni shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi nikisimama hapa nazungumzia suala la chai. Mpaka sasa hatuna viwanda vidogo vidogo vya kusaidia wakulima hawa. Hatuna mkakati wa mbolea au kuwasaidia kwa namna yoyote kama Taifa lakini bajeti inayotengwa ni ndogo na hata hiyo ndogo inayotengwa Wizara haitoi pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii bajeti sijajua walifikiria nini au kuna kitu gani wanakifanya? Hali ya hewa huwezi kuitegemea kwenye kilimo. Tanzania tunaishi kwa kutegemea Mungu anasema nini kwa ajili ya kutuletea mvua. Hatujajipanga kwenye umwagiliaji, hatujajipanga kuhifadhi maji ya mvua, tunasubiri Mungu atoe na asipotoa hatuna kilimo. Naomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango tulitazame suala hili kwa upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niende kwenye eneo la wafanyakazi. Sasa hivi imeletwa sheria ya ufutwaji wa Tume ya Mipango. Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango alikuwepo toka awamu iliyopita kwenye Idara hiyo, Marais karibu wanne wamepita hakuna aliyethubutu kufuta hii Idara lakini wanafanya hivyo kwa sababu wanataka wawe huru na kufanya wanavyotaka. Hawataki kuwa na chombo cha kuwasimamia, wanachota hela Bombardier, Chato, hawataki usimamizi. Kwa sababu tukiwa na hii Idara sisi tutaiuliza lakini wanaiondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mfuko mmoja wa mapato ya Serikali wanataka ubadilishwe sijajua wanawaza nini. Hatuwezi kumlazimisha maana ameshika mpinina sisi tumeshika makali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakiki wa wafanyakazi umekuwa kwa muda mrefu, kuna sehemu umemalizika lakini kuna watu walipandishwa madaraja miaka miwili iliyopita hawakulipwa mishahara yao. Umefika wakati wa kulipa mishahara yao sawasawa na madaraja waliyopanda

mnawaambia waandike barua kwa wakati mliosema kwa maana miaka ile mingine inapita bila wao kupewa haki yao, huu ni dhuluma na hii ni dhambi mnaipanda kwenye Taifa hili. Jasho la mtu likipotea, kuna wakati hata tunapeleka watoto wetu shule hawafaulu mitihani kumbe ni pesa ya laana. Umempeleka mtoto shule unalipa ada kumbe ile ada uliyolipa kuna watu wanalalamika mahali fulani. Namuonya Mhesimiwa Dkt. Mpango naomba atetee hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye viwanda, nitazungumzia upande wa Kiwanda cha Ngozi. Hatuna kiwanda cha ngozi na ng'ombe wanagongwa alama tayari hiyo ngozi yao haina thamani. Ng'ombe wanatembea kilometa nyingi, hiyo ngozi haina thamani. Nashauri kuwawekea wafugaji maeneo mazuri ya kulima na kutunza mifugo hiyo ili tupate thamani ya ngozi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda anavyovizungumza Mheshimiwa Mwijage, cherehani tatu anaita ni kiwanda, huku ni kuwachezea Watanzania. Namshauri kaka yangu asifanye vitu kisiasa. Mnapokuwa kwenye *cabinet,* Mheshimiwa Mwijage nakuamini, shauri hali halisi. Mimi nimegawa vyerehani zaidi ya 400, anataka kuniambia mimi ni mfadhili wa viwanda? Hiyo si sawa. *We need the real project,* hatuhitaji kufanya vitu kisiasa, kuwanufaisha Watanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la afya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la afya ni tatizo hasa kwa magonjwa yasiyoambukiza.

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa. Ahsante sana.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau na Mheshimiwa Khatib Said Haji ajiandae.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia katika bajeti hii iliyoko hapa mbele yetu. Kwanza kabisa, napenda niishukuru Serikali yangu kwa namna ambavyo imekuwa ikijitahidi kwa namna pekee kutatua matatizo ya wananchi japo kuna changamto mbalimbali hasa katika ukusanyaji wa pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru Mawaziri, viongozi na watumishi wa Wizara hii kwa namna ambavyo wameweza kuyapokea baadhi ya maoni ambayo tuliweza kuyatoa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ambayo ni pamoja na kuondoa baadhi ya kodi kwenye bidhaa mbalimbali zikiwemo taulo za kike kwa ajili ya watoto wetu wa kike, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, nimwombe Mheshimiwa Mpango ashirikiane na sekta zingine kwa ajili ya kudhibiti ubora wa hizi bidhaa ambazo mmeziondolea kodi. Kwa sababu wakati mwingine zitakuwa zinamnufaisha yule mfanyabiashara mkubwa na siyo mtumiaji. Kwa hiyo, tunategemea sana hizi bidhaa zitashuka bei. Naomba sana muangalie hilo na uwe ni uangalizi wa hali ya juu kwa sababu mara nyingine tutajikuta tunamsaidia tu yule mfanyabiashara mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nije kwenye mapato ya ndani na naomba niongelee ukwepaji wa kodi.

Si kwamba wananchi hawapendi kulipa kodi, wananchi wetu wakipata elimu ya kodi wako tayari kulipa kodi na waelimishwe ni kodi zipi wanapaswa kulipa. Kumekuwa na mlolongo wa kodi nyingi mno ndizo hizo zinamfanya mtu aone kwamba kwa nini kodi zimekuwa nyingi, leo una hii, kesho hii na hii. Ndiyo maana unakuta wananchi wakati mwingine wanaona maafisa wa *TRA* wanatoweka, siyo kwamba hawapendi, wapeni elimu ili wananchi waweze kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishampa Waziri maombi yangu aniletee wataalam wa *TRA* wa kodi waje jimboni kwangu, wawafundishe wananchi haya mambo waweze kuzijua hizo kodi mbalimbali wanazotakiwa kulipa. Zipo kodi zenye kero mpaka leo kama *hotel and service levy* katika baadhi ya halmashauri. Naomba mliangalie upya na muweze kulichanganua wananchi walielewe hata kwa kutumia vyombo vya habari. Naomba wananchi wapewe elimu wanapaswa kulipa nini kwenye hii *hotel and service levy* hasa kwenye zile *guest house* ndogo za vijijini ambazo zinasubiri siku ya mnada wale wauza ng'ombe waende wakalale pale, naomba mziangalie sana. Kwenye halmashauri zingine hasa ya kwangu wananchi bado wanateseka na hawazielewi lakini halmashauri wanalazimika kukusanya kutokana na miongozo waliyopelekewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naomba niongelee kodi za zimamoto. Kodi za zimamoto ni kero. Leo ukienda kununua kiwanja lazima utaambiwa ulipe kodi ya zimamoto, ni mchimbaji mdogo mdogo utalipa shilingi milioni mbili ama tatu, hazina kiwango, hazieleweki, unaanza ujenzi unatakiwa kulipa kodi ya zimamoto. Sasa zimamoto hiyo huduma iko wapi mpaka mtu unamchaji hiyo kodi ya zimamoto? Kwa mfano, kwangu Kavuu, hiyo zimamoto iko wapi? Wanatoka Mpanda Mjini wanaenda kulala kule kwa ajili tu ya ku-*harass* wafanyabiashara wadogo wadogo wenye *guest houses* kwa ajili ya hizi kodi za zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshampelekea Waziri malalamiko haya ya wananchi wangu naomba suala hili

alisughulikie. Waziri alinipa Kamishna wa Kodi akaniletea *bundle* la sheria, mimi sio mwanasheria. Kwa hiyo, naomba sana tunapoleta *concern* zetu zinazotoka kwa wananchi mzishughulikie. Naomba hili la zimamoto lishughulikiwe *specifically* katika Jimbo langu la Kavuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala lingine la ulimbikizaji wa madai mbalimbali ambayo bado wanaendelea kuhakiki. Uhakiki umeanza muda mrefu, sasa ifike mahali tuumalize huo uhakiki tuwalipe stahiki zao watumishi hasa katika sekta ya afya na sekta ya elimu. Naomba tufike mahali uhakiki sasa uishe na tuendelee mbele. Mheshimiwa Chenge ametoka kusema hapa tusipende kwenda mbele na kurudi nyuma, naomba twende mbele. Tukitembea haturudi nyuma hatua zinakwenda mbele na sisi tunataka twende, mbele ndiyo maendeleo. Kwa hiyo, naomba sasa tufike mahali tuwe na ukomo wa huu uhakiki, twende mbele ili tuone tunataka kuwasaidiaje watumishi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nije kwenye vipaumbele katika bajeti hii, nianze na kilimo. Kwa kweli bado hatufanyi vizuri, naomba tukiri ukweli katika sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo. Hata leo tukiangalia bajeti yao, ukiijumlisha sidhani kama inafika shilingi bilioni 100 kwa sekta zote tatu. Sasa hivi tumejikita kwenye miundombinu, reli hizo zinajengwa najua itafika mpaka Karema kwetu kule ili tuvushe mizigo mpaka Kalemii (Kongo) lakini tutasafirisha nini? Kama kwenye *production* hatutaki kwenda sambamba na uwekezaji katika miundombinu, haya mazao hayapo, miundombinu ipo sidhani kama inakaa vizuri. Kwa hiyo, kama kweli tuna nia ya dhati, naomba tuwe na ulinganisho kati ya *production* na hizi *means* za usafirishaji. Kwa maana kwamba mazao yetu sasa ndiyo yatabebwa na hizo reli ili yaweze kusafirishwa tupate kurudisha pesa ambayo tutakuwa tumeitumia katika kujenga reli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia upatikanaji wa pembejeo bado ni tatizo. Mwaka jana katika bajeti hii

niliongea, nikasema nawaomba muangalie jiografia na hali ya hewa ya maeneo mbalimbali. Kwa mfano, Mikoa ya Kusini Magharibi mvua zake zinaanza mapema, sasa mvua zinaanza mwezi wa tisa unapeleka pembejeo mwezi wa kumi au kumi na moja, unategemea nini kwa mkulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia angalia katika msimu wa mwaka huu kilimo cha mahindi imekuwa ni kilio kila sehemu na huyo mdudu mnayesema ametoka *America* sijui alikuja na nini, hata sijui? Kutoka America mpaka Tanzania tena Tanzania yenyewe Kavuu ambako sina hata barabara sasa sijui huyo mdudu alikujaje, ninyi wataalam mnajua. Naomba sana myaangalie haya mambo pindi mnapokuwa mnaleta vitu hivi hasa pembejeo kwa wakulima. Kama mnafanyia utafiti wa kutosha ni vyema mkaleta kule lakini ni vyema pia zikawahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie pia kwenye uvuvi na mifugo. Leo hii gumzo ni kupima samaki kwa rula, jamani! Hebu tufike mahali tuone tunafanyaje kazi, tusikurupuke.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nije kwenye huduma za jamii hasa upatikanaji wa maji. Tulipendekeza kwenye bajeti iliyopita kwamba iongezeke tozo ya Sh.50. Sasa hivi tuna tozo ya Sh.50, tukapendekeza iongezeke Sh.50. Leo umekuwa shahidi maswali ya maji yaliyokuwa yakiulizwa ni upatikanaji wa maji kwenye shule za msingi, sekondari, *A-Level.* Siyo hivyo tu, akinamama wanabakwa na wanauawa kwa imani za kichawi wanapokwenda kutafuta maji na mama sasa hivi hawezi kutembea peke yake. Nayaongea hayo wenzangu wa Shinyanga mnayafahamu, jimboni kwangu yanatokea, wanawake hawawezi kwenda kuchota maji sasa hivi kutokana na umbali mrefu kuogopa imani za kichawi za kunyongwa na kutupwa hovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri aongeze tozo hii ili maji yaweze kutosha tuwe na tozo ya Sh.100 katika Mfuko wa Maji. Nina uhakika tutayatatua haya matatizo na tutawaondolea vifo ambayo si vya lazima akina mama. Kwa

sababu sasa hawaendi mabombani kwa kuogopa kunyongwa, ni mbali. Hebu ongezeni hii pesa ifike Sh.100. Tumepunguza bei ya hizi *pads* kwa nini sasa tusiwawekee maji shuleni? Unakuta mtoto ana fagio, dumu na begi anaenda shuleni. Naomba sana ongezeni tozo ya Sh.50 ili tuwe na uhakika wa kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye elimu na afya, naomba muongeze pesa na iweze kutoka kwa wakati. Halmashauri hazina pesa za kutosha kutekeleza miradi, naomba Serikai yangu sasa ule ucheleweshaji wa kupeleka pesa kwa ajili ya miradi kwenye halmashauri na wenyewe ufikie ukomo. Pindi tunapopitisha bajeti, pesa ziende kwa wakati na miradi itatekelezwa kwa wakati.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, mengine nitaandika kwa maandishi lakini naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji na Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea ajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nianze kuungana na wale wote ambao wamepeleka pongezi zao kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. Pia nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote kwa kutuletea bajeti ambayo kwa kweli kwa kiasi kikubwa sana inaakisi yale mawazo yetu tuliyoyatoa na Mheshimiwa Waziri ameya-*accommodate* mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi Wabunge tumekuwa tukiambiwa sana kwamba tumekuwa Wabunge

wa kutumia, kila siku tunadai hospitali, shule, barabara na kadhalika hatuji na mawazo mbadala namna gani Serikali inaweza ikapata mapato. Katika mchango wangu wa leo najikita zaidi kutoa namna mbadala ambapo Serikali inaweza ikapata mapato mengi sana na ndiyo utakuwa mchango wangu kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kule nyumbani. Mheshimiwa Waziri tuliteta siku moja lakini naomba leo niliweke hapa hadharani na naomba sana alifanyie kazi. Kule Mafia tuna Taasisi ya Hifadhi ya Bahari inakusanya maduhuli, si wajibu wao, wanaifanya kazi ile siyo kwa ufanisi mkubwa. Niliomba maduhuli yale kutokana na watalii wanaoingia Kisiwani Mafia yachukuliwe na *TRA* maana ndiyo wataalam wa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Taasisi ya Hifadhi ya Bahari tunaitwika kazi nyingi. Kazi yake iwe ni kuhakikisha kwamba wanahifadhi mazalia ya samaki na shughuli nyingine za mambo tengefu yale. Mambo ya mapato wangechukua *TRA,* kuna kama shilingi bilioni mbili mpaka shilingi bilioni tatu kwa mwaka, kama mtatuletea *TRA* tutapata mapato mengi. Ofisi ya *TRA* ipo pale Mafia, wanaweza kukusanya yale mapato na Serikali ikapata pesa nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nimemuona hapa Waziri wa Nishati. Pale Mafia tuna kisima cha gesi kilichimbwa takriban miaka 10 au 15 iliyopita na Kampuni inaitwa *M&P - Maurel and Prom,* mwanzo waligundua kuna gesi nyingi sana pale lakini baadaye kukawa na *technical problems* hawakuweza kuendelea na kazi ile. Walipokuwa tayari sasa kwa ajili ya kuanza kuchimba na kuipata ile rasilimali ya gesi iliyopo Kisiwani Mafia, leseni yao ikawa imekwisha. Mpaka leo hii wanahangaika *TPDC,* Wizarani na kila mahali ili waweze ku-*renew* ile *license* yao waweze kuendelea na uchimbaji wa gesi ambayo imeonekana ipo nyingi sana katika Kisiwa cha Mafia. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati namwona hapa wahakikishe kwamba wanaharakisha huu mchakato wa hii kampuni ya *M&P*

wapate hii *license* waje wamalizie kazi ambayo tayari walishaianza pale Kisiwani Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka niishauri Serikali namna bora ya kupata mapato ni eneo la uvuvi hususan katika bahari kuu. Nilipata bahati na heshima kubwa ya Mheshimiwa Spika kuwemo katika Kamati ile ya masuala ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Tumeona mambo mengi lakini kwa ufupi tu ningeomba kumshauri Waziri wa Fedha muende mkaitafute ripoti ile, siwezi ku-*summarize* yale yote kwa muda huu wa dakika hizi chache nilioupata hapa lakini kuna habari nzuri sana mle ambazo zinaweza zikaisaidia Serikali yetu kupata mapato mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa ufupi tu kuna suala la bandari ya uvuvi na hili limezungumzwa sana. Mwaka wa Fedha 2014/2015 zilitolewa shilingi milioni 350 na Wizara ya Fedha kwenda Wizara ya Uvuvi ili kuanza masuala ya usanifu ili kuhakikisha kwamba bandari ile inajengwa lakini zile pesa sijui zilipotea wapi. Mwaka jana hii bajeti tunayoimaliza kesho kutwa zimetengwa shilingi milioni 500, hazikuwahi kutoka kutokana na makusanyo madogo. Bajeti hii zimetengwa shilingi milioni 500 nyingine kwa ajili ya usanifu wa kujenga bandari ya uvuvi lakini mpaka sasa bado haijaamuliwa *site* itakuwa wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kuishauri Serikali kwa kuwa tayari tuna mradi wa kujenga Bandari ya Bagamoyo, kwa nini msiunganishe Bandari ile ya Bagamoyo kukawa na *section* ya bandari ya uvuvi? Tunakosa mapato mengi sana katika uvuvi ule wa bahari kuu kwa sababu tu hatuna bandari ya uvuvi. Bandari ya uvuvi *multiplier effect* yake ni kwamba *value chain* yake ni kubwa sana inaweza ikatusaidia sana kupata mapato mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tulizungumza habari hapa ya kuwa na meli ya uvuvi, sikuliona suala hili katika bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, sijui wazo lile limefia wapi. Tuwe na meli zetu wenyewe ambazo zitakwenda mpaka kwenye maji ya kina kirefu kwa ajili ya

kupata mazao mengi ya uvuvi. Tumewaachia makampuni ya nje, yanakuja yanachuma, yanaondoka na bahati mbaya sana na katika eneo hili Mheshimiwa Naibu Waziri nimemuona, wahakikishe wanawaambia *TRA* basi walau waweke *mechanism* nzuri ambayo itatoza kodi katika hizi meli kubwa ambazo zinatoka nje, zinakuja hapa kwetu, zinavuna rasilimali lakini *TRA* hawakusanyi hata senti tano. Kwa hiyo, ni eneo ambalo tunaweza tukasema ni oevu, mnaweza kuangalia namna gani mnaweza mkaongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kulikuwa na sakata hapa la kupima samaki kwa rula. Mimi natokea Mafia, sisi ni wavuvi, kimsingi bajeti hii kwenye uvuvi wametusahau, hakuna kitu, kuna asilimia 0.01ya pesa zimewekwa pale kwa ajili ya mambo ya maendeleo kwenye tasnia hii ya uvuvi, kwa hiyo, tuna tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi navyozungumza na bahati nzuri nimemwona Waziri wa Uvuvi kule Mafia kimsingi tuna kiwanda kikubwa sana cha kuchakata samaki pale cha wale *Tanpesca* na *Alpha Logistics,* kinakaribia kufungwa. Walikuwa kila mwezi wanaondoa pale tani 20 mpaka tani 25 za samaki lakini kutokana na haya matamko yaliyokuja sasa hivi kiwanda kile kinashindwa kutoa samaki kwa sababu kuna samaki aina kama ya misusa, ngalala, hao ukubwa wao hakuna namna wanaweza wakaongezeka zaidi ya hizo sentimeta mnazozitaka ninyi. Kwa hiyo, wale ndugu zetu wa *Tanpesca* wamekataa kununua samaki kutoka kwa wavuvi wadogo kwa kuhofia kwamba huenda wakakamatwa. Hawa samaki niliowataja Mheshimiwa Waziri akae na wataalam wake waruhusiwe kuvuliwa kwa sababu hao samaki hakuna namna wanaweza wakaongezeka ukubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ile ilikuwa kila mwezi wanaleta tani 20 mpaka tani 25 sasa hivi huu mwezi wa tatu meli haijaja kwa sababu samaki wote wanaokwenda kule wanakuwa ni *reject.* Siyo wanakuwa *reject* kwa sababu labda umri haujafika, hapana! Hawa samaki kwa maumbile yao hawawezi kufika hizo *size* ambazo Wizara imeziweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na kuwa Serikali ina nia njema ya kuhakikisha kwamba tunapamba na uvuvi haramu, naomba Waziri au wataalam wake waende Mafia, wakae na wavuvi, waangalie ni aina gani ya samaki wanakua kiasi gani. Kwa sababu mnatoa matamko au sheria lakini msiangalie kwamba samaki duniani au hapa Tanzania wapo kwenye maziwa tu kwenye bahari kuna *species* mbalimbali za samaki na zinakuwa na ukubwa tofauti ambao hauwezi kufikia pengine hivyo viwangowanavyovizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo suala la utalii. Sisi Mafia kule pamoja na uvuvi, kitu kingine kikubwa kule ni utalii lakini a*ccessibility* ya Mafia ni kama haipo, kwa sababu usafiri una matatizo. Nashangaa sana, bahati mbaya watu wa Uchukuzi hapa hawapo, lakini Bakhresa ameipa Serikali meli ile *(sea bus)* ije Mafia. Meli ile ina matatizo madogo tu ya kurekebishwa lakini mpaka leo Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi bado wanaendelea na taratibu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Mafia wanateseka, hakuna usafiri, wanapanda *boat* mbovu ambazo siyo salama, wanahatarisha maisha yao, lakini Serikali imeshapewa *boat* kinachotakiwa ni *logistics* za kumaliza ili kuhakikisha kwamba ile meli inakuja Mafia na inaanza kazi. Kwa bahati mbaya sana ndugu zetu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano wanasuasua. Kwa nini hawataki kuiruhusu ile meli ikaja kuanza kazi Mafia hata kesho kutwa, kwa sababu tumepewa bure tu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Khatib Said Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea na Mheshimiwa Rehema Migilla atafuatia. Hawa wote watatu watachangia dakika nane nane.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kupata nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, nitaunga mkono hoja yake kwa mara ya mwanzo iwapo atatu ridhisha kwa majibu ya maswali yetu tunayoyatoa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la *TRA.* Wafanyabiashara wa Tanzania wanateseka sana kwa matatizo yanayosababishwa na Maafisa wa *TRA*. Kilio cha Waheshimiwa Wabunge ni matokeo halisi ya kinachofanyika huko nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Jiji Kuu la kibiashara la Dar es Salaam, maeneo ya Kariakoo, fremu nyingi zimefungwa na wafanyabiashara wameamua kuacha kufanya biashara kutokana na manyanyaso yanayotokana na *TRA*. Maafisa wa *TRA* wanajipa uwezo mkubwa wa kuandaa mazingira, Mheshimiwa Hawa amezungumza vizuri, nami namuunga mkono sana kwa alichokizungumza. Bahati nzuri kafikia mpaka kuwa shahidi wa matendo ya udhalilishaji wanayoyafanya baadhi ya Maafisa wa *TRA* wasio waaminifu kwa wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara hususan wadogo wadogo wa nchi hii ni watu ambao wanajiandalia mazingira; maana mitaji yao kuanzia mwanzo wa biashara zao ni watu ambao hawana msaada wowote unaotokana na chanzo chochote cha Serikali, ni jitihada zao binafsi zinazowafikisha mpaka kupata mitaji wakaanzisha biashara zao ndogo ndogo. Bahati mbaya sana mfanyabiashara huyo

mdogo wa Tanzania, anapopata wazo tu la kufanya biashara, anapoenda *TRA* kutaka kuanza hiyo biashara yenyewe, kwanza anaambiwa lipa kodi ya mapato. Hata biashara hajaifanya anatakiwa kulipa kodi. Kuna kitu kinaitwa *clearance,* hiyo huwezi kuipata kama hujalipa kodi ya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwaulize *TRA,* kodi ya mapato iliyotokana na nini? Hebu mtuambie, hiyo kodi ya mapato inatokana na nini? Ana wazo la kufanya biashara, anaenda kutafuta *certificate* zinakazomruhusu kufanya biashara lakini anaambiwa kwanza lazima ulipe *clearance*, ulipe nini, umepata nini na kutoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kufungwa fremu za Kariakoo siyo tija kwa *TRA* wala kwa Taifa. Matokeo ya wafanyabiashara kuhama nchi wakaenda kufanya biashara nchi za jirani siyo tija kwa Taifa hili. Mnapofanya jitihada za kuongeza mapato, lazima mzingatie mambo haya muhimu sana. Busara itumike katika kukusanya kodi, pia lazima kodi zetu ziendane na uhalisia wa kipato cha anayelipishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu vya ajabu sana. Nataka kutoa mfano mdogo. Leo hii ukileta kontena la vitenge kutoka nje, kodi inayotozwa na *TRA* kwa takwimu zao na hesabu zao, ni karibia shilingi milioni 80, kontena moja. Matokeo yake wafanyabiashara wanaingiza vitenge lakini kinachofanyika inakuwa ni *transit goods,* zinaishia nchi jirani ya Zambia. Kontena zinaenda Zambia na Uganda. Wanafungua kule na wanazirejesha ndani ya nchi yetu kwa njia za vichochoroni, njia zisizo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda leo Kariakoo utakuta vitenge vya nje vingi vinauzwa lakini nenda kwenye taarifa za *TRA* uone ni kontena ngapi za vitenge zimelipiwa, mtakuta hamna lakini kwenye soko la vitenge Kariakoo vimejaa tele. Kwa sababu ukienda Zambia kontena la vitenge haliwezi kuzidi shilingi milioni 20, lakini ninyi

mmejiwekea kodi ya shilingi milioni 80, mmetaka yote, mmekosa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, bidhaa ya magari yaliyotumika. Sheria za Kodi zilizoweka viwango, sina tatizo, asilimia 25 ni *import duty, excise duty* zote siyo tatizo. Tatizo linakuja kwenye *valuation* ya gari iliyotumika kutoka nje. Hivi tokea lini kitu cha kununuliwa mnadani *TRA* wanakiwekea *valuation,* yaani hiyo ni bei ambayo haitikisiki. Umeona wapi? Kitu cha mnada maana yake inategemeana na bei ya soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Suzuki Carry* hata uki-*google* hapo utaikuta Japan inauzwa dola 500, 700 mpaka 1,000. Rudi kwenye *tariff* za *TRA,* utaikuta imewekewa *valuation* ya dola 3,000*.* Maana yake akileta gari lile maana yake analipia kodi ambayo siyo halali kwa sababu sheria inataka *valuation* itozwe kulingana na viwango vya kodi ya *TRA*. Sasa vitu vya mnada toka lini vikawekewa *indicative price* ambayo inatumiwa na *TRA*? Hii inasababisha watu watafute njia nyingine za vichochoroni kupitisha magari yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii gari aina ya *Land Cruiser V8* ushuru wake unafikia shilingi milioni 80. Tembea, *Land Cruiser* zote zilizopo nchini, asilimia 90 ni ya msamaha wa kodi, ni la Msikiti, Kanisa hata kama wanaoendesha siyo wenyewe. Hii ni kwa sababu ya kodi ya shilingi milioni 80 laiti kodi ingewekwa shilingi milioni 25, 30 au 40 watu wangelipa, lakini mnataka nyingi, mnakosa vyote. Tuliache hilo, lakini nawaambieni tena, rudini muangalie, Maafisa wa *TRA* wanachowafanyia wafanyabiashara kinawaudhi na tena kinakera na sisi wawakilishi wao tunasema na naomba mchukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kilio ambacho wenzetu wa Kusini wanalia sana. Tunaapa hapa kila asubuhi, tunamwomba Mungu kwa dua kwamba tuwatendee Watanzania haki na tunamwombea sana Rais wetu Mungu amwongezee hekima ili yeye na sisi tunaoshauri tutimize haki kwa Watanzania. Watu wa Mtwara au watu

wa Kusini wanalia kilio hiki kwamba pesa zao wenyewe mnazizuia, humtaki kuzipeleka wakaendeleza maisha yao, nia ya Waziri ni nini kwa wananchi wa Kusini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamdhihaki Mungu kwa sababu tunapomlilia Mungu kwa kiapo na tunapoanza harakati zetu kwa kiapo cha kuwatendea haki Watanzania, tunakuwa tunamshtakia mambo yetu Mungu leo tunamdhihaki Mungu. Mheshimiwa Jenista ni hodari sana kusimama anapodhihakiwa Mheshimiwa Rais hapa lakini sio hodari wa kusimama anapodhihakiwa Mungu kwa kutowatendea haki Watanzania, hata kidogo. Akiguswa Mheshimiwa Rais, najua anatimiza wajibu wake lakini tutimize wajibu, asidhihakiwe Mungu kwa kutokuwatendea haki Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanacholilia watu wa Kusini ni haki yao, siyo kwamba wanaomba, ni chao wenyewe. Serikali inayosema imeongeza makusanyo, uchumi umekua, mko vizuri lakini nawaambieni, kama uchumi kukua ni hivi, maisha ya Watanzania yalivyo, ni afadhali ule utawala wa Mheshimiwa Kikwete uliopita ambao ulionekana unawapigaji, una wanaosafiri nje sana, kuna hewa nyingi lakini bado tija kwa Watanzania ilionekana. Serikali iliyodhibiti leo watumbuaji wanatumbua mpaka pesa za wakulima wa korosho wa Kusini. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea atafuatiwa na Mheshimiwa Rehema Migilla na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ajiandae.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuchangia machache katika bajeti hii. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya, nimeweza kumaliza Mfungo wa Ramadhani mimi na wapiga kura wangu wa Temeke na leo tunahitimisha siku za ziada sita katika kuukamilisha ule Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja iliyokuwa mbele yetu, nina mambo matatu tu ya kuyagusia endapo muda utanitosha. Kwanza, nitapenda kugusia pato la kila Mtanzania, mfumuko wa bei na mwisho nitamalizia na hujuma ya Serikali dhidi ya zao la korosho kule Mikoa ya Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla Mheshimiwa Waziri hajawasilisha hotuba ya bajeti yake, alitangulia kutoa Taarifa ya Hali ya Uchumi hapa nchini. Katika kuizungumzia hali ya uchumi hapa nchini yako mambo ambayo yameandikwa kwenye kitabu hiki ukiyasoma kama Mtanzania kwa kweli hayaeleweki. Nadhani Mheshimiwa Waziri alikuwa analenga kuwafurahisha pengine Wazungu, *World Bank* au *IMF* ili Serikali iendelee kupata sifa za kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema Serikali ya Awamu ya Tano imejitahidi kupandisha pato la Mtanzania mmoja mmoja kutoka Sh.2,086,000 mpaka Sh.2,275,000. Maana yake Mtanzania mmoja sasa pato lake limepanda kutoka Sh.5,700 kwa siku mpaka Sh.6,300 kwa siku. Nikajiuliza hii ni sifa au ni kejeli? Kwa sababu kipimo cha pato la Mtanzania ni kumwezesha kupata milo mitatu. Sasa kama tunajisifu kwamba tumemuwezesha Mtanzania kupata Sh.6,300 kwa siku, hiyo itakuwa ni kejeli, haiwezi kuwa sifa, kwa sababu Sh.6,300 huwezi kupata angalau mlo mmoja uliotimilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikajaribu kuingia sokoni, nikanunua tembele la Sh.1,000 kwa maana ya mafungu mawili, nikanunua unga nusu kilo Sh.1,200, nikanunua mkaa kipimo kidogo Sh.3,000, nikachanganya na pilipili, nyanya na

kitunguu Sh.6,300 imekwisha sijapata mafuta ya kula na chumvi nikaombe kwa jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunaleta bajeti ambayo ni ya kumwezesha Mtanzania kupata ugali na tembele la kuchemsha ndiyo uwe mlo wake mmoja wa siku nzima, nikagundua kwa nini Mheshimiwa Waziri pia alisema, akiwadhihaki tena kwamba umri wa Watanzania *average* ya kuishi ni miaka 64, *it is obvious.* Kama mlo wako wenyewe ni mmoja wa ugali na tembele la kuchemsha, utawezaje kuishi zaidi ya miaka 50? Hapo hujaumwa, yaani uombee usiumwe na hiyo familia iwe ni wewe ni mkeo au mke na mume ndiyo mtapata huo mlo mmoja wa ugali na tembele la kuchemsha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni dharau kwa Watanzania na ndiyo maana Serikali ya Chama cha Mapinduzi mnapenda sana sifa, mkisimama majukwaani muda wote mnajisifu, tumenunua *Bombardier*, tunajenga *standard gauge*, *stiegler's gorge,* hata siku moja hamjawahi kusema kwamba mmemwezesha Mtanzania sasa anaweza kupata mlo mmoja wa ugali na tembele la kuchemsha ni kwa sababu mnatambua hii siyo sifa, ni kejeli lakini kwenye kitabu hiki mmeiandika. Ndiyo maana nikasema, kitabu hiki pengine kilikusudia watu wengine nje ya nchi hii lakini siyo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pato linakwenda sambamba sana na mfumuko wa bei. Mtanzania leo hata ukimwezesha apate Sh.20,000 kwa siku, kama haitoshi kumwezesha kupata milo mitatu, ni sawasawa na bure. Kwenye Taarifa ya Hali ya Uchumi Mheshimiwa Waziri anasema, Serikali ya Awamu ya Tano imeweza kupunguza mfumuko wa bei. Nikajiuliza, ni bei za vitu gani ambazo Serikali imedhibiti? Ni bei ya chumvi, *biscuit* au ya *Big G*?

**TAARIFA**

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea, kuna taarifa.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilindie muda wangu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mbunge wangu. Anachozungumza ni suala la takwimu, nami ni mtaalamu wa takwimu na kwa sababu unalihutubia Taifa, nikaona nikupe taarifa. Tunapozungumza wastani wa kipato cha Mtanzania, tunahesabu kuanzia mtoto aliyezaliwa leo mwenye siku mbili au wiki moja. Sasa kama mtoto anazaliwa leo anaweza kula kiasi hicho, inakuwa ni miujiza, mpaka mzee mkongwe, kwa hiyo, ni wastani wa watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifikia takwimu hiyo, tutakuwa na ahueni. Ndiyo maana tunasema, ifikapo 2025 wastani wa kipato cha kila Mtanzania iwe ni dola 3,000. Usiwe na wasiwasi, ni suala la takwimu. Kwa hiyo, takwimu ndivyo zilivyo, wanapokwambia wastani, kuna mtu yuko juu mwisho na mtu mwingine yupo kwenye *extreme*. Awe na amani, tunakwenda vizuri na 2025 itakuwa dola 3,000 kwa kila mtu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Mtolea, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa yake kwa sababu anakiri kwamba kweli kwenye huo huo wastani, Watanzania hawapati milo mitatu, mpaka tusubiri mwaka 2025 tutapata milo mitatu. Kwa hiyo, yupo sahihi, ananiunga mkono kwa hiki nachokisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nikasema pato la mtu mmoja mmoja kama halimwezeshi kupata milo mitatu kwa kesi yetu hapa Tanzania, hata kama atakuwa anapata Sh.20,000 haiwezi kumsaidia. Ndiyo maana

nikasema huo mfumuko wa bei wanaosema wanau-*control* ni upi? Kwa sababu kama mfumuko wa bei ungekuwa *controlled* vizuri, Mtanzania hata angepata Sh.2,000 kwa siku, angeweza kumudu milo mitatu. Sisi kesi yetu ni milo mitatu tu hapa, wala siyo kiasi gani kinaingia mfukoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema wamepunguza mfumuko wa bei mwaka 2017, Serikali ya Awamu ya Tano wakati inaingia madarakani bei ya kilo moja ya sukari ilikuwa Sh.1,200, mwaka 2017 bei ya sukari ika-*shoot* kutoka kilo Sh.1,200 mpaka Sh.2,500/=. Wakalieleza Bunge hili na Taifa hili kwamba hiyo ni hujuma ya wafanyabiashara wameficha sukari kwenye *godown* na kwamba wataitafuta kwa gharama yoyote ili bei ya sukari irudi kwenye bei yake ya kawaida. Leo ni mwaka 2018 hawajarudi kutuambia walipata sukari kiasi gani kwenye *godown* na wameipeleka wapi? Cha ajabu zaidi, bei sasa imekwenda mbali zaidi, kilo ya sukari leo ni zaidi ya Sh.3,000. Sasa unajiuliza, bei ambayo wanai-*control* ni ya vitu gani, mbona hatuioni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tu hapa ikatoea tena *crisis* ya mafuta ya kula na Mheshimiwa Waziri Mkuu akaahidi hapa ametoa siku tatu. Utakumbuka maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yalikuja baada ya Waziri wa Viwanda na Biashara kutoa tamko hapa Bungeni kwamba malighafi ya mafuta iliyopo nchini haiwezi kusababisha bei ya mafuta ipande, hata kama ile meli itachelewa kupakua mafuta. Ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kupitia maelezo hayo akasema hapa, natoa siku tatu, mafuta yaliyofichwa yatoke. Mpaka leo bei ya mafuta ipo juu, haijashuka na hatujapewa taarifa yoyote. Tukisema tuna-*control* mfumuko wa bei, ni bei za vitu vipi? Hivi vitu ndiyo vinagusa maisha ya Mtanzania ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lililopita hapa lilipandisha bei ya mafuta ya taa kwa sababu ya kukomesha uchakachuaji. Walisema kabisa kwamba wanafanya hivyo kama *temporary solution* ya ku-*control* uchakachuaji wa mafuta, kwa hiyo, bei ya mafuta ya mafuta ya taa ifanane na bei ya *diesel*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *EWURA* sasa hivi inatumia mbinu za kisasa na teknolojia za kisasa, lakini bado eti tunaacha bei ya mafuta ya taa iwe sawa na ya *diesel* kwa ajili ya ku-*control* uchakachuaji. Kwa nini tumtese Mtanzania asiyekuwa na gari kwa sababu ya kulinda maslahi ya wenye magari? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya kwanza. Naomba dakika tatu basi nimalizie hujuma ya Kusini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haiwezekani Mheshimiwa.

Tunaendelea na Mheshimiwa Rehema Migilla, atafuatiwa na Mheshimiwa Lwakatare. Kama watamaliza mapema kabla ya muda wao, Mheshimiwa Prof. Norman Sigalla.

**MHE. REHEMA JUMA MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia kidogo katika hotuba ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia vitabu hivi na kuvisoma kwa umakini sana, kimaandishi vitabu hivi vina maelezo mazuri sana, lakini kwenye utekelezaji napata ukakasi. Kiukweli bajeti ya mwaka huu haiakisi maisha halisi ya Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kutokana na sababu kwamba leo hii ukiangalia maisha ya kila Mtanzania ni magumu sana. Bado kuna Watanzania wanakula mlo mmoja kwa siku, lakini sokoni mfumuko wa bei ni mkubwa sana, vitu vinauzwa kwa bei kubwa sana. Sambamba na hilo, hata mzunguko wa pesa huko mitaani haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii wafanyakazi wanalia, hawana pesa; wakulima wanalia, hawana pesa;

wafanyabiashara wanalia hawana pesa, halafu tunasema ni bajeti nzuri, huu ni uwongo. Bado katika vitabu hivi tunasema kwamba, eti bajeti hii ina lengo la kuondoa umaskini na kupeleka nchi kwenye nchi ya viwanda ilhali hatuyapi kipaumbele maeneo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na matatizo hayo ambayo yanaikumba hii bajeti yetu, naomba Serikali sasa ifanye yafuatayo ili kuhakikisha maisha ya Mtanzania ambayo tunalenga yamwondolee umasikini yanafanyiwa kazi. Kwanza Serikali idhibiti mfumuko wa bei, bei ni kubwa sana, lakini pia kupunguza riba kwenye mikopo. Suala lingine kuwepo basi na nidhamu kwenye matumizi ya mapato yetu. Leo hii tunachokipanga siyo ambacho tunakitekeleza. Bajeti ya mwaka 2017 haijatekelezeka kwa asilimia zinazotakiwa, halafu leo tunaleta bajeti nyingine ambayo ni kubwa zaidi kuliko ya mwaka 2017. Naomba haya masuala yafuatiliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuongelea leo ni kutoongezwa kwa mishahara kwa wafanyakazi na kulipa madeni ya wafanyakazi. Suala la kuongezewa mishahara kwa hawa wafanyakazi siyo suala la mtu kupenda, ni la kisheria. *Annual increment* iko kisheria, lakini leo hii uongezaji wa mishahara kwa wafanyakazi imekuwa mpaka mtu apende. Jamani kwa nini tunakwenda kinyume na utaratibu wa sheria inavyotaka? Tunataka sasa pindi anapo-*wind up* atuambie hii sheria ambayo iliruhusu *annual increment* iwepo na mliitunga humu Bungeni inafanyiwa kazi kwa kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ulipaji wa madeni. Wafanyakazi wa Tanzania *especially* walimu, wana madeni mengi sana. Wana madeni ya *arreas,* likizo, tofauti na mshahara, lakini madeni haya hayalipiki kwa kigezo cha uhakiki. Hivi ni uhakiki gani ambao hauna kikomo? Serikali inatumia upenyo wa uhakiki kutowalipa watu stahiki zao. Tunaomba huu uhakiki uwe na kikomo, watu walipwe stahiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ajira kwa vijana. Naipongeza Serikali kwa kutoa riba kwenye hii 10% ya maendeleo ya vijana na wanawake. Hata hivyo, kutoa riba haimaanishi kwamba ndiyo hawa vijana watakuwa wamekomboka kwenye suala la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo, nikiwa na sababu kwamba Halmashauri zetu tumezinyang'anya vyanzo vikubwa vya mapato kiasi kwamba mapato yanayobakia yanakuwa ni madogo hali inayosababisha ile *10%* iwe ndogo. Wanapoenda kwenye vile vikundi vyao wanapatiwa hela ndogo sana kiasi kwamba watu wanaamua kuacha pesa ile. Kwa hiyo, naomba sasa Halmashauri zirejeshewe vile vyanzo vyao vya mapato ili watu waweze kusaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine tujikite katika maeneo ya kipaumbele. Malengo ya bajeti hii yanalenga kuifikisha Tanzania katika uchumi wa viwanda, lakini tunaufikishaje uchumi wa viwanda ilhali maeneo ya kipaumbele kama kwenye kilimo, afya, elimu, tunayapelekea bajeti ndogo mno ambayo haitekelezeki? Naomba kilimo lipewe kipaumbele kwa sababu kwanza kinaajiri Watanzania walio wengi lakini pia kipelekewe pesa kwa wakati ili wakulima waweze kuwa na tija na kilimo chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni *TRA. TRA* na wenyewe ni *another disaster. TRA* tunaamini ndiyo chombo chetu cha kutukusanyia mapato lakini wamekuwa ni mwiba kwa wafanyabiashara na kwa kila kitu. Leo *TRA* anakwenda kukagua na wanatembea na makufuli muda wote. Sasa kama wanatembea na makufuli muda wote, wafanyabiashara wataogopa kufanya biashara na wakiogopa, watafunga biashara zao. Wakifunga biashara hatuwezi kupata mapato ambayo tunayatarajia. *TRA* wanatembea mpaka kwenye ma-*guest* usiku, kweli! Mtawatisha hadi wawekezaji, tuiangalie *TRA. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwenye kuboresha viwanda vyetu. Tuko kwenye nchi ya viwanda na tunaelekea kwenye Serikali ya viwanda. Viwanda tunavyo

vingi sana lakini mpaka dakika hii havifanyi kazi, vimekufa. Tunaiomba Serikali yetu, kabla ya kuanzisha viwanda vingine iviboreshe vile vilivyopo na kama kuna wawekezaji ambao wanashindwa kuviendesha basi wapewe wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kodi ndogo ndogo ambazo ni kero kwa wawekezaji zipunguzwe. Mfano Mkoa wa Tabora kuna Kiwanda cha Nyuzi, kipo siku nyingi sana, kilikuwa kinatoa ajira kwa wakazi wengi sana wa Tabora. Kiwanda kile kimekufa na walipewa Wahindi na bado kuna wananchi wa Tabora wanadai pesa ambazo zilizotokana na kiwanda hiki. Kama kweli, tunataka tuboreshe ajira na tufikie uchumi wa viwanda, basi hivi vilivyopo kwanza vihakikishwe vinaboreshwa na hao wawekezaji wanapunguziwa adha ndogo ndogo ili waweze kuwekeza kwa umakini sana. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehema kuna taarifa huku. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa heshima na taadhima, naomba nimpe taarifa rafiki yangu Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ambavyo vimekufa havifanyi kazi vilikuwa 56 Mei, 2017. Viwanda 18 nimelieleza Bunge vimeshaanza kufanya kazi, viwanda 35 Serikali imevichukua vitafanya kazi nyingine lakini kasi ya kuanzisha viwanda ni zaidi ya 56. Tuna viwanda 3,306 kwa kipindi cha miaka miwili. Tanzania nzima ina viwanda 54,000, hatuwezi kubaki na viwanda hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namsihi Mheshimiwa Mbunge tusibaki na viwanda hivi vilivyokufa, tuanzishe

viwanda vipya. Tulikuwa hatuna viwanda vya marumaru Tanzania, leo tuna viwanda vya marumaru tuna-*supply* Afrika nzima. Sasa tubaki tusiwe na viwanda tutakuwa mgeni wa nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaanzisha viwanda vya sukari, tusibaki na hivi viwili tuanzishe viwanda vya sukari. Namsihi Mheshimiwa Mbunge akubaliane nami, nampa taarifa. *(Makofi)*

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba atajibu muda wake ukifika. Naomba niendelee. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehema unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei. Naomba niendelee, nilindie muda wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mheshimiwa Waziri hawezi kutuambia kwamba eti tuanzishe viwanda vingine ilhali kuna vingine ambavyo vimekufa. Kwa nini tusifufue hivi kwanza? Leo uanze mradi mwingine wakati wa kwanza haujaukamilisha, ndiyo maana tuna-*fail* katika mambo yetu mengi kwa sababu ya kuanzisha miradi ambayo haitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. Suala lingine ni elimu bure. Elimu bure ina faida nyingi sana lakini hatukujiandaa. Tumeanzisha elimu bure ilhali hatujaandaa miundombinu ya kuhakikisha tunaenda sambamba na hii elimu bure. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Muda wako umekwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa wale ambao hawanifahamu vizuri, niliwahi kuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ndani ya Bunge hili. Nikiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, nilipata bahati kwa miaka mitano kusimamia bajeti mbadala ya Kambi lakini pia kuzisikiliza bajeti mbalimbali zilizokuwa zinawasilishwa na Mawaziri wa Fedha na Mipango. Sikuwahi kusikia Waheshimiwa Wabunge na hasa wa upande wa Chama Tawala kwamba kuna Kambi ambayo haikupewa mashadidio kushadidiwa maana siku zote wamekuwa wakisema hii bajeti ni kiboko, haijawahi kutokea, ni funga kazi, ni mwarobaini wa matatizo mpaka bajeti ya mwaka huu wanasema haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtu kama mimi mzoefu ambaye niliwahi kuwa ndani ya Bunge hili, ni kati ya ma-*veteran* wachache ambao nilichukua likizo kidogo kwenda kuchungulia wananchi wanaendeleaje halafu nikarudi, maneno haya huwa nayasikiliza kama swaga. Kwa hiyo, hayanipi matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea maneno ya Mheshimiwa Spika juzi juzi hapa wakati hotuba iliposomwa, Mheshimiwa Spika, akasema angetaka maelezo fasaha kutoka kwa Mheshimiwa Mpango kwamba kwa nini bajeti ya Kenya pamoja na idadi ndogo ya watu inakuwa karibu mara mbili ya bajeti yetu? Ni bajeti ambayo uki-*combine* ya Uganda, Tanzania na Rwanda na vichokochoko vingine, ndio bajeti ya Kenya?

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ni mepesi. Tatizo letu sisi tunafanya *business as usual.* Halafu naingiwa na wasiwasi, kwa *capacity* ya watu wetu; *capacity* ya wataalam, Mawaziri wetu, watu wanaomshauri Mheshimiwa Rais na siyo kwa awamu hii ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli, ni awamu zote tangu siku za nyuma. Ukiangalia bajeti za miaka ya nyuma, bajeti imekuwa inapanda lakini matatizo kwa nini ni yale

yale? Huwa nafika mahali najiuliza, hawa wataalam wetu wanasoma shule gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimewahi kusoma mahali, kuna Profesa mmoja wa nchi ya Norway; nitakapokumbuka *citation* nitaitafuta, anasema vijana na wasomi wa Kitanzania wanajua sana kukariri vitu ambavyo *sometimes* siyo lazima wavi-*apply,* kwa hiyo, ni watu ambao wamebobea kwenye *theory.* Nilipokuwa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, kulikuwa na mwanafunzi mmoja, ukienda *library* utakuta amepanga vitabu vinamzidi hata urefu, vingi tu, lakini ukija mtihani akijitahidi sana anaambulia karai. Yule bwana alikuwa anasifika, halafu anabeba vitabu kweli kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa mahali ninakokaa, nikajaribu kupanga vitabu ambavyo nimepewa hapa Bungeni, yaani mimi ni mrefu, sasa hivi vimenifika kwenye bega. Watanzania tunajua kuandika, mipango iko kwenye makaratasi, lakini unapokuja kwenye ku-*practise* pale ndipo tunatofautiana na wenzetu wa Kenya. Hapa tunazungumza mno vitu ambavyo vingine hata yule anayevisema haviamini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa nasikiliza sana, japo huwa sina bahati ya kupata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza na huenda nitahama hapa ninapokaa. Huwa nasikiliza linapigwa swali pale unakuja kusikiliza majibu; samahani, kwa mtu kama mimi naona hili jibu ni bora twende, kwamba leo lipite tukutane kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huo, kwa staili hii tunayokwenda nayo, mfumo huu tunaokwenda nao wa kibajeti, kwa sababu ni mfumo ambao unaweza ukau-*refer* kuanzia miaka ya nyuma, wala siyo awamu hii tu, tunakuwa na bajeti ambazo hazitekelezeki. Tunakuwa na maneno ambayo ni matamu kuyasikiliza, lakini unapokuja kwenye *practise* hayapo, huwezi ukayapata yote kiasi kwamba nasema hata Mheshimiwa Dkt. Mpango tungekuwa na uwezo wa kumpitishia bajeti ya shilingi trilioni 200, haki ya

Mungu kwa utaratibu na mfumo huu, nchi hii hatubadiliki, hatutoki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kenya mtu kuja kuwa Waziri, anachujwa na vitu vingi mno. Kwanza *capacity* yake yeye mwenyewe, yeye vipi? Mambo aliyonayo kichwani, je, anayaamini? Je, anaweza akayaweka katika vitendo na utekelezaji? Ndipo unampata mtu kweli anayeweza kusimama na maneno ambayo anayazungumza humu. Wengi hapa huwa wakijibu maswali, wakitoa mipango mbalimbali, wakisoma matamko unamwona kabisa huyu mtu ni mwongo yaani unamsoma kabisa ni mwongo yaani hata kile anachokizungumza hakiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba tubadilike, tuanzie hapo, tubadilike. Tuwe na mapinduzi ya kifikra na mapinduzi ya Bunge jipya ambalo linakwenda na hiyo *three line whip* kwamba ni dhamira ya mtu mwenyewe na ndiyo *capacity* yake na mitizamo yake na mtazamo wa Chama chake na Taifa lake. Hapa *over 95%* unakuta ni dhamira ya kichama, *that is a major problem,* kiasi kwamba mtu anaweza akawa na nondo zake, ni Profesa, *Doctor,* ana *Masters,* lakini unamwona kabisa kwa sababu ya dhamira moja kubeba *95%* inamsababishia azungumze kitu ambacho hata yeye hakiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumza na wananchi wangu wa Bukoba. Kule *Bukoba Town* tuna ile mialo ya Bakoba, Kahororo na *Custom,* watu wamezoea miaka yote tangu nizaliwe wanakwenda kuvua samaki kwa kutumia ndoano. Kuna kijana mmoja akanipigia simu jana, akasema Mheshimiwa Lwakatare, hebu tuambie nikiweka ndoana kule niweke na bango kwamba kama huna sentimita 25 usiguse? Nimekosa jibu la kumjibu. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo tunalolipata, tunapotunga sheria, kwanza naamini sheria nyingi tuna-*copy*

na ku-*paste,* ni matakwa ya Wazungu. Kwa sababu, Wazungu kwenye viwanda vyao wanataka samaki awe na sentimita 25 au sentimita ngapi, tukija hapa hatutumii hata *loophole* ya nguvu tulizopewa za kanuni. Naamini kama Mheshimiwa Waziri anaona sheria ni ya jumla sana na haitekelezeki katika mazingira yetu, basi atumie *loophole* ya Kanuni aweke na vigezo ambavyo vinaendana na maisha yetu ya kila siku na maisha ya watu wetu, lakini tukienda tu, yaani ni gari linakwenda lakini halijui kwamba kuna *reverse* na kona, haki ya Mungu wataumia wengi. Huu mtindo wa mzigo ufike, punda asife, tuache kuutumia tunawaumiza watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Marehemu Mwalimu Nyerere, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi, aliwahi kusema kwamba mtu akikuletea vichupa vilivyosagwa vinang'aa akakwambia kwamba hii ni almasi na anataka uamini kuwa ni almasi, wewe utakuwa ni zuzu yaani ukikubali anaokuona wewe ni zuzu. Mimi huwa ni mtu wa mwisho kutoamini kitu ambacho unaona kabisa dhahiri hakipo. *(Makofi)*

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo, Mheshimiwa.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mpango weka vitu ambavyo vinatekelezeka kwa elimu yako uliyonayo, usisikilize watu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Imebidi nicheke kidogo, huu mchango wa mwisho hapa wa Mheshimiwa *veteran* wetu humu ndani nimepata picha ya namna ambavyo unaboresha hii bajeti iliyo mbele yetu hapa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mpango naamini umepata mawazo mazuri kabisa ya Mheshimiwa Lwakatare ili uboreshe bajeti yako hapa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi. Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, mlishatajiwa majina, tunaanza na Mheshimiwa Prof. Norman Sigalla na Mheshimiwa Kubenea ajiandae.

**MHE. PROF. NORMAN A.S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa na nzuri inayofanywa chini ya uongozi wa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ya kuimarisha miundombinu na kutengeneza mazingira sahihi ya uwekezaji Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya eneo zuri sana ambalo Mheshimiwa Rais amefanya ni kuimarisha Benki ya Uwekezaji (*TIB)* na matawi yake ambapo sasa Mtanzania anayetaka kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji kinachohitaji mitaji mikubwa, benki zetu sasa zinaweza kufanya; ukitaka kuwekeza kwenye viwanda benki zetu sasa zinaweza kufanya; na uchimbaji wa mabwawa benki zetu sasa zinaweza kufanya. Kwa hiyo, naomba sana Watanzania kwa ujumla wao wale wanaopenda kuwekeza watembelee benki zetu za *TIB* ili waweze kutumia fursa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ni salamu za wananchi wa Makete. Wanampongeza Rais hasa kwa kutenga vijiji 51 katika ya 67 vilivyoko Makete ili waweze kupata umeme ambao utafasili uanzishwaji wa viwanda na matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili naomba nisisitize jambo moja. Wilaya kama Makete ambazo tunafahamu mchango wake kwenye nchi yetu ya Tanzania na hasa upande wa maji yanayozalisha umeme ikiwemo bwawa tarajiwa na mradi mzima wa *Stigler's Gorge,* Makete ndiyo *hub,* ndiyo *catchment* mama ya mito hiyo ya Ruaha Mkuu ambao baadaye unabadilika majina unaitwa Kilombero na baadaye kuitwa Rufuji. Naomba sana Serikali ipeleke maendeleo ili kuwazuia wananchi wa Makete wasije wakaingia kwenye jaribu la kuharibu vyanzo vya mito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapelekaje maendeleo? Kwa mfano, badala ya kupeleka umeme katika vijiji 51 ilikuwa ni kumaliza vijiji vyote 67 vilivyoko Makete ili wasikate miti, wasiharibu vyanzo vya mito ambapo kama wasipoharibu tunajihakikishia kwamba miradi tunayoifikiria na kuitekeleza kama *Stiegler's Gorge,* Bwawa la Mtera, Kihansi pamoja na Kidatu watapata maji kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, namwomba sana hasa rafiki yangu Mheshimiwa Waziri, sera zetu za uwekezaji zisikilizane na vitendo vyetu. Mipango yetu na nyimbo zetu za uwekezaji zisipingane na vitendo vyetu. Kwa mfano, sote tunafahamu kwamba maduka ya kubadilishia fedha kwa maana ya *Bureau De Change* tulianza na mtaji wa shilingi milioni 20 tukapanda kwenda shilingi milioni 40, shilingi milioni 80, shilingi milioni 100, lakini sasa nafahamu mtaji wa kuanzisha duka la kubadilisha fedha ni shilingi milioni 300. Tunataka watu wawekeze kwenye maduka ya kubadilisha fedha au wafunge maduka? Kwa vyovyote vile siyo dhana sahihi hata kidogo. Unapomtaka Mtanzania wa kawaida awe na duka la kubadilisha fedha lakini mtaji wake unasema shilingi milioni 300 siyo sawa. Ushauri wangu kwenye hili, mtaji wa kuanzisha maduka haya uwe kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Serikali ifahamu, ufa uliokuwepo kwenye maduka ya kubadilishia fedha ilikuwa ni mamlaka za Serikali kutokufuatilia kama hawa wabadilishaji wa fedha wanatoa risiti. Kwa sababu hakukuwa na risiti ambazo ziko *centralized* kwamba mtu

nikibadilisha dola 100,000, *BoT* au Hazina wanajuaje kwamba *Bureau A* amebadilisha fedha? Kwenye nchi nyingine ukishabadilisha, aki-*punch* tu, Hazina wanajua kwamba *Bureau* ya Norman ameshabadilisha fedha. Tujitahidi huko ili kupata kodi stahiki, siyo kubana. Tutafunga watu wengi na tukifunga maduka haya mengi, maana yake tutapoteza ajira nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo sasa, niiongeze tu hapo hili la kuhusu mitaji. Leo mtu anaulizwa umepata wapi shilingi milioni 300 za kufungua *Bureau De Change? I keep on asking myself,* hili swali linaisaidia Serikali kupata mapato? Sielewi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, juzi tarehe 4 Mei, 2018 nilikwenda kwenye Mkutano wa Uwekezaji pale Dubai. Niliyeambatana naye alikuwa ni rafiki yangu mfanyabiashara wa nchi jirani, alikuwa na *cash money* dola 400,000. Alipofika Dubai alipoambiwa a-*declare* akasema 400,000 *USD.* Pale pale wakampa *pass ya VIP* na kumwambia *Sir, do you want us to facilitate your protection while in Dubai?* Unataka tukulinde ukiwa hapa? Akasema hapana, *I am comfortable.* Je, unapenda tujue hoteli unayofikia? Akasema ndiyo, akataja hoteli yake. Akapewa heshima tofauti na Norman Sigalla King aliyekuwa na Dola 350 za kulipa tu hoteli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nini maana yake? Maana yake ni kwamba mwekezaji anapoleta fedha, *it is immaterial* kuhoji ametoa wapi? Ametumiaje ni sahihi kuuliza. Ndiyo maana kwenye mchango wangu mwingine nimesema, mtu kama anataka kuangusha Serikali yetu, huyo mfuatilieni. Dunia ya leo unaweza uka-*track* matumizi ya fedha bila kunihoji kabisa. *I will feel comfortable* kwamba *this is the correct avenue* ya ku-*invest.* Nitasema hapa ndiyo mahali pa kuwekeza, kwa nini? Siwi *disturbed,* sisumbuliwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana tufuatilie matumizi ya fedha wanazoingia nazo watu. Kwa vyovyote vile fedha ni jambo la msingi zikiingia kwenye nchi yetu isipokuwa matumizi yake ndiyo yanaeleza ushetani wa

fedha. Sisi Wachungaji Makanisani huwa tunapokea kila sadaka bila kuuliza inakotoka kwa sababu ni matumizi ya hela ndiyo yanayoeleza uovu wa mwenye hela na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili la haraka haraka ni sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo ndiyo uti wa mgongo kwa Watanzania. Kwenye bajeti ya rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango anaeleza wazi kwamba asilimia 66 ya Watanzania wanategemea kilimo. Ombi langu, moja, tuanzishe kiwanda cha kutengeneza mbolea ambayo itakuwa *branded* kutoka kwenye uzalishaji kwamba *this is not for export,* ni kwa ajili ya wakulima wa Tanzania na mfuko wake ni Sh.20,000 kwa yeyote anayetaka, bila kuweka *categories.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, *NFRA* kwa jinsi ilivyoanzishwa, bahati nzuri ni *part* ya andiko langu ndiyo lililoanzisha *NFRA.* Anayependa asome kitabu changu kinachosema 'Maendeleo ni Vita, tufanyeje'. Tulichopendekeza ni kwamba *NFRA* ipewe fedha nyingi za kutosha ili i-*act* kama *backup* ya wakulima wanapokuwa wamelima mahindi, wawe na *assurance* ya *price*, wajue bei yake kwamba naenda kukopa benki kwa sababu najua kilo moja ya mahindi ni shilingi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kwa Serikali, afadhali Serikali ipoteze shilingi bilioni 30 au shilingi bilioni 40 kwa kuwagawia wakulima waliolima kiukweli kuliko vinginevyo. Naiomba sana Serikali, fedha za kununulia mazao kama ya mahindi zipelekwe kwa wingi na tulazimishe wafanyabiashara wote kununua *NFRA* au kama hiyo Tume ya Mazao au *whatever* wanunue huko, lakini kwa mkulima tu-*ensure price* yake kwamba *the minimum price you will get is this much,* kwa hiyo, tupeleke fedha kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa haraka kwenye huduma za afya. Sasa hivi tunajikita kwenye kupeleka madawa, naomba sana Serikali ibadili sura. Sasa tupeleke elimu kwenye kula vyakula bora. Mwezi uliopita tumekwenda

Korea, tulikuwa tunakohoa tukauliza kwa mtu mwenye miaka 74 kama anaweza kutuonyesha kituo cha afya kiko wapi, anasema hafahamu kituo cha afya popote. Tukamwuliza, kwa nini? Akasema sijawahi kuugua, kwa hiyo, hajui lakini siri ni aina ya vyakula anavyokula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu, leo hii tunagombania sukari, tunaongelea habari ya mafuta, nchi za wenzetu, mafuta yanayoitwa sijui mawese na mafuta yoyote ya kupikia kwao zilipendwa. Hakuna wanaotumia mafuta hayo sasa, yanarushwa kwetu nchi changa. Kwa nini? Kwa sababu wanajua kuwa ni madhara kwenye afya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe na jambo la pili kutoka mwisho kuhusu umuhimu wa kutekeleza Mradi wa *Stiegler's,* chonde chonde, naiomba Serikali yangu ya CCM, mradi wa Mchuchuma na Liganga upewe kipaumbele. Nilisema wakati...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Malizia.

**MHE. PROF. NORMAN A.S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema wakati fulani hapa kwamba ndiyo mradi pekee ambao Tanzania ina hakika kwamba utalipa fedha tulizowekeza.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nianze tu na alipoishia Profesa, ndugu yangu kwamba mimi nashangaa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna, jiandae.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa na sielewi kama Taifa tunataka nini? Tunataka ujamaa au ubebepari? Tunataka umeme wa maji au wa makaa ya mawe? Yaani nashangaa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina taarifa hapa ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa ya tarehe 3 Juni, 2016 anasema kwamba Serikali inawekeza katika Mradi wa Mchuchuma na Liganga ambao utazalisha *megawatt* za umeme na kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Mradi huu navyofahamu ulikuwepo miaka mingi sana lakini haujatekelezwa na ulikuwa ndiyo ukombozi wa nchi hii katika umeme na ndiyo tulivyokuwa tunaambiwa hapa. Sasa tunakwenda katika umeme wa maji ambao tuna Mabwawa ya Nyumba ya Mungu, Kihansi, Mtera, Hale na Pangani na yote haya yanazalisha chini ya kiwango chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka nchi hii inapatwa na ukame, hatuna uhakika huo umeme wa maji tunaoenda kuzalisha kama utaweza kumudu tabianchi. Umeme wa makaa ya mawe na chuma cha Liganga una uhakikika kwamba hauwezi kuadhiriwa na tabianchi. Kuna umeme wa upepo wa Singida tumeshindwa kuuendeleza. Mradi wa Umeme wa Singida Benki ya *EXIM* ya China, Mheshimiwa Waziri anajua, ilishakubali kutoa mkopo kupitia *NDC* ili umeme ule uweze kuendelezwa, umeshindwa kuendelezwa. Sasa unashangaa kwa nini tunachukua vitu nusu nusu? Leo tunaanzisha hiki, hatufikishi mbali tunakiua; kesho tunaibuka na kitu kingine. Fedha za Watanzania zinazama kwenye miradi ambayo siyo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi watu wamezungumza hapa juu ya Kiwanda cha Urafiki ambacho kilikuwa ni mali ya Watanzania kwa asilimia 100. Wamekichukua kiwanda, wakakiuza kwa mwekezaji, mwekezaji akawa hana mtaji, wakamkopesha fedha za Serikali, Serikali ya Tanzania ikamdhamini kwenye benki za

nje, akaenda kukopa na fedha hakurudisha na hisa anazo yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili, Mzee Alhaj Ally Hassan Mwinyi aliwahi kuita timu yetu ya Taifa Kichwa cha Mwendawazimu kwamba kila mtu anajifundisha kunyoa. *Sasa mimi naiona hii Serikali yetu inafanana na kichwa cha mwendawazimu, kwamba kila mtu kila siku, kwamba huyu anakuja kujifundisha hapa, huyu anakuja kuchukua hapa, kila siku.* [**Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**]

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea, subiri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, Kanuni ya 64(1)(g). Kanuni hii inatufundisha na kutukumbusha Waheshimiwa Wabunge, tunapochangia michango yetu ndani ya Bunge ni lazima tutumie lugha za Kibunge ambazo hazidharau wala kudhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haipendezi kabisa katika masikio yetu Mbunge anaposimama ndani ya Bunge kuchangia anatumia neno zito la udhalilishaji la uendawazimu na kuifananisha Serikali hii ambayo imejipambanua katika mambo makubwa mengi ya kimsingi na yenye kuleta tija na maendeleo katika Taifa hili, Serikali hii inamlipa hata yeye mshahara na hata Wabunge wa Upinzani wameisifia, narudia kusema, hata Mheshimiwa Mch. Msigwa alithubutu kuisifia, halafu leo hapa ndani Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba Serikali hii ni sawa na kichwa cha mwendawazimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwa kweli Mheshimiwa Mbunge ajielekeze katika mchango kwa kutumia lugha za kibunge na afute kauli hiyo kwa sababu siyo kauli ya Kibunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kubenea, hiyo siyo kauli ya Kibunge, futa maneno hayo ya mwendawazimu.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza mimi nilikuwa namnukuu Mheshimiwa Rais wa Awamu Pili, nadhani Mheshimiwa Waziri alikuwa tu na mambo yake na Mheshimiwa Mch. Msigwa lakini nimefuta kauli hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli unashangaa kwamba jambo tunalianzisha, tumeanzisha umeme wa gesi, wamekuja hapa Maprofesa, Profesa Muhongo alitembea na agenda ya umeme wa gesi nchi nzima, ndiyo ilikuwa agenda. Leo tumeacha gesi, tunazungumza umeme wa maji. Umeme wa maji ulikuwepo wakati wa Mwalimu Nyerere yakajengwa hayo mabwawa makubwa, tukahama tukaenda kuanzisha umeme wa mashine za kukodi; Songas, *APTL*, Richmond, *DOWANS,* tumeona huko nako; yaani sijui tunaelekea wapi? Sijui Taifa hili wataalam wetu wanafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha, kaka yangu namheshimu sana, nimemsoma akiwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, amefanya kazi nzuri, naomba asimame kama Waziri wa Fedha, amshauri Mheshimiwa Rais vizuri. Rais wetu siyo mchumi na hakuna binadamu yeyote aliyekamilika mahali popote pale. Waziri amshauri Rais, awe kama Mawaziri wa Fedha waliopita. Alikuwepo Mheshimiwa Mgimwa, alikuwa Waziri wa Fedha anayejiamini alikataa mpaka kulipa hela za *Escrow, record* zipo. Mheshimiwa Waziri Mpango amshauri Rais, hivi kweli mnachukua fedha shilingi bilioni 211 za korosho za wananchi wa Mtwara hamzirudishi, mnarudisha shilingi

bilioni 10, mnakuja na Muswada leo wa kuzuia hizo fedha zisirudi tena Mtwara. Jamani, huu ni wizi wa fedha za wananchi. Hii ni dhuluma! Hawa ni wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama yangu Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti nilikuwa India wakati naumwa ni miongoni mwa watu wa kwanza waliokuja kuniangalia. Mama simamia hii kitu, itakuondoa Bungeni. Wananchi wa Mtwara hawatakuelewa. Hawakukuelewa kwenye gesi, hii ndiyo hawatakuelewa kabisa. Simama mama, fedha za wananchi hizi zinataka kuondoka, simama zitetee ili wananchi wa Mtwara, Kusini, Mafia na maeneo mengine wanaolima korosho wapate matunda ya zao lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, unakuta kodi kwenye ndizi zinazotengenezea pombe, matunda, mimi nilitegemea tuletewe fedha za makinikia zile shilingi trilioni 409, tuzione humu ili wananchi wetu waachane na hizi kodi na *TRA* iache kukimbizana na Wamachinga Kariakoo. Shilingi trilioni 409 ni fedha nyingi kweli ambazo zinatosha kuendesha nchi hii kwa zaidi ya miaka 10. Sasa badala yake hizo fedha hazipo, wimbo wa makinikia hatuusikii tena, tuachane na hivi vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema hivi, ukikuta Serikali inakimbizana na Wamachinga mtaani, haikusanyi kodi kwa wafanyabiashara wakubwa, ujue kuna tatizo. Sisi kodi zetu zote ni kwa wafanyabiashara ndogo ndogo; wauza vitumbua, bodaboda, Machinga, tuachane na vitu hivi, tuleteeni kodi za migodi, ondoeni misamaha ya mafuta kwenye migodi, tuleteeni vitu vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti nzima hii wanasema haitekelezeki, mimi sijui kama haitekelezeki, lakini Mheshimiwa Waziri anajua kwamba mapato yetu yanashuka mwezi hadi mwezi na kwenye mwezi Mei na Aprili mwaka huu, mapato yetu yalipungua na yalikuwepo mapendekezo ya kupunguza

fedha za maendeleo katika baadhi ya maeneo. Ni lazima Serikali itafute mpango madhubuti wa kuendesha uchumi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkiwa mnakwenda kulia, mnajiita wajamaa wakati Serikali haimiliki hata benki moja kwa asilimia 100, inamiliki asilimia 30 au asilimia 31 kwenye *NMB* na *NBC,* halafu Serikali inajiita ya ujamaa. Mtu mmoja anasimama anajiita mjamaa lakini ukimwangalia kwa nyuma ana shamba heka 150 halafu anasema ni mjamaa. Sasa sijui ni mjamaa au Kijiji cha Ujamaa, mimi sielewi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Taifa ni letu wote na likididimia, tunadidimia sote, hakuna atakayekuwa salama. Mheshimiwa Waziri analeta mapendekezo na amesema kwenye Muswada na analeta humu kwamba kutakuwa na akaunti moja ya kuhifadhi fedha. Mkipata Rais anayefanana na Sani Abacha tutakuja kulia huku. Ni lazima tuweke mipaka ya madaraka. Ninyi mlikuja na mapendekezo ya kupunguza madaraka ya Rais katika Katiba Mpya. Mapendekezo ya Katiba Pendekezwa ni kupunguza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, malizia.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema Mheshimiwa Waziri wa Fedha amshauri Rais vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Anna Gidarya, Mheshimiwa Oscar Mukasa na Mheshimiwa Maulid Abdallah Mtulia wajiandae.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika bajeti hii kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kunukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 8(1), inasema:-

*"(a) Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii.*

*(b) Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi; na*

*(c) Serikali itawajibika kwa wananchi."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii imeletwa na tunaisifia ni bajeti nzuri. Maandishi ni mazuri, matendo ni mabaya kuliko tunavyofikiria. Hata Biblia inasema, heri yule aliyejenga juu ya mwamba kuliko yule aliyejenga juu ya mchanga. Ndugu zangu Taifa linaenda kuangamia. Uchumi wa Taifa unaenda kuangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, simulizi hizi za kusema uchumi umepanda amepata wapi? Wizara ya Kilimo mwaka 2016/2017 mpaka Machi fedha zilizopelekwa ni shilingi bilioni 2,252 sawa na asilimia 2.22, asilimia 98 ya bajeti haikutekelezwa. Katika Wizara ya Mifugo, makadirio yalikuwa ni shilingi bilioni 4 lakini pesa iliyotolewa ni shilingi milioni 130 sawa na asilimia 3.25, asilimia 97, haikutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye maji, pesa zilizotengwa ni shilingi bilioni 913, iliyotolewa ni shilingi bilioni 230,997 sawa na asilimia 25, asilimia 75 haikutekelezwa. Hizi ni simulizi alizoandika Mheshimiwa Dkt. Mpango kwenye kitabu hiki. Kama hizi za huku nyuma zimeshindikana kutekelezwa lakini amekuja tena na 2017/2018 Mifugo na Uvuvi wametenga fedha ileile ya mwaka 2017 lakini pesa iliyotolewa mpaka sasa ni sifuri. Hizi ni simulizi, Watanzania wana hali mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Mheshimiwa Waziri hamshauri Rais wakasimamia hata kwenye zile ahadi 10 za

Mheshimiwa Rais? Mheshimiwa Rais wakati wa uchaguzi alitoa ahadi 10. Kwanza, alisema ataboresha mfumo wa kiutendaji Serikalini. Pili, ataboresha Huduma za Afya. Tatu, ataboresha maslahi ya wafanyakazi lakini wafanyakazi wameishia kutumbuliwa, wala hawajaongezewa hata senti tano kwenye mishahara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya nne alisema, anaboresha elimu na elimu bure. Elimu bure imekuwa ni majanga katika Taifa letu. Ahadi ya tano alisema ataboresha maji, maji yako wapi? Namuuliza Mheshimiwa Dkt. Mpango, bajeti ya maji iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya sita akasema ataboresha kilimo, uvuvi, mifugo na viwanda. Kilimo na Mifugo ndiyo hiyo ya sifuri sifuri. Mheshimiwa Dkt. Mpango ameleta simulizi isiyosahaulika ndani ya Bunge. Saba, Mheshimiwa Rais alisema kuwe na kipato kizuri cha kuongeza uchumi, uchumi uko wapi? Nane, akasema kuongeza fursa za ajira, ajira ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya tisa akasema, kupunguza tozo na kodi zisizo za lazima hasa kwa wafanyabiashara wadogo wadogo. Sasa tozo imekuwa ni mwiba, mshike mshike mtaani. Watu wanaingia wanakagua mpaka *draw* za watu. Umetusakizia mbwa mkali wa mapato, *TRA.* Leo hii mpaka mabeseni ya vitunguu yanakamatwa, ukiwa na nyanya tano, ushuru, ukiwa na nyanya 10 ushuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mpango, asifikiri tunamchukia, tunamwambia kwa sababu Bunge ndilo lenye dhamana ya wananchi. Vichwa vyote hivi unavyoviona, watu hawa wanajibika kwa Watanzania. Kwa nini Waziri mmoja tu aliangamize hili Taifa? Baba yangu yangu Mheshimiwa Waziri tulia, kaa, mshauri Mheshimiwa Rais, timizeni hizi ahadi. Hizi bajeti za kisekta zinaendana na ahadi za Mheshimiwa Rais, kwa nini hamtaki kumshauri? Mnasema viwanda, viwanda mtavipata wapi wakati kwenye kilimo

kuna sifuri, elimu ndiyo hakuna, kila siku tunalalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tozo za *TRA* ambazo zinatuletea shida, *TRA* wamekuwa kama wezi. Umetoka na *TV* yako nyumbani unapeleka kwa fundi, anakwambia nipe risiti. Mimi nimenunua *TV* tangu mwaka 2008, risiti najua iko wapi? Msituchonganishe, mnavunja mahusiano baina ya *TRA* na watu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za sikukuu, wanusanusa kwenye maduka ya watu wanataka nini? Saa 4.00 asubuhi anakwambia naomba ripoti, ripoti inatolewa pale mtu anapofunga mahesabu ya siku, hiyo ya saa 4.00 yeye anatoa wapi ripoti? Kwa hiyo, saa 4.00 anatoa ripoti, saa 7.00 akifunga duka akienda kula akirudi anatoa ripoti. Kwa nini hamjatengeneza utaratibu wa kuelimisha wafanyabiashara? Hii ni dhambi kubwa sana, itamtafuna Mheshimiwa Dkt. Mpango. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii *issue* ya Polisi, tunataka watuambie Polisi wamegeuka kuwa wakusanya ushuru wa nchi hii? Polisi wamejazana barabarani, kila mtu ana mashine, wameongeza idadi ya magari, kila siku magari matano, utakamata magari ya nani? Wanasababisha nchi hii kuangamia kwa sababu ya maarifa. Serikali haijakokotoa vyanzo vya mapato ambayo tunafikiri kwamba tutapata mapato wamekuja tu wana-*hang* halafu sasa wameelekeza kwa wale wanaofikiri wataleta hela, Polisi hawataweza kuinua uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *issue* ya *standard gauge*. Mradi huu hauwezi kutekelezeka. Kama tunataka kuingia kwenye ushindani wa soko, Kenya wanatengeneza *standard gauge* inayotumia mafuta sisi tunatengeneza inayotumia umeme kwa kutegemea umeme wa *Stiegler's Gorge.* Tutatoka humu Bungeni mpaka huo mradi utimie, wote tumekufa. Tukifika kule, tutakuta na Kenya nao wameshatuwahi hakuna tena habari ya *standard gauge*. Nani anayekuja kwenye gharama kubwa wakati kuna

*standard gauge* inayotumia mafuta yenye gharama nafuu? Hakuna *standard gauge* inayoweza kujengwa kwa ajili ya kubeba tu abiria. Kama huo ndiyo mpango wenu, tutakuwa tumefeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengine siyo lazima tuyaseme kwa sababu macho yanaona lakini inabidi tuyaseme. Kwa nini Serikali isije na vipaumbele vinne tu ambavyo vinaweza kutekelezeka kuliko kuja na mlolongo wa vipaumbele ambavyo havitekelezeki? Leo nchi hii inahema kwa ajili ya sigara na pombe. Kila mwaka kodi ya pombe na sigara inapandishwa, japo wameandika ni hatari kwa afya zetu. Hakuna vyanzo vingine vya mapato? Wameacha kuweka wasimamizi katika zile sekta tunazofikiri zinatuletea pesa, wamekuja na hizi hela ndogo ndogo za kuokoteza, hizi ni pesa za kuokoteza. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mheshimiwa Waziri akajipange, tunataka bajeti inayotekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mukasa, Mheshimiwa Abdallah Mtulia na Mheshimiwa Hawa Chakoma ajiandae.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, namshukuru Mungu lakini nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango, Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalam wake wote kwa kuandaa bajeti lakini kwa kufanya kazi nzuri. Kuna maeneo yenye upungufu, lakini natambua kuna kazi imefanyika vinginevyo Taifa lingekuwa limesisimama kabisa. Kwa hiyo, nawapongeza kwa kazi iliyofanyika lakini nitasema maeneo yale ambayo hayako vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, langu la kwanza mahsusi ni wigo wa walipa kodi, ndipo tatizo langu lilipo. Mwaka 2004, kama siyo 2005, Fernando de Soto's ambaye Waziri anamfahamu vizuri kuliko hata mimi, alishiriki kuandika MKURABITA, alisema zaidi ya asilimia 90 ya shughuli za kiuchumi kwenye nchi hii zinafanya kazi nje ya sheria na shughuli za kijasiriamali asilimia 98 zinafanya kazi nje ya sheria na mbili tu ndiyo ziko ndani ya sheria. Alisema pia mali zetu kama ardhi na vinginevyo, asilimia 11 pekee ndiyo ziko ndani ya mfumo, kwa hiyo, ndiyo zinalipa kodi. Kwa hiyo, tuna wigo mkubwa sana wa mali na shughuli za uchumi ambazo ziko nje ya sheria hazilipi kodi. Kwa wakati huo alithamanisha shughuli za kiuchumi na mali ambazo ziko nje ya uchumi na hazilipi kodi, ilikuwa ni karibu mara kumi zaidi ya pesa yote ya nje, *Direct Foreign Investment* inayoingia nchi hii toka tumepata uhuru mpaka mwaka huo. Unaona kwamba ni uchumi mkubwa sana uko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilileta hili kwa muktadha wa sasa, nakumbuka tarehe 25 Machi, kama sikosei, Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli akiwa Morogoro, moja ya kauli zake alikuwa anawakemea *TRA* kufanya kazi kwa kuwa-*harass* wafanyabiashara. Naamini kabisa na ni wazi hakuwa anazungumza hivyo kwa maana ya kwamba tusikusanye kodi, lakini ukitafsiri hiyo ni kutafuta namna gani watu walipe kodi lakini wigo uwe mpana, tutafute kupanua ili watu walipe kiwango ambacho kila mtu anakimudu na kwa sababu ni wengi, tutapata tija zaidi kwa maana ya kodi na hakutakuwa na haja ya kukimbizana. Hiyo ndiyo tafsiri rahisi kabisa ya alichokuwa anakisema Mheshimiwa Rais. Sasa nikawa nafikiri hebu tujikite kwenye kutanua wigo wa kodi, ndiyo moja ya matatizo makubwa yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mmoja umetokea juzi hapa, mimi nimetafakari sana hii habari ya kupima samaki kwa rula. Nikawa nafikiri hivi habari ya samaki, ni kweli tunahitaji kusimamia sheria kwamba samaki wavuliwe pale ambapo wana viwango lakini hii habari ya kutanua wigo wa kodi na kusimamia sheria kwenye sekta mbalimbali tunahitaji kuviweka kwenye muktadha sahihi wa kila sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, nafikiri njia rahisi ni kutafuta namna ya ku-*balance* kati ya ufugaji wa samaki ili isaidie, watu wasijikite zaidi kuvua kwenye maziwa na bahari, wavue huko wanakofuga. Hii itakuwa imetibu mambo mawili; amezuia kila mtu kwenda kule lakini ameanzisha ajira ambako tutapata kodi, watu familia zao maisha yatakwenda na tutapata kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata habari ya mifugo, tumepiga kelele sana watu wa Kanda ya Ziwa. Nilisema na ninasema tena. Mimi sio mmoja kati ya watu wanaotetea mifugo wakae hifadhini lakini ni mmoja wa watu ambao sielewi kuwaondoa tu hifadhini ili kukidhi sheria, lakini hatutumii hiyo fursa kubadilisha hii mifugo ikawa ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kuna habari hapa imesemwa ya kugonga wale ng'ombe mihuri, nafikiri Mheshimiwa Rais wakati anatoa agizo hilo alikuwa analenga ni namna gani tujipange. Siyo lazima tukae kwenye kugonga mihuri, kwanza tunaharibu ile ngozi, tunapunguza thamani. Teknolojia sasa hivi iko juu, tena hapa hapa Tanzania, ukienda Sokoine tu hapo, Chuo Kikuu cha Kilimo, ng'ombe anamezeshwa *chip,* anatembea na *chip* yake, ukikaa kwenye kompyuta unamwona, unawahesabu ng'ombe 8,000 wako Biharamulo, akifa au akichinjwa unaona taa imezimika, unampa Afisa Ugani wako namna ya kudhibiti wa kwake, unajua nani kachinjwa, nani hajachinjwa, ni rahisi. Hebu tutafute ubunifu ambao utadhibiti watu wasiwe na ng'ombe wengi, lakini umedhibiti na umeweza kurasimisha na kutengeneza ajira na wigo wa kodi. Tupanue wigo wa kodi Mheshimiwa Dkt. Mpango, tatizo langu liko hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye habari ya upangaji wa mipango yetu, haikai vizuri sana hapa, ingekaa kwenye Wizara ile ya Mipango, lakini ngoja niiseme ataona atakavyoiunganisha, ni habari ya sensa. Sensa yetu ndiyo inayotupa idadi ya watu ili kujipanga. Inafahamika duniani

na hata sisi tunafahamu na Waziri anafahamu sensa ina upungufu, tena hasa ya kwetu ambayo mara nyingi kuna watu wanakimbia kwa sababu tofauti tofauti, tunashindwa kupata idadi kamili. Sensa iliyopita inasema Dar es Salaam ni watu milioni tano, lakini kwa hesabu ya kawaida tu, hata ukikaa ukiangalia, pale siyo milioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, watu wa *NIDA* wanaoandikisha vitambulisho vya Taifa, ukiangalia idadi ya namba waliyoandikisha mpaka sasa Wilaya ya Temeke peke yake ambayo wanaanzia umri wa miaka 18 kwenda juu na tukikumbuka demografia inasema kwamba umri wa miaka 18 kwenda chini ndiyo watu wengi, ndiyo *base*, ukilinganisha idadi hiyo ya umri wa miaka 18 kwenda juu na idadi ya sensa inayosema kwa Temeke, ni vitu viwili tofauti. Tutafute tuwe na idadi sahihi ili tuweze kutekeleza mipango yetu na majibu yapo hapa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi, 2018 nilikwenda Mkoa wa Songwe kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa pale. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe ametengeneza Daftari la Wakazi la kielektroniki, mnaweza ku-*check* hata kesho, akikaa mezani anaweza akabonyeza *button* anakwambia leo wanafunzi ambao hawakwenda shule watoro ni wangapi, siku hiyo hiyo *real time.* Mkoa wa Songwe, nchi hii, siyo nchi nyingine. Hebu tutafute namna gani twende tujifunze pale, watu wa *NBS* wakae watazame...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia na Mheshimiwa Hawa Mchafu ajiandae.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata fursa hii adhimu na mimi kuchangia. Pili, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyofanya na tunakubali kibinadamu kwamba kuna yaliyopungua na ndiyo maana na sisi tumepata fursa hii ya kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika Jiji la Dar es Salaam na bahati njema nawe ni wa Dar es Salaam. Dar es Salaam ni kitovu au chemchem ya mabadiliko kwa Tanzania. Dar es Salaam ilitoa ushiriki mkubwa kabisa katika kuleta mageuzi na uhuru wa nchi. Mheshimiwa Mwalimu Nyerere alianza Dar es Salaam na wazee wake wa Pwani pale kupigania uhuru. Kwa hiyo, Dar es Salaam tuna kila sababu ya kuhakikisha unakuwa mji wa kisasa na chemchem ya uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ina mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu. Takwimu zinaonesha makusanyo ya kodi ya nchi yetu nusu yanatoka Dar es Salaam. Kama tutapanga mipango yetu mizuri zaidi, kuna uwezekano mkubwa kabisa Dar es Salaam ikaongeza mapato. Kama tunavyofahamu Dar es Salaam ina zaidi ya ya watu milioni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka nini sisi watu wa Dar es Salaam? Dar es Salaam tunataka Serikali ituwekee miundombinu ya kisasa ambayo itaweza kupunguza foleni. Uchumi wa Dar es Salaam unaweza ukaenda mara mbili zaidi endapo watu wa Tegeta, Mbondole na Pembamnazi wanaweza kufika Kariakoo kwa wakati na mtu wa Kongowe anaweza kufika Tegeta kwa wakati. Ili hili lifanyike, lazima Mheshimiwa Waziri aitazame Dar es Salaam kama *Special Zone*, kama sehemu ambayo uchumi wa nchi unaweza ukaimarika kupitia Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumza hivi kama Mbunge wa Kinondoni, niko katikati pale, lakini watu wanaokwenda Tegeta wanategemea barabara za kwangu pale Magomeni, Ndugumbi, Makumbusho, Kijitonyama,

Kinondoni yenyewe, Hananasifu, Kigogo lazima wapite. Tunapokuwa na miundombinu mibovu katika maeneo hayo ya kati, wewe shahidi, tunapokuwa na miundombinu mibovu Ilala mtu hawezi kufika pembezoni. Kama tunataka maendeleo ya kweli, basi lazima tujikite kuhakikisha tunaleta mabadiliko Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wangu wa Dar es Salaam siwezi kuwaombea pembejeo hapa kwa sababu kazi yao kubwa wamejikita katika sehemu ya kujiajiri wenyewe. Tunapozungumzia uchumi wa Dar es Salaam, tunazungumzia biashara. Lazima Mheshimiwa Waziri ahakikishe anatuwekea mazingira bora ya biashara. Zamani Jiji la Dar es Salaam tulikuwa tunapokea wageni kutoka Burundi, Rwanda, Congo wanakuja kununua bidhaa zao pale sasa hivi wale watu hawapatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napozungumza hivi naamini Mheshimiwa Waziri hili analitambua. Sasa tusiweke mazingira magumu mpaka ikapelekea wageni hawa wakaona ni bora kulichukua kontena kulipeleka kwao kuliko kuja pale Dar es Salaam. Kwa sababu wakija Dar es Salaam watu wa Ilala, Kinondoni na Temeke *guest* zao zitapata watu, uchumi unazunguka. Kwa hiyo, hili ni muhimu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine watu wetu wa Dar es Salaam wamejiingiza katika sekta ya habari, utamaduni, sanaa na michezo. Tunapozungumzia Wizara ya Michezo kwetu sisi inafanana na Wizara ya Kilimo kwa sababu asilimia 60 ya watu wa Dar es Salaam shughuli zao ni za kujiajiri wenyewe, sanaa, habari na michezo. Vijana wamefungua ma-*blog* mengi, wako kwenye *social media*, wanaigiza, wanaimba na wanacheza. Ukienda katika Wizara ya Michezo katika fungu la maendeleo, utakuta kuna shilingi bilioni 8, shilingi bilioni 3 kwa ajili ya *TBC*, shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya viwanja, sasa unakuta hawa vijana hatujawatengea kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati wenzetu wengine wanadai pembejeo kwa watu wao, sisi watu wa

Dar es Salaam tunataka vijana wetu watengenezewe *studio* waingie watoe muziki safi. Tunataka vijana wetu watengenezewe jumba kwa ajili ya kwenda ku-*act* na wapate hatimiliki ya kazi zao. Hizi ndiyo kazi ambazo nadhani watu wa Dar es Salaam tukifanyiwa uchumi wetu utakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu mafanikio ya bajeti yetu. Kuna watu wanazungumza hii ni bajeti hewa, bajeti ya kufikirika na kadhalika, lakini jamani tuwe wa kweli, bajeti hii ni nzuri na lazima tujue tulikotoka. Sisi wengine tunakumbuka tuliingia kwenye siasa kwa matatizo gani? Tuliingia kwenye siasa wakati huo barabara ya Kibiti – Lindi haipitiki, hakuna Daraja la Mkapa. Tuliingia kwenye siasa mtu akitaka kutoka Dodoma kwenda Arusha lazima afike Chalinze. Mtu akitaka kutoka Dodoma kwenda Mbeya lazima afike Morogoro. Kulikuwa hakuna Daraja la Kikwete wala Daraja la Ifakara. Tumetoka mbali sana jamani, lazima tuone tulikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeondoa riba kwa vijana. Mimi nikienda Misikitini kuwahamasisha watu wangu namna gani wataitumia Serikali, nikiwaambia mikopo, walikuwa wananiuliza sasa hii riba itakuwaje na sisi hatutaki kutumia riba? Leo Serikali imesikia imeondoa riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye miradi mikubwa, sisi watu wa Dar es Salaam ndiyo watumiaji wakubwa wa umeme. Hizi propaganda ya kuacha huu mradi wa *Stiegler's Gorge* zinatoka wapi? Watu wa Dar es Salaam tunatumia umeme zaidi ya nusu ya umeme wote unaozalishwa. Tunajua kuzalisha *megawatt* moja ya umeme wa gesi ni ghali kuliko umeme wa maji, dola milioni 1.2 na hii nyingine ni dola milioni 1. Hata uzalishaji wake, *megawatt* moja inauzwa kwa Sh.136 wakati ya maji ni Sh.36. *TANESCO* leo wananunua umeme kwa *unit* moja Sh.148 wanauza kwa Sh.200, tukitengeneza umeme wa maji…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, malizia.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bei itashuka na watu wa Dar es Salaam watanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chakoma, Mheshimiwa Shabiby, Mtera. Mheshimiwa Bwanausi na Mheshimiwa Musa Ntimizi ajiandae.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Dkt. Kijaji kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa hakika kwa Wizara hii kutupiwa lawama ni jambo la kawaida kwa sababu ni Wizara ngumu na hasa ukizingatia kwamba fedha tunazozipata hazitoshelezi kufanya kila jambo kwa wakati tunaohitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye suala la mapato. Naona bado kabisa tuna mianya ya ukusanyaji wa mapato. Nikianza na mfano mdogo tu, bahati nzuri niliwahi kuwa Dar es Salaam pale, suala la *Property Tax,* kiwango tunachokusanya hakifanani na hali halisi ambayo tungeweza kupata. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, akae vizuri na watu wa *TRA* ukusanyaji wa fedha hizi ni mdogo sana. Pia hata suala zima la kukadiria, suala la malipo ya hizi fedha za *Property Tax* haziko katika kiwango kinachostahili. Kwa hiyo, naomba sana kwamba suala la ukusanyaji mapato katika kila eneo ambalo linatakiwa zikusanye lifanywe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sasa hivi ukienda katika *petrol stations* zetu nyingi, kila *petrol station* karibu wiki nzima hii nikipita wanasema zile mashine zimeharibika. Kwa hiyo, kuna kila dalili kwamba katika miezi hii tutakosa

mapato mengi. Naomba tu nimshauri Mheshimiwa Waziri, hivi haiwezekani badala ya kufunga zile mashine wale wafanyabishara wakubwa wa mafuta wanaomiliki vile vituo wakatozwa kodi moja kwa moja kule wanakonunulia mafuta ya jumla badala ya kuweka hizi mashine ambazo kila wakati zitakuwa zinaonekana zimeharibika. Nadhani tuangalie mfumo bora utakaosaidia ili huyu mlipa kodi alipe vizuri na Serikali ipate kipato chake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nichangie kuhusiana na mapato ni suala la kilimo. Tunakwenda kuua zao la korosho ambalo lilikuwa linaipatia Serikali fedha nyingi sana. Nina mashaka sana inawezekana walioko Hazina pale kuanzia Katibu Mkuu na wengine ambao wana mamlaka hawaijui korosho vizuri. Ndiyo maana zile fedha zikija wanaona hakuna sababu ya kurudisha kule. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, fedha hizi zirejeshwe kwa wahusika wakulima ili ziweze kuzalisha tena. Kwa sababu fedha hizi kama hazitoki kwa ajili ya pembejeo, unategemea msimu ujao wakulima wale watazalishaje zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kule suala la kuanzisha vitalu vile vya kupata mbegu mpya. Wale wote walioandaa zile mbegu bora za korosho ambazo zimesambazwa hawajalipwa hata senti tano na walitumia fedha zao na wengine walikopa benki. Mimi nakubali kwamba ni kweli kuna baadhi yao inawezekana hawakuwa wakweli katika jambo hili lakini huo uhakiki ukishamalizika, basi wale ambao wanatakiwa kulipwa waweze kulipwa fedha zao, sasa uhakiki unafanyika lakini fedha hazirejeshwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamezungumza hapa kwamba zao hili linahitaji utafiti na zile fedha zilikuwa zinarudi kule zinakwenda kwenye utafiti. Kwa maana hiyo Chuo cha pale Naliendele kitakufa, hawawezi kufanya utafiti kwa sababu hawapati fedha ambazo walikuwa wanapata kutoka kwenye Bodi ya Korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kabisa kwamba kuna baadhi ya fedha zilikuwa zikirudi kule hazitumiki vizuri. Nashauri uhakiki ufanyike ili zile fedha zirudishwe ili ziweze kuleta tija katika zao hili la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilitaka nizungumzie ni juu ya viwanda. Bahati nzuri na Waziri wa Viwanda yupo, suala la kubangua korosho na kuweka thamani ya korosho ni jambo muhimu sana. Hili jambo tumelizungumza sana sioni *progress*, sioni kama kuna jambo la msingi linafanyika, tunawanufaisha wenzetu wa nchi za India ambako tunapeleka korosho ghafi, sisi tunategemea kuuza korosho ghafi. Viwanda vipo na ilitakiwa kwanza wale ambao wamechukua wavirejeshe Serikalini ili tupate wawekezaji watakaobangua korosho, lakini hivi sasa hakuna suala lolote la msingi ambalo linafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni juu ya ugatuaji wa madaraka kurejesha kwenye Serikali za Mitaa. Tanzania ilikuwa ni miongoni mwa nchi ambazo zimefanya vizuri sana katika Afrika katika suala zima la kushusha madaraka kwenye Serikali za Mitaa. Hivi sasa naona kila Wizara inataka kuchukua mamlaka zote zilizoko kwenye Serikali za Mitaa zirudi Wizarani kwao. Kwa hali hii, Serikali za Mitaa zinakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, enzi ya Mwalimu waliwahi kuzivunja Serikali za Mitaa lakini baadaye umuhimu wa Serikali ya Mitaa ulionekana na zilirejeshwa. Tusifike huko kuziua tena Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nilikuwa nashauri kwamba kama tunawaondoa Maafisa Ugani wote kule na wanarudi katika Wizara zao, lazima tutengeneze muundo mpya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, malizia.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutengeneze muundo mpya ambao utafanya Mabaraza ya Madiwani yafanye kazi, lakini kwa sasa katika utaratibu huu Mabaraza yale hayatafanya kazi vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Ntimizi, jiandae Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia mawazo yangu na ya Wana-Igalula katika mpango na bajeti ya Serikali ambayo imesomwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia uchumi wetu na kumshauri Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi hii unakwenda vema na mwisho wa siku maisha ya wananchi wetu yanakwenda sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya Mipango na Bajeti amezungumzia mambo mengi, lakini nataka nimpongeze ameondoa baadhi ya kodi na tozo ndogo ndogo ambazo zilikuwa kero kubwa kwa wananchi wetu huko vijijini. Naomba nipongeze kazi kubwa ambayo inafanyika, tulishauri katika bajeti zilizopita kwamba uchumi wa nchi yetu unachangiwa sana na ubora na utendaji kazi wa bandari yetu. Sasa tunaona bandari yetu inaboreshwa, ni moja ya sababu itakayosababisha uchumi wa nchi yetu uende sawasawa. Napongeza sana kwa kazi kubwa inayofanyika pale katika bandari yetu ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uanzishaji wa *blue print,* wafanyabiashara walikuwa wanalalamika taasisi nyingi za kutoza kodi lakini leo tunaenda kuzikusanya katika sehemu

moja. Jambo hili litawarahisishia wafanyabiashara wetu kufanya biashara katika maeneo yao mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia ununuzi wa ndege. Tunataka kuimarisha uchumi wetu, tunataka tukusanye fedha za kutosha katika eneo la utalii, ni lazima tufanye maamuzi mengine ambayo baadhi ya watu wanayaona ni matatizo lakini huko tunakokwenda yataleta manufaa makubwa sana kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi wakazi wa Mkoa wa Tabora ujenzi wa reli ya *standard gauge* ilikuwa ni kilio chetu kikubwa sana. Kwa sasa usafiri wa reli siyo madhubuti sana, lakini kwa ujenzi wa *standard gauge* tunaelekea kwenye usafiri wa uhakika sana kwa sisi wakazi wa Mkoa wa Tabora. Hata tumbaku yetu inaposafirishwa kutoka Tabora kwenda sokoni, inatumia barabara na gharama zake zinakuwa kubwa. Kwa hiyo, ujenzi wa *standard gauge* utatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitoe mawazo haraka haraka kwa sababu najua muda ni mdogo, nianze na nukuu ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 79. Wakati anafanya hitimisho alisema, kujenga uchumi wa viwanda utachochea ajira na ustawi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie sana hapa hasa kwa sisi tunaotoka vijijini, unapozungumzia uchumi wa viwanda na maisha ya wananchi wetu asilimia kubwa unazungumzia *raw material. Raw material* za viwanda hivi zinatokana na kilimo na asilimia 85 ya wananchi wetu wanategemea kilimo sasa kisipoboreshwa hata hili suala la kusema kwamba tunataka kukuza uchumi wa viwanda itakuwa ni tatizo. Viwanda vyetu vinategemea tumbaku, katani, mpunga na nyanya. Je, bajeti yetu inasema nini katika kuwawezesha hawa wananchi wetu kuweza kuendesha kilimo cha kisasa ambacho ni kilimo cha umwagiliaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bajeti tunayoimaliza sasa, kwa kweli katika eneo la umwagiliaji ni sawasawa na zero, hatujafanya kwa kiasi kikubwa sana. Naomba Mheshimiwa Waziri, tukitaka kuzungumzia uchumi wa viwanda tusiache suala la kusaidia kilimo cha kisasa hasa katika eneo hili la umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya sisi kuzalisha *raw material* tunatakiwa tusafirishe mazao yetu kwenda sokoni. Ni jambo la msingi sana kuiwezesha *TARURA. TARURA* inatengeneza barabara zetu za vijijini. Kama barabara za vijijini zitakuwa mbovu, usafirishaji wa mazao kutoka vijijini kuja kwenye soko pia ni tatizo, utaongeza gharama za *raw materials* hizo na mwisho wa siku itakuja ku-*affect* viwanda vyetu huko tunakokwenda. Tuiangalie *TARURA* na tuipatie fedha za kutosha ili iweze kutatua kero ya barabara zetu huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia uchumi wa viwanda, uchumi wa vidogo vidogo unaajiri kwa asilimia kubwa sana watu ambao wako katika maeneo yetu ya vijijini. Viwanda vidogo visipowezeshwa na hapa nataka nizunguzie *SIDO*, *SIDO* inatengeneza zana ambazo nyingi kati ya hizo zinatumika vijijini kwetu. Kama nilivyosema, viwanda vidogo vingi ndiyo vinatoa ajira ya kutosha. *SIDO* haijawekewa fedha za kutosha, naomba tuiangalie ili iweze kusaidia viwanda vidogo vidogo katika maeneo yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la umeme. Unapozungumzia uchumi wa nchi kama suala la umeme litakuwa ni tatizo, bado tutakuwa tunapiga *mark time*. Shida moja iliyopo pale ni bajeti tuliyoipitisha kupelekwa ili kutekeleza miradi iliyopo. Miradi mingi ya umeme vijijini kwetu kwa sasa inasuasua kwa sababu Wizara haijawezeshwa fedha za kutosha ili kutekeleza miradi hii. Hapa nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya lakini tuwawezeshe fedha ili waweze kutekeleza miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la maji. Unapozungumzia uchumi maji ni jambo la msingi sana. Mwaka jana tulitenga shilingi bilioni 673 walipelekewa shilingi bilioni 347 tu. Tuli-*survive* na ile Sh.50 tuliyoipitisha hapa ya tozo ya mafuta, Wabunge wengi walishauri tuongeze Sh.50, hebu naomba tukubali tuongeze ile Sh.50 ili tupate Sh.100 tukatatue tatizo la maji. Tunahitaji tutengeneze miradi mikubwa ya umwagiliaji, tujenge mabwawa ya maji na kulipa wakandarasi wanaofanya kazi kule. Tukiongeza ile Sh.50 nina hakika kabisa miradi mingi ya maji itatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sana kwamba tunapopitisha bajeti kupanga ni jambo moja na sisi tunatimiza wajibu wetu wa kushauri. Mambo mengi yanashindwa kutekelezeka kwa sababu bajeti tuliyoipanga na kuipitisha mara nyingi haiendi katika zile sekta husika.

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Fedha ijitahidi kupeleka fedha zile ambazo tumezipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Njalu Daudi, wajiandae Mheshimiwa Hasna Mwilima na Mheshimiwa Abdallah Bulembo.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba hii. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha pamoja na Watendaji wake, Katibu Mkuu pamoja na washirika wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tunalolizungumzia ni muhimu sana na Bunge kama Watanzania lazima tujue safari ya maendeleo inaenda polepole lakini hadi hapo

tulipofikia tuko pazuri sana. Leo tunazunguka katika nchi yetu kwa kutumia *taxi* kwa sababu ya uboreshaji na ukusanyaji mzuri wa mapato yetu. Niwapongeze watu wa *TRA* kwa kazi kubwa. Nimpongeze Kamishna wa *TRA* kwa jambo ambalo amelianzisha la kuzunguka na kukutana na walipa kodi wadogo wadogo, ni jambo ambalo tulikuwa hatujawahi kuliona. Leo walipa kodi wetu hawa wanapata elimu nzuri ya kuweza kulipa kodi na kuweza kukusanya mapato mengi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie tu jambo moja. Katika ukurasa wa 69 wa hotuba yake ameeleza mfumo mzuri kwamba fedha zote za Bodi za Mazao zitakusanywa na Mfuko Mkuu wa Serikali, ni jambo jema, atupe *commitment* itakayokuwa rafiki na *time* ya kilimo, kwa sababu jambo hili linaenda kwa muda. Wasiwasi mwingi kwa Wabunge ukisikiliza michango yao ni kwamba fedha hizi zikiingia kwenye kapu lile zitapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuhakikishie fedha hizi zitarudi kwa wakulima *on time* ili tusije tukaachana na muda kwa sababu ukiangalia kwenye pamba au tumbaku yote yanaenda na muda. Mheshimiwa na Wizara yake waangalie ni jinsi gani watakuwa wanarejesha kwenye Bodi husika kulingana na muda wa mahitaji ili tuondokane na hii tabia ya kulaumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba Mheshimiwa Waziri alizungumzia suala zima la kufuta Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mazao ya mifugo. Katika kupitia kitabu hiki na *Bill* itakayokuja kusomwa nimeona kipengele cha soya lakini Tanzania kama nchi cha muhimu ni kupunguza tozo kwenye alizeti, pamba, mahindi na karanga, ndiyo tutaongeza bei kwa wakulima wetu kwa sababu soya hapa nchini haizalishwi sanasana iko Malawi, iko sehemu ndogo sana kule Songea na inazalishwa kwa *percent* ndogo sana. Wafanyabiashara wadogo wadogo wanachukua mashudu ya alizeti na pamba. Utakapoiweka hivyo bei zetu zitaendelea kuwa nzuri lakini tutachochea uzalishaji mkubwa wa mazao

ambayo tunayatumia wenyewe. Naomba na hilo nalo Mheshimiwa Waziri alichukue na alifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekaa takribani miezi mitatu, tunaitegemea sana Wizara hii kutukusanyia fedha ili tuzipeleke kwenye maendeleo ya wananchi wetu. Kwa Mkoa wetu wa Simiyu tuna mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Viktoria kuja Mkoa wetu wa Simiyu ikiwepo Bariadi, Itilima, Meatu, Maswa na Busega kwa ujumla. Mheshimiwa Waziri ndiye mwenye jukumu kubwa la kuhakikisha anazungumza na wadau wetu, naomba afanye hivyo ili fedha zipatikane mradi ule uweze kufanya kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifumo ambayo wameipendekeza ni mizuri sana. Mifumo hii ikisimamiwa vizuri inaweza ikaleta tija na tukaondokana na malalamiko ya kila siku. Mifumo hii ya kielektroniki ambayo wanaileta iko vizuri, lakini ziko changamoto ambazo zinajitokeza kila kukicha, wakati mwingine *network* zinapotea zaidi ya siku mbili, tatu, kwa hiyo, unaweza ukakuta Serikali inapoteza mapato. Mkiweka misingi na mifumo mizuri inaweza ikatusaidia sana tukawa na jambo ambalo linaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila jambo tunalolianzisha tujaribu kulifanyia *analysis* za kutosha na tuwe na uvumilivu wa kukubali mambo ambayo yanaenda vizuri. Nashauri Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla waendelee kupokea michango mbalimbali ili kushughulikia changamoto zilizopo kwenye maeneo yetu mbalimbali. Lengo ni moja tumekubaliana lazima tuwe na mfumo rafiki utakaosaidia kuleta tija kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ushauri na naomba mliangalie. Tunazo halmashauri zaidi ya mia moja, tunakusanya kodi na kukopesha mikopo midogo midogo. Nashauri jambo hili kwa siku zijazo Waziri ajaribu kulitazama ili fedha hizi ziende kwenye kapu na taasisi moja ili kusudi vijana wetu wawe wanaenda kuzikopa na kufuatiliwa kwa utaratibu mzuri, kuliko hivi sasa fedha hizi zimekuwa nyingi

lakini ukiangalia marejesho yake hayana tija. Fedha hizi ni nyingi ikiwa zitakusanywa vizuri na kuwekwa kwenye kapu na taasisi moja ya kifedha, zinaweza kutoa mchango mkubwa sana na kuleta uchumi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo sasa mfano, Wilaya '*X*' Afisa Maendeleo akihama mkopo ule unafifia na kupotea/kufa lakini kama kuna taasisi ya fedha imekabidhiwa fedha hizi inaweza kujiendesha vizuri na tukawa na fedha nyingi. Pia kwa kufanya hivyo hizi kelele tunazopiga kila siku kwamba halmashauri hazitengi fedha zitaisha kwa sababu halmashauri husika kwa makusanyo itakayokusanya asilimia 10 itachukuliwa itapelekwa kwenye chombo ambacho kimepewa mamlaka na aliyepewa mamlaka haya lazima azikopeshe kwa vijana wetu ili kusudi tuweze kutengeneza uchumi mzuri lakini vilevile tuweze kuwajengea uwezo vijana wetu kwa ajili ya kujipatia kipato na kizazi kinachokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Jesca Kishoa wajiandae.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kuwasilisha bajeti yenye matumaini kwa Watanzania. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri kwa sababu mimi niko kwenye Kamati ya Bajeti kwa kusikiliza Wajumbe wa Kamati na kuweza kufanyia marekebisho mambo mbalimbali. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ukurasa wa mapendekezo ya bajeti, ukurasa wa 29 unaosema kwamba, kutoa kipaumbele kwa ukamilishaji wa miradi iliyoanzishwa

na wananchi. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, tulikuwa tupokee shilingi bilioni 251 kwa ajili ya miradi ya afya na elimu, lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa pesa zile bado hazijafika kwenye maeneo yetu. Waziri anafahamu kwamba Waziri wa TAMISEMI aliwaita Wakurugenzi wakakubaliana kwamba ni miradi gani ya kimkakati ambayo wanapendekeza kwenye Halmashauri zao na wakataja ile miradi. Kwa hiyo, tumuombe sana Mheshimiwa Waziri suala la afya na elimu ya msingi na sekondari ni muhimu sana katika majimbo yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu wananchi tumewahamasisha, wamejenga madarasa, wamejenga zahanati, wamejenga vituo vya afya, wanategemea Serikali watakwenda kumalizia kupaua na taratibu zingine ili madarasa haya yaweze kutumika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba ajitahidi kama anaweza atupatie ile shilingi bilioni 251 ili Waheshimiwa Wabunge wote wakitoka humu waweze kuwa na jambo la kuzungumza kwa wananchi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, sisi wote tunafahamu bila maji hakuna uhai. Waislamu huwa tunafunga na leo bado watu wanaendelea kwenye sita, akifungua kitu cha kwanza anakimbilia maji. Sasa tunazungumzia miradi ya maji, hali ya miradi hiyo siyo nzuri. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atukubalie kwenye mapendekezo ya *Finance Bill* tuone ni jinsi gani tunaweza tukapenyeza hapo ile Sh.50 kwa ajili ya kwenda kwenye Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linawezekana, hata kama Wabunge wengi waliosimama hapa hawakusema lakini kila mmoja ukimuuliza hapa ni wangapi wanapendekeza ile Sh.50 iongezwe ili iende kwenye Mfuko wa Maji, wote watasema ndiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba kwenye *Finance Bill* aweze kuliangalia hili na sisi tuko kwenye Kamati ya Bajeti tunaendelea kutoa mapendekezo nadhani na hili tutalileta kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie kilimo. Uvinza ni wakulima wa tumbaku lakini zao hili wakulima wamefika mahala wamelikatia kabisa tamaa na chanzo kikuu wanachokitegemea halmashauri ni zao hili. Tunaomba sana Wizara ya Kilimo iangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Mikoa ya Kusini wanaomba zile shilingi bilioni 81, lakini na mimi pia nazisemea zile shilingi bilioni 81 kwa sababu asilimia 65 kwa mujibu wa sheria inatakiwa iende kwa wakulima wa korosho, tunaomba ziende. Kwa nini nasema hivi Mheshimiwa Waziri? Waziri ni mzaliwa wa Kigoma, Naliendele wametuletea miche ya mikorosho, tumepokea miche ya mikorosho, tumehamasisha, wananchi wa Uvinza wamepanda korosho kwa mara ya kwanza. Sasa wakisikia korosho imekufa Ukanda wa Kusini na wenyewe watakata tamaa. Kwa hiyo, tunaomba ile asilimia 65 ipelekwe ili na mikoa mingine kama Tabora, Kigoma, Dodoma ambao tumeitikia kulima hili zao la korosho basi tuweze kupata motisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie miundombinu. Tunapitisha bajeti za Wizara hapa lakini hatimaye inafika tarehe 30 Juni, utekelezaji hakuna. Natambua kwamba sisi tumepata pesa ya Daraja la Ilagala, nimwombe Mheshimiwa Waziri atuletee hiyo pesa ya kujenga Daraja la Ilagala. Wananchi watakuwa wameokoka na vifo vya wamama wajawazito na watoto vitapungua. Wanapopata uchungu wakifika kwenye *ferry, SUMATRA* wametuambia saa 12.00 jioni ndiyo mwisho wa kivuko kutumika. Daraja la Ilagala likijengwa wale wanawake wa kata sita watakuwa wanavuka wanaenda kwenye Kituo cha Afya cha Ilagala wanajifungua kwa wakati bila madhara yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia hili suala la *Electronic Tax*. Hili suala siyo baya, tunachosema sisi tunaomba yale mapendekezo ya Mwenyekiti waKamati ya Bajeti yapokelewe na yazingatiwe. Kwa sababu huyu mtu kwa muda wa mwaka mmoja atakuwa amerudisha hela yake na faida juu. Tunapompa mkataba wa miaka mitano tunaonesha ni jinsi gani ataondoka ametajirika kwa pesa za

walalahoi. Kwa nini nasema za walalahoi? Tukitumia huu mfumo kwa kampuni hiyo tuliyoipendekeza wanaokwenda kuathirika ni walaji, mfano, wanywaji wa soda, bia na maji na wavutaji sigara. Kwa hiyo, hatulikatai hili lakini kwa nini basi tusitoe kipaumbele kwenye kampuni za wazawa? Kwa hiyo, hili suala liangaliwe tusilirukie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie ukurasa wa 72. Wilaya ya Uvinza ni wadau wa chumvi. Tunashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri ameona umuhimu wa kutoa tozo mbalimbali. Kwenye hii tozo ya kwanza ukurasa wa 73(a), kufuta ushuru wa mazao ya chumvi unaotozwa na halmashauri, Mheshimiwa Waziri ametuua. Halmashauri ya Uvinza tunategemea tumbaku na chumvi, hii 0.03 tunaomba atuachie. Leo tulikuwa na mmiliki wa kile kiwanda yeye mwenyewe ameona kwamba hii 0.03 isifutwe, iendelee kuwepo ili na sisi halmashauri tuweze kupata hapo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri, tunayo madini ya chokaa. Madini haya hapa Tanzania hatuna viwanda vikubwa tuna viwanda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, malizia.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili la kwenye chumvi liende pia na kwenye chokaa ili wanaochimba chokaa waweze kunufaika na mimi pia ni mdau wa suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Alhaj Abdallah Bulembo, Mheshimiwa Jesca na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ajiandae.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niungane na wenzangu lakini awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Mpango, hongera sana, unajua mishale hii inavyopigwa ndiyo maana amekalia kiti hicho. Kwa hiyo, awe mvumilivu maana asingekikalia asingepigwa. Nimpongeze shemeji yangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Ndugu Dotto, Manaibu wake wote, Makamishna wa *TRA* na wengine wote, hongereni kwa kufanya kazi katika eneo ambalo kila mtu anaangalia maana ni maeneo ya pesa hayo, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa kwanza ni katika eneo la bima. Mwaka jana tulipitisha sheria hapa kwa ajili ya *NIC* lakini ndani ya bima hii kuna watu watatu. Kuna huyu mkubwa *NIC*, *broker* na *agent*. Mheshimiwa Mpango mbona *broker* hawa mnawaua? Kwa nini mnatoa maelekezo watu waende *direct* kwa *insurer*, hawa *broker* waende wapi? Leseni mnachukua, sheria iliyowaunda ipo, hamuwasaidii, kwa nini tunaiua hii *industry*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inatakiwa ifanye kazi na mashirika mbalimbali lakini *broker* mmemuweka ninyi. Kama hafai basi naomba tulete sheria ya kumfuta na tukimfuta mniambie kama *NIC* ana rasilimali watu wa kuweza kuhudumia maeneo yote haya, hawezi. Nakuombeni sana, kama kuna waraka mmeutoa ule kwenye bima, huyu bwana mgeni wa bima huyu mwambieni aanze kusoma upya kidogo kwamba hawa *broker* bila kuwepo yeye hawezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina miradi mingi mikubwa. Tuna ndege, *standard gauge*, tuna madude makubwa sana, kwa nini hamuweki kwenye *clause* za *procurement* zenu kwamba mwekezaji yeyote atakayekuja *insurer* atakuwa *NIC*? *NIC* kama hawezi ata-*syndicate* na watu wa nje lakini atapata pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wakati anakuja kwenye ushauri wangu hebu walindeni *brokers* na *agents*. Kwa nini *agent* wanakuwepo, huwezi kukata *insurance*

mahala popote, lakini mnaposema mtu aende *direct* hawa watu mnawaua.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni ushuru wa *stamp*, dakika 10 ni kidogo. Sipingani na ushuru wa *stamp* nakubaliana nao lakini nina maswali. Kwanza miaka mitano ni mingi kwa mujibu wa hesabu, Waziri akija hapa atuambie kama ni mwaka mmoja au miwili tutamuelewa. Pili, tatizo ninalolipata huyu mtu akitengeneza lita moja na nusu analipa Sh.13,500, lakini chupa moja na nusu ile ina mia tano mara tatu, ukipiga hesabu yake Sh.13,500 ni Sh.40,500 na hawa wanywa maji ndio wengi zaidi kuliko hii lita moja na nusu, hesabu mbona haikubali? Tunapiga hesabu gani? Unaenda kwa mtu wa *soft drinks* unataka alipe Sh.13,500 kama anauza 150 haiwezi tena kuendelea kuwa Sh.13,500 itakuwa Sh.13,200. Kwa nini huyu mtu wa chini ndiyo tunamuumiza zaidi? Kwa nini tusielekee kwenye bia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hakuna soda ulishasikia ni *forgery,* hakuna soda ya kutengeneza mtaani, lakini hizi pombe kali hizi ndiyo zinatengenezwa magarasha mengi huku mtaani, kwa nini bei kubwa hii tusingeipeleka kwenye pombe kali? Kwenye mapendekezo yenu pombe kali mnaiweka mbali kidogo. Naomba tuelekee hapa ili tumsaidie mtu wa kawaida anayekunywa maji na soda aendelee ku-*relax*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai, kwenye Kamati ya Bajeti tumeangalia mtu huyu atapata hii hela kwa mwaka mmoja tu, hata tufanyeje *capital* anayoitumia na faida yake mwaka mmoja inamtosha, tunampa miaka mingi ya nini? Waheshimiwa Wabunge nawaombeni tuweke mguu chini, apewe mwaka mmoja au miwili, *stamp* hatuikatai baada ya hapo hii iwe shughuli ya *TRA* kiwe chanzo chao. Kwa nini tumtajirishe mtu mpaka mwisho na hizi hela anapeleka nje, hazikai nchini. Mheshimiwa Waziri tusaidie hapo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahamia kwa wakwe zangu kule Mtwara na Lindi kuhusu korosho. Hivi hii hela ya korosho ni yetu kwani? Serikali hii hela ni yetu? Tunaitaka ya nini? Kwa

nini tutunge sheria kwa sababu tumeona kuna mapato? Hiki ni chanzo chao wapeni. Mkienda kwenye pamba chanzo chao wapeni, mkienda kwenye kahawa wapeni. Kwa nini Serikali tunaingia kwenye ugomvi ambao hauna msingi, msingi wa hizi hela ni nini? Kwa nini tuliue zao hili? Kwa nini tuue kahawa na pamba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hii siyo chanzo cha Mheshimiwa Dkt. Mpango, pesa hii inatoka kwa mkulima mwenyewe, sasa unaipangiaje bajeti, unaiwekaje kwenye Mfuko wa Pamoja? Jamani sisi tunakaa jukwaani kuomba kura, msitupe tabu kabisa. Yaliyotokea Mtwara tunayajua, tusijifanye kuna pamba masikioni. Tumefanyaje Mtwara kupata amani mnajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasema Mheshimiwa Bwege hapa mkaona kawaida, siyo maneno madogo hayo kwenye siasa, ni maneno makubwa sana. Lazima muende mbele mrudi nyuma, hela hizi kwa nini zitupe kero zinatusaidia nini? Nawaombeni Serikali sikivu mpo mnasikia, wote mpo hapa, nendeni mjadiliane, achaneni na hela ya korosho msituletee balaa, wapeni hela zao tuendelee na vyanzo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeletewa Sheria ya Serikali za Mita, nataka kuunganisha mambo yote lakini sasa nataka kuongelea asilimia 10. Tumeondoa vyanzo vingi kwenye *Local Government,* kuna Halmashauri haziwezi kuwalipa Madiwani posho zao na kuweka mafuta lakini hapa tunasema asilimia 10 wakipata tunaiundia sheria, nakuja na wazo jipya nini tufanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye *Municipality* za Dar es Salaam, Ilala, Arusha, Mbeya na Ilemela Mwanza hawa walipe asilimia 10 lakini zile Halmashauri ambazo zinashindwa kununua mafuta, Serikali kwa sababu mmechukua vyanzo m-*top up* pale asilimia 10 muipeleke kama ruzuku kule chini ili akina mama na vijana wakope. Haiwezekani Halmashauri inakusanya shilingi milioni 100 posho za Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa haziwezekani

halafu tunawaruhusu kwamba kweli kila Halmashauri itoe asilimia 10 kwenye chanzo gani? Kuna vyanzo gani mmebakiza huko? *TARURA,* mabango na *property tax* mmeondoa, hakuna kitu kule. Kwenye *Municipality* na Majiji kwa sababu kuna watu wengi inawezekana lakini huku chini siyo, naomba mrudi nyuma muangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea hapa nikiamini mwaka kesho ni mwaka wa uchaguzi, tusipate tabu za lazima hapa kwa sababu ya bajeti. Halmashauri hazijiwezi, hazijiendeshi wapelekeeni ruzuku ya *10%* ili mikoa, wananchi na halmashauri zote wawe na uwezo wa kukopa asilimia 10. Tusitoe mfano wa Kinondoni au Ilala ukafananisha na Katavi na Tunduru, havifanani! Nchi hii iko tofauti na mapato yapo tofauti. Kwa hiyo, hiyo asilimia 10 huko juu muiangalie tuwapelekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye michezo ya kubahatisha kuna Bahati Nasibu ya Taifa haipo katika nchi yetu, ipo hatujui inafanya kazi wapi. Kwa nini Bahati Nasibu ya Taifa tunaitoa 6 kuipeleka 10, tunataka nini? Bahati Nasibu ya Taifa sehemu nyingi zilizoendelea ukienda Ghana, Nigeria na sehemu nyingine chanzo hiki ni cha Serikali Kuu kwa maana ya Wizara ya Fedha. Ninyi mnatakiwa mtafute anayeweza mkae naye lakini huyu akipatikana atatengeneza nchi nzima kwa sababu ata-*invest* mtaji wake. Kwa nini mnamzuia kabla hajaja, tunaweka hiki chanzo cha nini, kwa nini tunaongeza hela hapa? Tutakosa watu wa kuja kufanya kazi hii na hii hela ni ya Serikali. Chanzo hiki kingekuwa kinafanya kazi vizuri mngepata hela nyingi za bure pale zipo, lakini mkiongeza kodi wawekezaji watajikata, itakuwa shida. Kwa nini msikubaliane katika hili?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, malizia.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema ninyi watu wa Mifugo

muende pale Masaka Uganda ukifika Lukaya wanafuga *bycatch,* mjifunze wenzenu wanafanyaje muache kutembea na rula. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Jesca, Mheshimiwa Bukwimba na Mheshimiwa Prof. Maghembe wajiandae.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni bahati mbaya sana huu ni mwaka wa tatu nikiwa humu Bungeni kama Mbunge, kwenye Mabunge ya Bajeti, Bunge linakuwa linajikita zaidi kujadili ni namna gani Serikali itumie fedha badala kwa sehemu kubwa kujadili ni namna gani Serikali ikusanye fedha. Nitakwenda kujikita kwenye eneo la ukusanyaji wa fedha. Kuna eneo moja ambalo ni *very strategic* napenda Mheshimiwa Mpango alizingatie kwa umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua kwamba Serikali inamiliki *shares* kwenye makampuni mbalimbali, yapo makampuni ambayo Serikali ina *total ownership* lakini pia yapo makampuni ambayo Serikali inamiliki asilimia fulani ya *shares*. Kuna changamoto kubwa sana hapa, haya makampuni ambayo Serikali inamiliki *share* kadhaa yamekuwa yana tabia ya kutoa taarifa ambazo siyo sahihi. Haya makampuni yanatoa taarifa ambazo siyo sahihi kwenye mitaji yake, faida inayoingiza na usahihi wa gawio ambalo linatolewa Serikalini. Sababu kubwa ya Serikali kushindwa kukagua gawio ambalo inapata kutoka kwenye makampuni haya ni kwa sababu kuna sheria ambayo ipo inambana/inamzuia *CAG* kufanya uchunguzi kwenye makampuni ambayo Serikali inamiliki *shares* chini ya asilimia 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mpango hauoni kwamba kuna haja kubwa sana ya Serikali kuchukua *shares* zake kuzihamisha kutoka kwenye haya makampuni na kuzipeleka kwenye Soko la Mitaji *(Stock Market)?* Tunajua kwamba kwenye *Stock Market* kuna *very serious scrutiny,* wanafanya ukaguzi wa kina na mahesabu

yanawekwa wazi. Napenda kutumia fursa hii kumwomba sana kuchukua *shares* kutoka kwenye makampuni mhamishie kwenye Soko la Mitaji ili muweze kujua haya makampuni yanaingiza mtaji na faida kiasi gani na mwisho mjue usahihi wa gawio ambalo Serikali inapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifano mizuri sana. Makampuni yote ambayo yako *listed* kwenye soko la mitaji mfano *NMB* na *TBL* wanafanya vizuri sana, wanatoa gawio kubwa kwa Serikali lakini pia wanatoa kodi kubwa sana kwa Serikali. Ni kwa sababu kuna uwazi mkubwa ambao unatokana na *Stock Market.* Hata humu Bungeni tulipitisha sheria ya kuyataka makampuni ya mawasiliano na makampuni ya madini kuwa *registered* kwenye Soko la Mitaji *purposely* kutaka yawe wazi. Sasa unajiuliza kwa nini hamuoni umuhimu kwenye eneo ambalo mna-*interest* kwa sababu mna *shares* kwenye haya makampuni, mkachukua *shares* mkazipeleka kwenye Soko la Mitaji ili muwe na uhakika wa gawio ambalo Serikali inaingiza? Naomba atakapokuja ku-*wind up* hapa ajaribu kuligusia hili kwa umuhimu wake mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mpango vizuri sana; kuna eneo nimeona amefuta kodi kwa ajili ya ku-*influence the investors, well and good*, hilo nampongeza sana. Kuna jambo moja ambalo napenda kumshauri, kuna kodi ambayo ina utata mkubwa sana, nashauri ipitiwe upya ikiwezekana na yenyewe iondolewe kwa sababu ina-*discourage* sana *investors.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *investor* anaweza akaja aka-*invest* kupitia viwanda moja kwa moja na yupo mwingine anaweza akaja aka-*invest* kupitia kununua *shares* kwenye Soko la Mitaji. Sasa unakuta mwekezaji ameweka *shares* zake kwenye Soko la Mitaji, zimekaa kule labda takribani miaka mitatu akaona hakuna kinachoongezeka akaamua kutaka kuziuza, anapokwenda kuziuza muda aliotumia kununua labda ni miaka mitatu iliyopita, *let's say* labda alinunua dola 1,000 kwa miaka mitatu iliyopita wakati huo *exchange rate*

ikiwa ni Sh.2,000 akaja labda akauza baada ya miaka mitatu *shares* zile zile dola 1,000 kwa *exchange rate* ya Sh.2,200, mnakuja kumtoza *Capital Gain Tax* kwenye ongezeko la *exchange rate*. Hii kodi ina-*discourage* sana *investors,* nashauri hii kodi iondolewe kwa sababu mnapokuja kukata *Capital Gain Tax* kwenye ongezeko la *exchange rate* mnakuwa hamuwatendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo napenda pia kuligusia kwenye sekta ya mifugo. Haya ni maajabu ya dunia, Tanzania tunazalisha maziwa kwa mwaka takribani lita bilioni 2.4, Kenya hapo majirani zetu wanazalisha kwa mwaka lita takribani bilioni 5.4, tuna *difference* karibu ya lita bilioni 3. Kinachonishangaza zaidi ni kwamba wakati Kenya wanazalisha lita za maziwa bilioni 5.4 Tanzania tunazalisha lita bilioni 2.4 wakati tuna ardhi kubwa sana, mito mingi sana, maziwa na mifugo mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Mpina na nashukuru yupo hapa, hakuna sehemu yoyote nimeona amegusia suala hili na ameeleza ana mkakati gani kuifanya Tanzania kuwa *champion* kwenye uzalishaji wa maziwa. Kama Taifa tuna kila sababu ya kuwa maridadi kwenye uzalishaji wa maziwa kutokana na namna ambavyo tumebarikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na suala la *LNG.* Hili suala la *LNG* nililizungumza toka mwaka 2015 naingia humu Bungeni. Limekuwa ni suala ambalo limepigwa danadana miaka nenda miaka rudi. Nilipitia jarida moja la *Reuters* mwezi Machi, 2018, *TPDC* wananukuliwa wanasema kwamba makubaliano ya *LNG* pamoja na haya makampuni mjadala wake kwa sababu umeshakuwa mzito na wameushindwa, Serikali imetangaza sasa apatikane Mshauri Mwelekezi aweze kutoa mawazo yake aisaidie Serikali kuweza kuingia makubaliano sahihi na haya makampuni. Mkurugenzi wa *TPDC* akanukuliwa akisema kwamba toka mwezi Machi mpaka kufikia mwezi wa Mei, suala hili litakuwa

limekwishatekelezeka, lakini mpaka sasa hivi tunaenda mwezi Agosti hakuna kunachoeleweka wala kinachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana kwa sababu huu ni mradi ambao unakwenda kutengeneza historia mpya ya Taifa letu katika ukanda wa Afrika Mashariki, hakuna mradi mkubwa kama huu Ukanda wa Afrika Mashariki nzima. Ni mradi mkubwa sana. Ni *investment* kubwa sana ambapo kama Serikali nilitegemea hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri angeielezea kwa mapana yake, kwa uzuri na kwa kuifafanua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyoendelea kuchelewa hivi Msumbiji wameshateka soko lote la *East Africa.* Ni vema tukatumia nafasi hii vizuri, kama huyo mtaalam mnamtafuta wa kuja kusaidia ku-*negotiate* kwenye masuala ya kisheria na kuhakikisha kwamba kunakuwa na *win-win situation do that,* kwa nini mnachelewa? Kwa nini suala hili mnakuwa mnalipiga danadana miaka nenda miaka rudi? Inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie Deni la Taifa. Deni la Taifa linazidi kukua kwa kasi ya ajabu na linazidi kukua kwa sababu kuna mambo mengine ambayo tunayaona kama ni madogo lakini yanachangia kwa kiwango kikubwa sana ukuaji wa deni hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kumsikia Mheshimiwa Rais hata Mheshimiwa Waziri kipindi fulani akisema kwamba Serikali iko pia *busy* kulipa madeni ya kipindi cha nyuma sana. Kwa kufanya hivyo, tafsiri yake ni kwamba kuna fedha ambazo Serikali inalipa madeni ya nyuma ambayo yalikopwa kwa *exchange rate* ya kiwango hicho kwa wakati huo. Mnapokuwa mnalipa wakati huu mnalipa kwa *exchange rate* ya wakati huu kwa maana hiyo mnakuwa mnalipa fedha nyingi zaidi ukilinganisha na kama madeni hayo yangelipwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna njia ambayo niliisoma ambayo Uganda wanai-*apply* katika kukopa na kulipa. Kuna mfumo ambao...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia, kama huwezi basi, maana inaelekea darasa zuri unapata nyumbani kutoka kwa Mr. Kwa hiyo, ahsante. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Bukwimba na Mheshimiwa Prof. Maghembe ajiandae.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wameifanya hasa katika kuandaa bajeti hii muhimu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nichukue nafasi hii kupongeza kwa dhati kwa kuondoa kodi kwenye taulo za kike ambayo ilikuwa ni kero ya muda mrefu. Tuna imani kubwa huu ni mwanzo mzuri na kwamba wananchi sasa hasa akina mama na watoto wa kike wataweza kunufaika kwa kuondolewa kodi katika taulo za kike kwa ajili ya kujihifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nichukue nafasi hii kupongeza sana kwa jinsi ambavyo wameweka kipaumbele cha kwanza kabisa kwenye suala la kilimo ikifuatiwa na suala la viwanda, hatimaye kwenye huduma za jamii na mwisho kabisa kwenye miundombinu muhimu wezeshi kwa ajili ya uchumi kukua. Nikianza kwenye sekta ya kilimo, ni muhimu sana kwa sababu asilimia kubwa ya Watanzania wanajishughulisha na kilimo. Kwa sababu hiyo

Serikali ikiangalia suala la kilimo hasa ambavyo imezungumza kwamba itawezesha kuanzisha skimu za umwagiliaji, nipongeze sana kwa ajili ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa tunalo Ziwa Viktoria na mikoa mingine kwa mfano Ziwa Tanganyika na maziwa mengine, tukianzisha skimu za umwagiliaji nina uhakika kwamba wananchi wataweza kunufaika, tutapata mazao ya uhakika mwaka mzima. Kwa hiyo, nipongeze tu na niombe sasa utekelezaji uwe ni wa kweli katika jambo hili, lisije tu kuonekana kwenye karatasi lakini kwenye vitendo halisi lisionekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika suala la kilimo ni muhimu sana Serikali iangalie namna sasa ile Benki yetu ya Kilimo *(TADB)* ambayo tumeianzisha inavyoweza kufanya kazi. Hii benki kweli ipo lakini inapatikana mjini tu. Kwa mfano, kwenye Kanda yetu ya Ziwa Benki ya *TADB* inapatikana Mkoani Mwanza. Sasa mkulima wa kawaida siyo jambo rahisi kutoka Geita avuke kote kule mpaka Mwanza kwenda kuchukua mkopo kwenye Benki ya *TADB.* Kwa hiyo, Serikali iangalie sasa kujenga mazingira mazuri kuwezesha benki HII iweze kuwafikia wananchi hasa wakulima vijijini ili waweze kunufaika katika suala zima la kupata mikopo nafuu ili kujikimu na kujiendeleza katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pia, suala la wataalam katika sekta ya kilimo ni muhimu. Nasema hivyo kwa sababu mara nyingi katika vijiji vyetu siku hizi hakuna wataalam kabisa wa kilimo. Unakuta mtaalam mmoja anapatikana kwenye makao makuu tu ya kata ambapo wakulima wanapatikana vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa Serikali imeweka kipaumbele kuboresha suala la kilimo, tuangalie uwezekano wa kuwa na wataalam wa kutosha kwenye vijiji na kata. Kikubwa zaidi wataalam hawa wafanye kazi zao vizuri kuwaelimisha wakulima badala ya kilimo tulichokizoea ambacho hakina tija, tuweze kubadilika kuwa na kilimo

chenye tija na hatimaye tuweze kukuza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika viwanda, nipongeze sana kwamba Serikali imejikita kujenga mazingira wezeshi ili wawekezaji wengi waweze kuingia ndani ya Tanzania na kuwekeza, pia hata wawekezaji wa ndani. Naomba sasa katika suala la uwekezaji na viwanda muwaangalie wafanyabiashara ambao kwa muda mrefu wafanyabiashara wengi wamekuwa na changamoto nyingi sana. Mimi natokea kwenye eneo ambapo kuna sehemu kuna biashara kubwa kwa mfano katika *center* moja ya Katoro, wafanyabiashara wana changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali kwa ujumla iangalie namna ya kutatua kero na changamoto mbalimbali za wafanyabiashara ili waweze kuendelea kuwekeza zaidi kwenye viwanda kwa sababu bila kuwalea hawa wafanyabiashara wadogo ambao wapo sasa haiwezekani wakaweza kuwa wafanyabiashara wakubwa. Naomba katika fedha hizi ikiwezekana kuwepo na fedha kwa ajili ya kuwaelimisha zaidi wafanyabiashara wadogowadogo, kikubwa zaidi mazingira yao ya utendaji wa kazi yaweze kuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kutokana na kwamba mara nyingi unakuta *TRA* wana-*harass* sana wafanyabiashara vijijini, wanakwenda pale mtu anarundikiwa kodi hapa na pale, kunakuwa na mazungumzo ambayo siyo mazuri. Nashukuru kwenye bajeti hii Waziri ametoa kauli kwamba kuwepo na urafiki kati ya *TRA* na wafanyabiashara. Napongeza sana *statement* hiyo, niombe sasa walioko kule kwenye wilaya na mikoa wahakikishe wanafanyia kazi jambo hili ili kuwezesha wafanyabiashara wadogo waweze kufanya biashara zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la huduma za kijamii ikiwemo sekta ya afya, naishukuru sana Serikali kwa sababu imewekeza sana kwenye afya. Nilikuwa najaribu

kusoma katika mpango huu, sijaona mpango wa Serikali kuajiri watumishi wa sekta ya afya. Natoa msisitizo kwamba katika bajeti ya mwaka huu tuangalie namna ya kuajiri watumishi katika sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tu kwenye Halmashauri yangu ya Geita tuna upungufu wa wataalam wa afya 200. Ndiyo maana kunatokea changamoto za vifo vya akina mama na watoto wakati wa kujifungua kwa sababu hakuna mtoa huduma katika zahanati au kituo cha afya. Kwa hiyo, napongeza kwa kazi kubwa kwamba tunajenga vituo vya afya na zahanati lakini tuongeze wataalam katika maeneo haya ili waweze kufanya kazi zao kusaidia wananchi, hasa ambao wanapata matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu unakuta kituo cha afya au zahanati kina mtaalam mmoja au wawili, ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, niombe Serikali kwa kuwa kwenye bajeti huku sijaona hilo, nimejaribu kuangalia lakini sikuweza kuona, nitoe tu msisitizo kwamba mwaka huu wa fedha tuajiri wataalam wa kutosha katika sekta ya afya ili kuwezesha akina mama na watoto waweze kuwa na afya pia waweze kufanya kazi zao vizuri. Unakuta hao hao wachache wanapata shida sana maana watu wanaosubiri huduma ni wengi. Kwa hiyo, wakati mwingine mtu anaweza akawa na majibu hata ambayo hayaeleweki kwa sababu amechoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sekta ya maji ni muhimu sana hasa vijijini. Niombe tuweze kutekeleza kama ambavyo tumepanga, kwa sababu tulivyopanga hapa mipango ni mizuri sana. Nachoomba utekelezaji uweze kufanyika ili tuweze kuwafikia wananchi wetu katika kuwapa huduma kadri ambavyo Serikali imekusudia, *otherwise* bajeti iko vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa makusanyo, kuna changamoto kubwa sana. Kwenye matumizi ya vile vifaa vya kielektroniki kwa kweli kuna changamoto kubwa

sana na ndiyo maana Serikali haipati mapato ya kutosha kwa sababu vifaa hivi havipatikani. Hata vilivyopo pale havifanyi kazi vizuri, unakuta unakwenda labda kituo cha mafuta lakini hupewi risiti, unaifuatilia risiti unaweza ukatumia nusu saa nzima kuipata. Kwa hiyo, watu wengi wanakata tamaa wanaziacha na mwisho wa siku Serikali haipati mapato yake sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango waangalie jambo hili kwamba namna gani tuweze kuboresha ili utoaji wa risiti na upatikanaji wa mashine hizi uwe mzuri. Kuna nchi nyingi za nje, nimebahatika kusafiri nje pia, kila ukipewa huduma yoyote mahali popote pale lazima utapewa risiti saa hiyo hiyo tena kwa haraka. Katika nchi yetu unapewa huduma labda ya mafuta lakini inakuchukua nusu saa kupata risiti, wakati mwingine unakata tamaa unasema labda niondoke. Niiombe Serikali hapo muendelee kuweka nguvu zaidi katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi tutoe elimu kwa wananchi kuomba risiti. Kwa sasa hivi elimu ipo lakini wanachi hawaombi zile risiti. Nnasema hivyo kwa sababu juzi tu kituo cha mafuta kina risiti nyingi watu hawachukui risiti zao. Kwa hiyo, Serikali iwekeze kwenye elimu ya mlipa kodi, kwa sababu bila ya kodi hatuwezi kupata maendeleo katika nchi yetu. Wananchi wana uelewa mkubwa wakielimishwa wanaelewa vizuri. Kwa hiyo niendelee kuomba Serikali kupitia Wizara husika tuendelee kutoa elimu hii na Wabunge tushirikiane kwa pamoja kuwaambia wananchi na wananchi wana uelewa mkubwa, tusisitize suala la kuomba risiti ni kitu muhimu sana ili kuweza kuchangia katika pato la Taifa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miundombinu, naipongeze sana Serikali kwamba imekusudia kujenga mradi mkubwa sana wa umeme *Stiegler's Gorge.* Nina uhakika kwamba kupitia mradi huu wananchi tunaweza kupata umeme wa uhakika. Kikubwa zaidi niombe

sasa Serikali iendelee kusambaza umeme kwa kasi hasa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napongeza sana Serikali na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Prof. Maghembe, Mheshimiwa Anastazia Wambura na Mhshimiwa Martin Msuha wajiaendae.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nijadili hoja yetu hii ya Wizara ya Fedha kuhusu bajeti kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kabisa kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na wataalam wao kwa kweli kwa bajeti nzuri sana mwaka huu. Kwa mara ya kwanza wale waliokuwa wanategemea kwamba bei za bia na soda ndiyo zitakuwa uti wa mgongo wa bajeti nadhani wameona kwamba kuna watu wanafikiri na kufanya kazi nzuri ya kutengeneza bajeti ya maendeleo ya nchi hii na mimi nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo makubwa ambayo wamefanya ni kuanza sasa kuelekea kwenye harakati za kuvutia sana wawekezaji. Hatua ya kupunguza Kodi ya Mashirika au *Corporate Tax,* utaratibu mpya uliowekwa wa kumpa Waziri mamlaka ya kuweza kusamehe kodi na hasa pale ambapo tulikuwa tunatoza kodi kwenye misaada ambayo tunapewa na nchi za nje, hizi ni hatua nzuri sana. Hatua hizi nzuri zimefanywa pamoja na kuandaa *Investment Blue Print* mpya kwa nchi yetu na tunategemea kabisa kwamba hatua hizi kwa pamoja zitaongeza uwekezaji wa wawekezaji wanaotoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe mapendekezo ambayo yanajenga hatua ambazo zimechukuliwa. Jambo la kwanza, Serikali ingefikiria kupunguza *VAT* kutoka 18% angalau ifikie 15%. Jambo la pili,

Serikali ingefikiria kuwatambua wawekezaji wa ndani kama ambavyo inawafikiria wawekezaji wa nje. Kwa sababu kwa vyovyote vile, hata kama tutavutia wawekezaji wengi sana kutoka nje lakini watakaojenga uchumi wa Tanzania na watakaokuwa wengi katika uwekezaji ni wawekezaji wa ndani, wawekezaji wadogo, wa kati na wakubwa katika nchi yetu. Hawa ndiyo watakuwa uti wa mgongo katika uchumi wetu, hili ni jambo muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo, ni muhimu Serikali ifikirie kupunguza riba ya mikopo kutoka kwenye mabenki yetu. Riba ya mikopo katika benki zetu inakatisha tamaa sana uwekezaji. Wawekezaji wa nje wanachukua mikopo kwenye benki zao kwa riba ya asilimia 1.5 mpaka asilimia 2, wawekezaji wa kwetu wanachukua mikopo kwa asilimia 21, ikiwa rahisi sana ni asilimia 15, hawawezi kushindana kwa vyovyote vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba kwa miaka 10 tumekuwa tunasukuma sana jambo hili na ni kama limeshindikana. Majirani zetu Wakenya walikuwa na hali kama hii, Bunge lao likachoka kusukuma *Central Bank* kupunguza riba na wakatunga sheria kwamba benki zisizidishe *interest level* fulani wanapotoa mikopo kwa ajili ya uwekezaji. Nasi hatuna haja sasa ya kujikusanya kama Bunge na kulazimisha benki yetu, lakini Serikali ifikirie kupunguza riba ili wawekezaji wa ndani waweze kukopa na kushindana na wale wa nje.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la lingine mwekezaji ni yuleyule. Wahenga wa Kipare wanasema kama unampenda jongoo lazima upende na miguu yake. Wawekezaji wa ndani kabla hawajaanza kufanya biashara wakapata faida ambayo ndiyo inatakiwa itozwe kodi wanakadiriwa kodi kwa maana wanatakiwa walipe kodi kwenye mkopo waliouchukua kuandaa uwekezaji, sasa haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutajengaje kada ya wawekezaji wa ndani kama tunaanza kuwakata kodi hata

kabla hawajaanza kuzalisha? Napenda tuanze kufikiria wawekezaji wa ndani na wenyewe wapewe *tax holiday,* wawekezaji wa nje tunawapa *five years tax holiday,* tufikirie kuwapa *tax holiday* wawekezaji wa ndani, angalau hata miaka miwili. Mapendekezo yangu yangekuwa kwamba kama tunaweza kuwangojea wawekezaji wa nje miaka mitano tusishindwe kumngojea mtu mwenye duka mtaani miaka mitatu ndiyo aanze kulipa kodi wakati amejizatiti katika biashara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda sana niliseme ni juu ya mashirika yetu haya yanaitwa *Regulatory Institutions.* Hizi *Regulatory Institutions* zetu kama *EWURA, SUMATRA, TBS* na mashirika yote haya ambayo yanatoa huduma hiyo, yanaundwa kwa lengo la kutoa huduma lakini yakianza kazi yanaanza kazi kama mashirika ya kukusanya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alisema hapa juzi Mbunge wa Singida Mjini, Mheshimiwa Sima, kwamba mashirika haya yote yangekuwa *managed* chini ya paa moja *(one roof)* yalipwe mchango mmoja tu halafu yawe yanatoa huduma kwa wawekezaji. Yanasumbua sana wawekezaji na uwekezaji unakuwa mgumu kwa sababu hiyo. Hayo ndiyo yalikuwa muhimu kwangu niliyoyaona katika upande wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, kwa *ingenuity* hiihii ambayo wametumia katika kuangalia kodi waangalie pia maeneo ambayo yanaweza kuleta mapato makubwa kwa Serikali kwa uwekezaji mdogo. Nitatoa mfano mmoja, hapa kwetu Tanzania tuna hekta ambazo ziko chini ya umwagiliaji 489,000. Uzalishaji katika haya mashamba ya umwagiliaji ya hekta 489,000 kwa uzalishaji wa mpunga ni kama tani moja mpaka tani moja na nusu kwa hekta moja. Kwa ujumla tunapata kama tani 700,000 kutokana na haya mashamba ambayo yameandaliwa kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wakulima wangefundishwa kilimo bora cha kulima mpunga na wakalima mara mbili kwa mwaka, hekta moja ingeweza kutoa tani 10 mpaka 15 kama wanalima misimu miwili kwa sababu wananyeshea. Kwa uzalishaji huo tungeweza kuwalisha mchele watu wa Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Kongo, Zambia, Mozambique na Malawi, wote ambao wananunua mchele kutoka nchi za nje. Hesabu ambazo nime...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Prof. Maghembe, malizia.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *calculation* ambayo nimefanya hapa juu ya bahasha kwa mwaka mmoja tungeweza kupata dola bilioni 3 mpaka bilioni 7 kutoka kwenye mpunga peke yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Martin Msuha na Mheshimiwa Albert Obama wajiandae. Hawapo, Mheshimiwa Obama.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia bajeti iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake yote, kwa kweli wanatupa ushirikiano mkubwa sana kwenye Kamati yetu ya Bajeti. Vilevile niendelee kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati na Makamu wake kwa kutuendesha vizuri ndani ya Kamati kwani tumeendelea kutoa maoni yetu kwenye sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kwa miradi inayotekelezwa na waliyoipanga kwenye bajeti

hii sisi tumeibariki, tunaona kwamba haina matatizo, ni miradi muhimu. Miradi ya ndege, meli kwenye maziwa na bahari huko na miradi mingine ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze bajeti kwani lengo linaonesha kwamba mnataka kulinda viwanda vya ndani na kuhamasisha uzalishaji. Kwa hiyo, hilo nalo tunawapongeza na tunampongeza Rais kwa dhamira njema ya kuleta bajeti nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo machache tu kwenye ushauri ambayo napenda niyaseme. Kwanza ni namna ambavyo tumeanza kuua halmashauri zetu. Nilikuwa nafikiri mpaka muda huu tungekuwa tumeshaleta sheria ya kufuta *local government* kwa sababu sasa hivi meno yote yameondoka. Ukiangalia vyanzo vingi vimechukuliwa, miradi mingi ya maji imekwenda Wizara ya Maji, kilimo ndiyo hivyo na mambo mengine. Kwa hiyo, ifike hatua mlete sheria ya kuua huu ugatuaji ambao tuliupigania kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tulikuwa na Waziri wa Fedha tumeongea naye juu ya namna ya kuanzisha akaunti ya pamoja ndani ya Wizara ya Fedha, hii ambayo inaonesha kwamba halmashauri zetu zitakufa. Kwa hiyo, nashauri kwamba tulete sheria tuweze kufuta halmashauri zetu mara moja ili tuweze kuendelea na *centralization* ambayo tunaitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu wakulima wa zabibu wa Mkoa wa Dodoma. Kodi zilizopo kwenye zabibu na mvinyo unaotengeneza pombe kali kama *valour* zinazotokana na zabibu iko juu, tunaomba iangaliwe. Wakulima wa zabibu Mkoa wa Dodoma wanalia kwelikweli, tunaomba kwa kweli iweze kuiangaliwa ili kwenye *Finance Bill* muweze kuleta *amendment* kama Serikali ili tuweze kuwaokoa. Walikuwa wamezoea kodi ya Sh.450 sasa mmepeleka karibu Sh.3,315. Kwa hiyo, tunaomba hilo eneo waweze kuliangalia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ni kuhusu *ETS.* Kwenye *ETS* Mheshimiwa Waziri tumekaa naye kwa muda mrefu, mmetufundisha kama Kamati ya Bajeti lakini kuna maeneo ambayo bado tunaona kwamba kwenye bidhaa, bia, sigara hamkuongeza lakini mmeiongezea kwenye gharama ya kuweka hizo stempu ambapo wafanyabiashara itabidi waingie gharama kubwa kuliko waliyokuwa wanalipa ili kuweza kuweka hizo stempu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba hilo kwa kweli mliangalie, hizo gharama ziweze kuwa *revised.* Kwa kuwa *production* inaonekana itakuwa kubwa, kwa hiyo, tunashauri ile *rate* iweze kuwa ndogo. Tulifikiri teknolojia itaweza kuleta gharama ndogo zaidi kwani teknolojia haiwezi kuleta gharama kubwa. Kwa hiyo, tunaomba kwa kweli muendelee kuliangalia. Nimesikia, kuna mtu ameniambia anafikiri Mheshimiwa Rais amesema itakuwa miaka miwili lakini mmewapa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 2 Februari, Serikali yetu hii ili-*publish regulations* ambazo Kamati ya Bajeti ndiyo tumeziona leo. Hatujawahi kuona *regulation* ya *ETS* ambayo ndiyo hii hapa ilikuwa *published* lakini hatujawahi kuiongea kabisa. Nasi tumeisoma leo kidogo bado hatujamaliza na hatuwezi kusema mengi zaidi kwa sababu tutakutana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tujiangalie sana na mifumo maana kwenye sheria humu inasema kama mtu amefungiwa huo mtambo, wakati wa kuzalisha ikitoa hitilafu anatakiwa asimamishe uzalishaji. Wanasema *TRA* itaweza ku-*respond* katika saa 48. Tukumbuke *raw material* za viwandani zingine zina *expire* baada ya saa mawili au matatu, kama yameshakorogwa yanatakiwa yazalishwe. Sasa ikisimama inakuaje, hizo gharama nani ata-*incur*? Mheshimiwa Waziri ana timu nzuri, naomba muendelee kuliangalia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kodi ya ardhi. Wako watu wenye mashamba makubwa ya katani, pamba,

tumbaku, mmetoa gharama ya *land free* kutoka 400 mpaka 1,000, watu wana mashamba makubwa, kutengeneza shamba kwa muda mwaka inamchukua gharama nyingi na gharama nyingine tena ni ya kodi. Ardhi tulipewa na Mungu bure, ingekuwa sehemu ya mtaji wa mtu aendelee. Watu wana mashamba ya chai, *land rent* ni bei kubwa kuliko zao lililopandwa pale juu. Kwa kweli nashauri Waziri aweze kuliangalia hili na hata Waziri wa Ardhi aweze kuliangalia, msitumie ardhi kama ndiyo mtaji wa kila kitu na huku tulipewa na Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba wakandarasi walipwe. Kwa wale wakandarisi mliowahakiki muwalipe fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linatuudhi sisi watu wa Dar es Salam tunapokuwa tuko kule na katika Mikoa mingine ya Mwanza na kadhalika ni kufunga madukasaa 12.00 asubuhi mpaka saa 4.00 ya kila Jumamosi iendayo kwa Mungu katika mikoa yote ya Tanzania. Hebu tujaribu kufanya utafiti kuona hasara tunazozipata, kodi tunazozipoteza, unaamka asubuhi unataka kutumia fedha ya mtu anasafiri hakuna kibanda cha kutuma fedha. Watu tulizoea supu za asubuhi, hatuwezi kunywa supu Jumamosi. Mheshimiwa Waziri hebu mlipitie, sheria ya usafi tunaiheshimu, ingeweza ikatokea hata kwa mwezi mara moja, haiwezi kila Jumamosi ni matatizo huwezi kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja na Waziri ajue *challenge* kubwa ni kwamba tuna fedha kidogo lakini mipango ni mingi, lazima ifike mahali tu-*compromise*. Watu nao ni muhimu, kipato cha watu ni muhimu, kwa hiyo, tu-*balance* mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii kuchangia bajeti hii ambayo ina mwelekeo mzuri sana katika nchi yetu hii, hususani katika miundombinu ambayo itatuondoa hapa tulipo na kusogea mbele zaidi. Pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na uzima kuweza kusimama hapa kuzungumzia juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani kule ilikuwa mtu akitaka kubebesa ikiwa ile mistari ya kubebesea imemshinda basi huwa anatafuta maandiko matakatifu aidha aya za Quran au anaweza akatumia hata mistari ya Biblia ili kubebesea. Wakati mwingine ujue mtu kama huyu anakuwa ameshaishiwa. Kwa hiyo, wakati mwingine watu wanaotumia hizi aya inakuwa sivyo wanazitoa katika mantiki yake kwa sababu tu ya kutaka kuhalalisha neno analotaka kulisema, naomba hili tujaribu kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali hasa kwa marekebisho ya bandari, ikiwemo Bandari za Dar es Salam, Mtwara lakini pia na mipango iliyopo kwa ajili ya Bandari ya Tanga. Bandari inachangia zaidi ya asilimia 70 ya pato letu au ya kodi zinazokusanywa, bidhaa nyingi sana zinapitia bandarini, kwa hiyo naipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa kuwa tunazifanya hizi bandari zifanye kazi vizuri na tunazirekebisha, tuzidi kufanya kazi katika miundombinu iliyobakia kama reli na barabara ili huo mzigo unaopokelewa ufikie vizuri. Huo ni ushauri wangu baada ya pongezi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingine ni katika kuimarisha Shirika la Ndege. Sawa ndege zetu zitakuja na zitakuwepo, lakini pia naipongeza Serikali kwa kuimarisha viwanja vya ndege, kuna viwanja vya ndege14 ukisoma katika hotuba ya miundombinu vitafanyiwa marekebisho na zaidi vitawekewa taa za kuongozea ndege. Hapa naishukuru Serikali lakini ilifanye hili kwa haraka kwa sababu wasipolifanya kwa haraka ina maana tutapoteza vitu vingi sana au mapato mengi sana kutokana na ndege zetu kulala

jioni, ikifika jioni zinalala. Kwa hiyo, viwanja vya ndege tukiviimarisha ina maana hapa ndege zetu zitafanya kazi vizuri hata wakati wa usiku na itapunguza muda wa kulala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili ambalo limezungumzwa katika Wizara tano, suala la *VAT* ya bidhaa zinazokuwa *manufactured Tanzania Mainland* ambazo zitapelekwa Zanzibar. Tulifanya marekebisha mwaka 2016/ 2017 katika *Finance Act* tukaweka *zero rate*. Tumeweka *zero rate* lakini kwa mtu ambaye atanunua kwa *manufacturer* na *zero rate* kwa mtu ambaye ni *VAT registered.* Mheshimiwa Waziri hili suala analifahamu sana, tumelizungumza hapa siku ya Wizara ya Muungano ilikuwa kama ni changamoto, kama changamoto hii haijapatiwa ufumbuzi inageuka inakuwa kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Finance Bill* ya safari hii hatujaona hili suala. Zanzibar kule watu wanatozwa *VAT* asilimia 36; asilimia 18 anatozwa *original* na asilimia 18 anatozwa kule kwenye *destination.* Tatizo hili lipo katika ile sheria, kwa nini tusiondoe utaratibu huu tukarudia ule utaratibu wa marejesho kama ilivyokuwa zamani? Kwa sababu tukisema tunataka tutumie *destination principle* ina maana kwamba tuendane na vitu vinafuatana navyo. Mheshimiwa Waziri ni mtaalam zaidi katika masuala haya, hili suala linawaudhi wananchi wetu wa Zanzibar. Zanzibar hakuna mashamba, Zanzibar kuna wafanyabiashara. Kwa hiyo, wafanyabiashara hawa ukawawekea kikwazo ina maana kwamba maisha ya watu yanakua mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala linakosesha mapato Zanzibar na Bara, pia linasababisha magendo yawe makubwa zaidi na wafanyabiashara na mitaji yao itakufa. Kwa hiyo, naomba hili suala lifuatiliwe na litolewe ufafanuzi. Mimi nimeuliza Zanzibar wamesema hawajatoa ushauri kabisa katika suala hili na lilishazungumzwa kama kero mpaka mbele ya Rais wetu Mtukufu na hapa tumelizungumza sana lakini halijafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *Electronic Tax Stamp*. Suala hili kidogo naona kwangu liko kinyume zaidi. Kwanza siyo *economy*, fedha za kukusanyia ni kubwa zaidi kuliko kodi inayoenda kukusanywa kwa lita. Yaani lita *Excise Duty* yake ni ndogo kuliko gharama za kukusanyia hizo fedha zenyewe, kwa hiyo siyo *economy.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, nimejaribuni kulinganisha jedwali tumeweka *Excise Duty* kwa bidhaa ambazo zitatoka nje za vinywaji, ukija ukapima moja kwa moja ukihesabu ile gharama itakayoongezeka ya hii *Electronic Tax Stamp* ni kubwa kuliko gharama ambayo tumemtoza yule ambaye atatoa hicho kinywaji nje. Tukitazama katika majedwali haya tutaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo pia tumesema kwamba kuna mkataba, huu mkataba haiwezekani ikawa ni kikwazo cha kutoondoa maamuzi haya. Kwa sababu mtu unaweza ukaozesha mtoto ikawa siyo wako. Kwa hiyo, ukiozesha mtoto siyo wako ina maana kwamba lazima mkataba huo ufe au cheti hicho cha ndoa hakikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitolee mfano mwingine hata sumu mtu anapokunywa huwa anapewa maziwa. Kwa hiyo, kama tumeshaingia katika mkataba huu naomba tungejiondoa kwa sababu hauna maslahi kwa wananchi, walaji ndiyo watakaolipa gharama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia huyu *vendor* ambaye tunataka kumtumia Kenya tayari amekuwa *suspended,* kwa nini tunataka kumtumia? Kingine, kuna *regulation* tayari zilishatengenezwa. Kwa hiyo, ni sawasawa na kwamba tuko katika hatua ya kuvalishana pete halafu mtoto anazaliwa ina maana mtoto alizaliwa kabla ya ndoa, sasa hiki kitu naomba kiangaliwe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *tax amnesty* ambayo Mheshimwa Waziri amepewa uwezo katika *Tax Administration Act, section* 70. Naomba mngeshauriana na

mngeshauriana na Zanzibar, kwa sababu Zanzibar wanakusanya kodi *income tax* zinabakia kule kule. Ukisema Waziri wa huku unazisamehe na katika sheria *Minister* siyo *Minister responsible for Finance* wa Zanzibar inakuwa ni yule wa Tanzania. Kwa hiyo, naomba mngeshauriana nao kwa sababu mnaweza mkasamehe kitu huku lakini kule kikaleta *impact* katika mapato ambayo yanatakiwa yakusanywe katika *penalties, interest* na mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu tozo ya maji ya Sh.50. Tumeona ugumu wake, tutumie ile *bird in the hand fallacy,* mwenzetu Waziri ni Mchumi, ndege mmoja aliye mkononi ana thamani zaidi kuliko mia ambao wanaoruka katika mbuga au katika msitu au sehemu nyingine yoyote. Waswahili wanasema moja shika, siyo kumi nenda uje. Kweli Serikali imesaini mikopo hata juzi tumeona katika TV kutoka Ufaransa, lakini sasa hii ni ya kwetu, tukikusanya tutapata pesa yetu, hii ndiyo ile moja ya kwetu, moja shika siyo kumi nenda uje. Ndege huyu yuko mkononi ana thamani zaidi. Naomba hilo tulijali na tuweze kulisisitiza liwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe hongera kwa Serikali kuhusu taulo za kike. Ni sawa tunaipa hongera Serikali lakini taulo hizi za kike pia kuna baadhi ya bidhaa zinafungamana nazo navyo vingeweza kusamehewa. Kuna *equipment's* na *materials* pengine yanakuwa *imported,*hivi navyo pia tungejaribu kutizama ili tukapata uwanja mpana ili hili jambo likawa zuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kupunguza *Income Tax* kwa kampuni za wazalishaji wapya wa madawa. Naomba pia ingekuwa ni busara mkawashauri na wale wa Zanzibar kwa sababu makusanyo ya Zanzibar yanakusanywa Zanzibar na yanabakia Zanzibar. Kwa hiyo, ukisema huku ushasamehe hivyo watu wanatafuta *loophole* na anaweza akapenya na pengine inaweza ikaja ikaathiri. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ajaribu kutueleza, je, makubaliano yapi yalifikiwa katika suala hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni makusanyo ambayo Serikali Kuu itakuwa inakusanya kila kitu. Kusema kweli hapa kidogo inaweza ikatupelekea katika nafasi mbaya sana ya kiuchumi. Ina maana kwamba ukifeli upande mmoja kila kitu kinaharibika. Kila kitu kikiharibika ina maana lawama zote zitakwenda Serikali Kuu. Tujaribu kutazama hii *diversification* inasaidia, tukiwa na *portfolio* ya kukusanya mahali na kutumia katika maeneo mengine *atleast* inapunguza zile *risk* za kukwamakwama. Kuna vitu vingine utendaji wake utakuwa unakwama kwa sababu mapato yote yanakusanywa upande mmoja. Kwa mujibu wa sheria hii inayotaka kutumika sasa hivi, imewekwa baada ya siku moja kama fedha hazijatumika fedha zitarudi. Je, zitarudishwa tena kwa muda gani au ziombwe tena vipi? Kwa hiyo, hili naomba Serikali ijaribu kulitazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu korosho, asilimia 65 ya korosho katika *export levy.* Hili *at least* lingekuwa linafanyika kama lilivyopangwa, kwamba zirudi kwa wakati vinginevyo, jamaa zangu wa Kimakonde wana msemo mmoja wanasema kwamba, *'Channumbile Nnungu Cha Kumemena'*, ina maana kwamba kila kilichoumbwa na Mungu kinaliwa tu. Hizi asilimia 65 ikiwa haturudishi tukamemena hukuhuku tutawapa taabu na hili zao halitakuja kustawi tena. Tumetanua wigo wa zao, tumeongeza mikoa, sasa hivi hatuko Kusini peke yake tunakuja Kanda ya Kati, tunakwenda na Magharibi, kwa hiyo, tutazame kwamba hili jambo linaendaje katika huu ushuru wa korosho ambao unakusanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na Serikali ijaribu kuangalia ushauri ambao tunaipa. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yote ya wachangiaji wa leo imekwisha.

Wageni waliopo Bungeni jioni hii ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 15 wa Mheshimiwa Eng.

Atashasta Nditiye, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha St. John, wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na mwanafunzi mmoja kutoka Chuo cha Mipango. Karibuni.*kula aumbile (Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanachuo 25 na mwalimu mmoja kutoka Chuo cha Zion kilichopo Jijini Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Margaret Sitta, Mwenyekiti wa *TWPG* anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa katika kuelekea siku ya hafla ya uchangishaji fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya mtoto wa kike mashuleni *TWPG* imeandaa bidhaa mbalimbali ambazo zinauzwa kwa lengo la kuchangisha fedha za ujenzi wa vyoo vya mfano kwenye majimbo yote 264. Moja ya bidhaa hizo ni vikombe ambavyo vinapatikana lango kuu la kuingia Bungeni pamoja na lango kuu la Jengo la Utawala. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa kununua bidhaa hiyo ili kuchangia ujenzi huo.

Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Jesca Kishoa alipokuwa anachangia jioni hii nilimpa pongezi kwa elimu anayopewa. Ukweli ni kuwa, Mheshimiwa Jesca Kishoa huo ulikuwa ni utafiti wake mwenyewe na anajifundisha mwenyewe, nampongeza kwa mchango mzuri ambao yeye mwenyewe ameufanyia *research. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.15 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 22 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*